Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

# OFISI YA WAZIRI MKUU

# BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI MEI 2017 MPAKA MEI 2018

JUNI, 2018

# OFISI YA WAZIRI MKUU

# BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SERA YA TAIFA YA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI MEI 2017 MPAKA MEI 2018

JUNI, 2018

# Yaliyomo


**1.0. BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI ........ 1**
1.1. UTANGULIZI ........ 1
1.2. DIRA ........ 1
1.3. DHAMIRA ........ 1
1.4. AMALI ZA BARAZA ........ 2
1.5. MAJUKUMU ........ 2
1.6. WAJUMBE WA BARAZA ........ 2
1.7. UONGOZI WA SEKRETARIATI YA BARAZA ........ 4
1.8. MUUNDO NA WAFANYAKAZI WA SEKRETARIATI ........ 6
1.9. TEKNOLOJIA, HABARI NA MAWASILIANO ........ 6

**2.0. UKUAJI WA UCHUMI ........ 8**
2.1. HALI YA SASA YA UCHUMI ........ 8
2.2. PATO LA TAIFA ........ 10
2.3. MCHANGO WA KISEKTA KATIKA PATO LA TAIFA ........ 10

**3.0. SERA NA SHERIA ........ 12**
3.1. SERA ZINAZOFANYIWA MAPITIO HIVI SASA ........ 13

**4.0. MAZINGIRA YA BIASHARA ........ 15**

**5.0. SEKTA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI ........ 19**
5.1. MAPITIO YA SERA ........ 19
5.2. UMILIKISHAJI WA ARDHI MIJINI NA VIJIJINI ........ 20
5.3. PROGRAMU YA KURASIMISHA NA KUZUIA UJENZI HOLELA MIJINI (2013–2023) ........ 20
5.4. PROGRAMU YA KUWEZESHA UMILIKISHAJI ARDHI VIJIJINI (2014 – 2019) ........ 20
5.5. UPATIKANAJI WA ARDHI KWA AJILI YA KILIMO NA UFUGAJI ........ 21
5.6. MIKOPO YA UJENZI WA NYUMBA ........ 21
5.7. UJENZI WA NYUMBA BORA NA ZA GHARAMA NAFUU ........ 22
5.8. NYUMBA ZA GHARAMA NAFUU ZA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA ........ 23

**6.0. MAENDELEO YA USHIRIKA ........ 25**
6.1. HALI YA VYAMA VYA USHIRIKA NA IDADI YA WANACHAMA ........ 25
6.2. HALI YA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA MIKOA 6 ILIYOHAKIKIWA ........ 27
6.3. MAFUNZO KWA VYAMA VYA USHIRIKA ........ 28
6.4. CHANGAMOTO ........ 29

**7.0. UWEKEZAJI WA MITAJI KATIKA SOKO LA HISA (DSE) ........ 31**
7.1. SHUGHULI ZA UENDESHAJI WA SOKO LA HISA KWA MWAKA 2017/18 ........ 31
7.2. UUZAJI NA UNUNUZI WA DHAMANA ........ 33
7.3. ONGEZEKO LA IDADI YA WAWEKEZAJI ........ 33
7.4. UTEKELEZAJI WA SHERIA YA EPOCA ........ 33

7.5. KUKAMILISHA UTAFITI WA BIDHAA NA HUDUMA MPYA SOKONI ....34
7.6. KUANDAA MPANGO MKAKATI ....34
7.7. KUANZISHA KAMPUNI TANZU ....34
7.8. ELIMU KWA UMMA NA UHAMASISHAJI ....34

**8.0. MIFUKO YA UWEZESHAJI NA PROGRAMU ZA MITAJI....36**
8.1. MAELEZO KUHUSU MIFUKO....38

**9.0. VIKUNDI VYA KIFEDHA VYA KIJAMII....49**
9.1. UKUAJI WA VIKUNDI VYA KIFEDHA VYA KIJAMII ....49
9.3. SERA YA TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA KIFEDHA YA MWAKA 2017....51
9.4. MAADHIMISHO YA SIKU YA VICOBA TANZANIA....52

**10.0. USHIRIKIWA WATANZANIA KATIKA UWEKEZAJI (LOCAL CONTENT)....54**
10.1. UJENZI WA UBORESHAJI WA BARABARA YA JUU (FLYOVER) TAZARA: ....54
10.2. UJENZI WA BARABARA ZA JUU UBUNGO (UBUNGO INTERCHANGE) ....55
10.3. MRADI WA PILIPILI WELL-1 ....56
10.4. MRADI WA UJENZI WA RELI (STANDARD GAUGE RAILWAY)....56
10.5. MTAMBO WA KUZALISHA GESI WA MNAZI BAY ....56
10.6. MRADI WA SONGAS ....57
10.7. MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI KUTOKA HOIMA UGANDA MPAKA CHONGELEANI TANGA ....57
10.8. KAMPUNI YA WILLIAMSON DIAMONDS LIMITED....57
10.9. KAMPUNI YA SHANTA MINING CO. LTD ....58
10.10. KAMPUNI YA ANGLO GOLD ASHANTI- GEITA GOLD MINE (AGA-GGM)....59
10.11. KAMPUNI YA STAMIGOLD BIHARAMULO MINE....59
10.12. KAMPUNI YA BULYANHULU GOLD MINE LTD ....59
10.13. KAMPUNI YA NORTH MARA GOLD MINE LTD ....60
10.14. KAMPUNI YA PANGEA MINERALS LIMITED....60
10.15. TAFITI NA MIKUTANO ....60

**11.0. UWEZESHAJI WA WAKULIMA NA VIWANDA....63**
11.1. KURATIBU WAKULIMA WA NJE WA MIWA KWA AJILI YA KIWANDA CHA MKULAZI....63
11.2. KUUNGANISHA WAKULIMA WA MAENBE NA KIWANDA CHA AZAM....64
11.3. KUSHIRIKIANA NA TASAF KUWAINGIZA WANANCHI KUTOKA KAYA MASKINI KWENDA SHUGHULI KIUCHUMI....65

**12.0. UJASIRIAMALI ....67**
12.1. KAMATI YA TAIFA YA MAENDELEO YA UJASIRIAMALI ....67
12.2. MKAKATI WA TAIFA WA UJASIRIAMALI....67
12.3. KURATIBU MAENDELEO YA BIASHARA YA SEKTA NDOGO NA YA KATI....69

**13.0. UWEZESHAJI WA VIJANA....72**
13.1. PROGRAMU YA KIJANA JIAJIRI ....72
13.2. PROGRAMU YA KIJANA JIANDALIE AJIRA ....73

13.3. WIKI YA VIJANA KITAIFA ....73
13.7. MAFUNZO KWA WAHITIMU WA VYUO ....74
13.8. KUTENGA MAENEO YA VIJANA ....74
13.9. PROGRAMU YA KUKUZA UJUZI ....74
13.10. MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA (YDF) ....74
13.11. PROGRAMU YA MAFUNZO YA UJASIRIAMALI KWA VIJANA WA JKT....74
13.12. MASHIRIKA YASIYOKUWA YA KISERIKALI ....75

**14.0. UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI....77**
14.1. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI ....77
14.2. PROGRAMU YA KUSAIDIA WANAWAKE MKOA WA KIGOMA ....79
14.3. Utekelezaji wa Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake ....80

**15.0. MANUNUZI YA UMMA ....82**
15.1. MWONGOZO WA KUSHIRIKISHA MAKUNDI MAALUM KATIKA MANUNUZI YA UMMA ....82
15.2. MFUMO WA MANUNUZI KWA MTANDAO "TANEPS" ....83
15.3. USHIRIKI WA WANANCHI KUPITIA MIRADI YA MATENGENEZO YA BARABARA VIJIJINI ....83
15.4. FAIDA ZA USHIRIKISHWAJI WA WANANCHI....83
15.5. USHIRIKISHWAJI WA WADAU KATIKA DHANA YA USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA MANUNUZI YA UMMA....84

# 1.0. BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI

## 1.1. UTANGULIZI

Tangu Tanzania ipate uhuru mwaka 1961, Serikali imekuwa ikifanya juhudi mbalimbali ili wananchi waweze kushiriki kikamilifu katika kujenga uchumi wa nchi yao. Jitihada hizo ni pamoja na Azimio la Arusha ambalo liliweka njia kuu za uchumi mikononi mwa wananchi, Vijiji vya Ujamaa, Kilimo cha Kufa na Kupona. Dira ya Taifa ya mwaka 2025 inalenga kuwa ifikapo mwaka 2025 sehemu kubwa ya uchumi wa nchi iwe inamilikiwa na watanzania wenyewe. Ili kufikia malengo hayo serikali ilibuni na kutekeleza Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unasimamiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ambalo ni chombo cha juu Kitaifa cha kusimamia, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli zilizoanishwa katika sera hiyo.

Baraza ni taasisi ambayo ipo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu limeundwa kwa mujibu wa sheria ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004. Lengo la Sera hii ni kuwawezesha watanzania kushiriki kikamilifu katika kujenga na kumiliki uchumi wa nchi yao.

Baraza lilizinduliwa rasmi mwezi Novemba, 2005, na lilianza rasmi utekelezaji wa majukumu yake mwezi Mei 2007 baada ya kuundwa kwa Sekretarieti ya Baraza ambayo ni nyenzo ya utekelezaji wa majukumu ya Baraza.

## 1.2. DIRA

Dira ya Baraza ni kuongoza kimkakati katika kuwezesha, kuratibu, kusimamia, kufuatilia na kutathmini shughuli zote zinazolenga kuwawezesha Wananchi wa Tanzania Kiuchumi.

## 1.3. DHAMIRA

Kuwaongoza watanzania kuelekea uchumi imara kupitia uimarishaji wa mazingira ambayo ni rafiki kwa wafanyabiashara kwa ujumla na kuhamasisha ushiriki wa jamii kwenye shughuli halali za kiuchumi.

## 1.4. AMALI ZA BARAZA

Katika kutekeleza majukumu yake Baraza linaamini katika:-

| | | |
|---|---|---|
| Uwazi | Umahiri | Uwajibikaji |
| Usawa | Uadilifu | Umoja |

## 1.5. MAJUKUMU

Majukumu ya Baraza yametokana na maudhui yaliyoainishwa katika Sera ya Uwezeshaji na Sheria ya Uwezeshaji ya mwaka 2004. Majukumu makuu ya Baraza ni:

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuwapatia watanzania fursa za kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi; | 2. | Kuandaa Mpango Mkakati wa kisekta na wa Sekta mbalimbali wa upatikanaji na matumizi ya raslimali kwa shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi; |
| 3. | Kuhamasisha na kuhimiza uwekaji wa Akiba, Uwekezaji na Ushirikishwaji makini wa Wananchi kwenye shughuli za kiuchumi; | 4. | Kuandaa Mkakati wa kitaifa wa Uraghibishi wa sekta mbalimbali wa shughuli za uwezeshaji wananchi kiuchumi; |
| 5. | Kuendeleza na kuwezesha shughuli za kibiashara zinazoanzishwa na kuendeshwa na watanzania; | 6. | Kuainisha fursa za mafunzo ya kiuchumi na uwekezaji na kuratibu programu za mafunzo hayo; |
| 7. | Kusimamia, kuongoza na kutafuta vyanzo vya fedha na michango kwa ajili ya Mfuko wa Uwezeshaji; | 8. | Kuhamasisha Utafiti wa shughuli za kiuchumi na kuhimiza ushirikiano na Taasisi za Utafiti; |
| 9. | Kufanya mapitio ya sheria mbalimbali kwa lengo la kutoa mapendekezo ambayo yatalenga kuboresha mazingira ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. | 10. | Kuandaa Mfumo wa kufuatilia maendeleo ya shughuli za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na kutathmini matokeo; na Mfumo wa Menejimenti ya Habari za Uwezeshaji; |
| 11. | Kushauri kwenye shughuli zote za uanzishaji wa vikundi, ushirika, ushirikiano na ushirikiano wa biashara wa muda mfupi. | 12. | Kuanzisha mfumo wa utoaji taarifa za uwezeshaji wa wananchi kiuchumi kutoka sekta zote; |

## 1.6. WAJUMBE WA BARAZA

Hili ni Baraza la nne (4) tangu kuanzishwa kwa Taasisi hii. Wajumbe wa Baraza waliteuliwa mnamo tarehe 17 Desemba, 2016. Baraza la sasa lina wajumbe tisa (9) ikiwa ni pamoja na mwenyekiti. Baraza limeundwa na wajumbe wenye uzoefu wa fani mbalimbali kama vile Viongozi wa Serikali Wastaafu, Wanataaluma, Watafiti, Wafanyabiashara na Taasisi Zisizokuwa za Serikali za maendeleo ya wananchi. Wajumbe hao wa Baraza pamoja na picha zao ni:-



**Dkt. John Kiang'u Jingu, *Mwenyekiti wa Baraza***

Ni Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya Sayansi ya Siasa na Utawala. Vilevile ni Mkurugenzi wa Kituo cha Taaluma za Mikakati na Amani (Center for Strategic & Peace Studies) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Pia, ni Mhadhiri Mchagizi wa masomo ya Utawala na Elimu katika Chuo Kikuu cha Limerick kilichopo nchini Ireland. Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, alimteua Dkt. John Jingu, kuwa Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi, Disemba 2016.

**Profesa Samuel M. Wangwe, *Mjumbe***



Ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya REPOA. Mwenyekiti wa Bodi ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) na Tume ya Ushindani wa Biashara (FCC). Pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa DAIMA Ltd (Daima Associates Limited). Mshauri wa sera katika ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, aliwahi kuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Masuala ya Uchumi (Economic and Social Research Foundation - ESRF).

Amewahi kuwa mjumbe wa kamati ya nne ya kuandaa Mpango wa miaka mitano wa viwanda na teknolojia; Kamati ya kuboresha ukusanyaji wa takwimu za kitaifa; Mwenyekiti wa kamati ya kitaifa ya ushauri wa uanzishwaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.



**Profesa Lucian A. Msambichaka, *Mjumbe***

Ni Profesa Mstaafu wa Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam katika masuala ya Uchumi wa kilimo. Mwenyekiti wa Bodi ya Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW) na ni Mwenyekiti wa Bodi ya Benki ya Biashara DCB. Alikuwa Mwenyekiti Mwanzilishi wa Bodi ya Bima ya Afya (NHIF), Mwenyekiti Mwanzilishi wa Bodi ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Usihirika na Biashara (MUCCoBS), Moshi na Mkurugenzi Mwanzilishi wa Kituo cha Ushauri cha Chuo Kikuu cha Dar-es-Salaam.

Pia aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo cha Uwekezaji (TIC) na Kaimu Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Alikuwa Mshauri Mkuu na Mwezeshaji Kiongozi wa "Majadiliano ya Ushirikiano kwa Manufaa ya Wote (Global Smart Partnership Dialogue)" na Mshauri Mkuu na Mwezeshaji Kiongozi wa "Majadiliano ya Kitaifa Kuhusu Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Tanzania".

**Bw. Ladislaus J. Mwamanga, *Mjumbe***



Ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Rais wa kusaidia kaya maskini (Social Action Fund - TASAF). Kabla ya kujiunga TASAF alifanyakazi Shirika la Petroli Tanzania (Tanzania Petroleum Development Corporation - TPDC), Benki ya Taifa ya Biashara (National Bank of Commerce - NBC); Oil Marketing Company na Total Tanzania Limited (1994 – 1999).



**Dkt. Frederick S. Ringo, *Mjumbe***

Ni Wakili wa Mahakama Kuu ya Tanzania na ni Mhadhiri Mwandamizi wa Shule ya Sheria katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam katika masuala ya sheria ya biashara na fedha. Aliwahi kuwa Afisa Sheria Mkuu (PSRC), Mkuu wa kitengo cha Huduma za Kisheria (Africa Export-Import Bank -Cairo) na Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Ushindani wa Biashara (Fair Competition Commission). Ni mwanachama wa Taasisi ya Wasuruhishi wa Migogoro (UK na Tanzania).

**Bibi Anna T. Maembe, *Mjumbe***



Ni Katibu Mkuu mstaafu kutoka Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, akiwa hapo alifanya mambo mengi ya kimkakati kwa ajili ya wanawake na watoto. Cheo hiki alidumu nacho kati ya mwaka 2011 mpaka 2015. Amekuwa mtumishi wa umma kwa kipindi cha miaka 34. Ameshiriki kuongoza masuala mengi ya Serikali ikiwamo kuongoza Bodi mablimbali za Taasisi za Umma. Pia ametoa machapisho mbalimbali katika masuala ya utunzaji wa mazingira na kutoa ushauri kwa Taasisi mbalimbali za ndani na nje ya nchi. Yeye ni mbobezi katika masuala ya mazingira.



**Dkt. Augustine Y. Hangi, *Mjumbe***

Ni Mwenyekiti Mtendaji wa kampuni ya Madini (Mineral Resources Company Limited). Ametoa shauri mbalimbali zinazohusiana na masuala ya madini. Kabla ya kushika nafasi yake ya sasa, Dkt. Augustine Y. Hangi alikuwa kaimu Mkurugenzi wa London-based Diamond Sorting Organization (TANSORT). Aliwahi pia kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Madini Tanzania (STAMICO) kwa miaka 13 mpaka mwaka 2004. Tangu mwaka 2009 mpaka sasa amekuwa akifanya kazi na Chuo Kikuu Huria (Open University of Tanzania) kama msimamizi wa wanafunzi wanaosomea shahada ya uzamili. Kabla ya hapo alikuwa mhadhiri wa chuo hicho kati ya mwaka 2007 na 2009. Kwa hivi sasa pia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Mineral Resources Company Limited, Aliwahi kuwa Mjumbe wa bodi ya Tanzania Minerals Audit Agency na pia mjumbe wa bodi ya Williamson Diamonds Limited.

**Dkt. Astronaut Bagile, *Mjumbe***

Ni Mkurugenzi Mtendaji na mwanzilishi wa shirika lisilo la kiserikali la Women In Social Entrereneurship (WISE). Amefanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali ya kitaifa na kimataifa kwa miaka 25 akichangia kuinua hali za uchumi za wananchi husan makundi yaliyo na hali duni zaidi kama wakulima, wanawake, vijana na watoto. Ni mjumbe wa bodi wa shirika la kimataifa linalojihusisha na utafiti wa masuala ya kijinsia na wanawake Afrika (AAWORD) lililo na makao yake Senegal. Pia ni Mjumbe wa bodi wa shirika lisilo la kiserikali lijulikanalo kama SCODIA.





**Bibi Neema M. Kiure, *Mjumbe***

Ni Mkaguzi Mshiriki Mwenza wa Ernst & Young (EY). Aliungana na Ernst & Young (EY) tangu mwaka 2005. Kabla ya hapo alifanyakazi na Diamond Trust Bank (T) Limited kama Meneja wa Fedha na Utawala mnamo mwaka 2004. Pia aliwahi kufanya kazi na PriceWaterhouseCoopers (PwC) kama Mkaguzi manmo mwaka 2004 na pia alifanyakazi na ULC (Tanzania) Limited kama Mhasibu Mkuu mnamo mwaka 2000.

Pia hufundisha masomo ya Utawala Bora wa wakurugenzi wa makampuni uliothibitishwa na Jumuiya ya Madola, amewahi kufundisha masomo ya muda maalum kwa ajili ya kujiandaa na mitihani ya Uhasibu. Ni mjumbe wa bodi ya Wahasibu na Wakaguzi wa (NBAA) na ni mjumbe wa bodi wa Shirikisho la Kimataifa la Wahasibu (IFAC). Alikuwa kiongozi wa Mradi wa kuhakikisha Serikali inaweza kuingia kwenye mfumo wa Kanuni za Kimataifa za Uaandaji wa hesabu katika taasi za umma (IPSAS).

## 1.7. UONGOZI WA SEKRETARIATI YA BARAZA

Kwa mujibu kifungu cha 14 cha sheria ya uwezeshaji ya mwaka 2004, Menejimenti ya Baraza inaongozwa na Katibu Mtendaji ambaye huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Baraza huajiri Wakurugenzi na Mameneja. Kwa sasa timu ya Menejimenti ina watumishi wafuatao:-



**Bibi Beng'i M. Issa, *Katibu Mtendaji***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 4 Desemba, 2014. Pia ni Katibu wa Baraza. Kabla ya uteuzi huo alifanya kazi Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania (Tanzania Commission For AIDS - TACAIDS) kama Mkurugenzi wa Fedha, Utawala na Utafutaji Rasilimali kwa miaka 12. Pia alikuwa Mdhibiti wa Fedha wa Taasisi ya CARE International Tanzania kwa miaka 3. Aliwahi kuwa mhadhiri wa masuala ya fedha na uhasibu katika kilichokuwa Chuo cha Uongozi wa Maendeleo (IDM Mzumbe) sasa Chuo Kikuu kwa kipindi cha miaka 9 (1992 -2000). Ni Mwenyekiti wa Bodi za Benki ya Wanawake (TWB) na Taasisi ya Ushindani ya Ujasiriamali Tanzania (TECC). Vilevile ni makamu mwenyekiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Mafuta na Gesi (PURA). Aliwahi kuwa Mjumbe wa Bodi ya Benki ya DCB na ni mjumbe wa bodi ya Tanzania Women Chamber of Commerce (TWCC).

**Bi Anna D. Lyimo*, Mkurugenzi wa Uwezeshaji***



Kabla ya kuteuliwa nafasi hii mwezi Octoba, 2014, alikuwa afisa mkuu mwandamizi wa utetezi na uraghbishi (Advocacy and Publicity) tangu mwaka 2007 wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kabla ya kujiunga na Baraza, alifanyakazi kama mchumi katika Ofisi ya Rais Mipango na Ubinafsishaji na Wizara ya Mipango, Uchumi na Uwezeshaji kutoka Januari 2005 mpaka Agosti 2007. Amefanyakazi pia katika Taasisi ya uchunguzi wa afya ya Ifakara ambayo sasa inajulikana kama Ifakara Health Research and Development Centre (Januari 2004 – Agosti, 2005). Ni mjumbe wa bodi wa Taasisi ya Ushindani ya Ujasiriamali Tanzania (TECC).



**Bw. Edwin Chrisant, *Mkurugenzi wa Mifuko ya Uwezeshaji***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo tangu mwezi Octoba, 2014. Kabla ya hapo alikuwa afisa mkuu mwandamizi wa Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi tangu mwaka 2011 mpaka mwaka 2014 katika Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kabla ya kujiunga na Baraza, alifanyakazi kama meneja uhusiano CRDB Microfinance Services Company Limited (2008-2011); Mpango wa huduma za kifedha Vijijini (Rural Financial Services Programme - RFSP) toka mwaka 2005-2008 na Pride Tanzania kama Afisa Mikopo kuanzia mwaka 2000 mpaka 2005.

**Bw.Suleiman M. Malela*, Kaimu Mkurugenzi wa Fedha na Utawala***



Aliteuliwa kushika nafasi hiyo mwezi Octoba, 2016. Kabla ya uteuzi huo Bw.Suleiman M. Malela alikuwa mkuu wa kitengo cha Ukaguzi wa Ndani kutoka mwezi Octoba, 2008 alipoajiriwa na Baraza mpaka mwezi Octoba, 2016.Kabla ya kujiunga na Baraza, Bw. Malela alifanya kazi Shirika la Bima la Taifa Tanzania (National Insurance Corporation - NIC) katika nafasi mbalimbali kuanzia mwaka 1993 mpaka 2008.



**Bw. Samwel Kiondo*, Kaimu Mkurugenzi wa Sera, Mipango, Utafiti na Ufuatiliaji na tathmini***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo mwaka, 2015. Kabla ya uteuzi huo alikuwa Afisa Mkuu katika Idara ya Bajeti ya Serikali, Wizara ya Fedha na Mipango kutoka mwaka 1997 mpaka 2015. Pia alifanya kazi Tume ya Mipango kati ya mwaka 1991 mpaka 1997 kama Afisa Mipango. Ni mjumbe wa bodi wa Mamlaka ya Hali ya Hewa.

**Bi Esther B. Mmbaga*, Kaimu Mkurugenzi wa Ushiriki wa Watanzania Kwenye Uwekezaji***

Aliteuliwa kushika nafasi hiyo mwaka, 2015. Pamoja na uteuzi huo Bi Esther pia ni Mkuu wa Kitengo cha Sheria kutoka mwaka 2007 alipoajiriwa na Baraza. Ni mjumbe wa bodi ya Taasisi ya watoa huduma kwenye tasnia ya mafuta na gesi (ATOGS). Kabla ya kujiunga na Baraza, Bi Esther alifanya kazi katika idara ya mahakama kama Hakimu Mkazi toka mwezi Mei, 2003 mpaka mwezi Aprili, 2007.



## 1.8. MUUNDO NA WAFANYAKAZI WA SEKRETARIATI

Uratibu wa utekelezaji wa Sera ya Uwezeshaji na shughuli zake unafanywa na Sekretarieti ambayo inaongozwa na Katibu Mtendaji. Wakati inaanzishwa, Sekretarieti ya Baraza iliidhinishiwa kuwa na watumishi 40. Kwa kipindi cha Mei, 2017 mpaka Aprili, 2018 Sekretarieti ilikuwa na watumishi 29, kati yao wanaume ni 17 na wanawake ni 12. Watumishi 26 ni wa ajira ya kudumu na malipo ya uzeeni, mtumishi 1 ni wa ajira ya mkataba, na watumishi 2 ni wa ajira ya muda maalum.

## 1.9. TEKNOLOJIA, HABARI NA MAWASILIANO

Kutokana na mwongozo wa serikali wa Wakala wa Serikali Mtandao, Taasisi zote za serikali zinatakiwa kutumia vituo vya Serikali kuhifadhi taarifa, tovuti, n.k. Kwa tafsiri sahihi vituo vikuu vya Serikali kwa sasa ni *seva za Wakala wa Serikali Mtandao* na *"data center"* za Serikali zilizoko wizara ya Ujenzi na Mawasiliano. Baraza liko katika hatua za mwisho kabisa kutekeleza maagizo haya, baada ya kuwasiliana na Wakala wa Serikali Mtandao.

Katika kufanikisha uhamishaji huu wa tovuti ya Uwezeshaji, Wakala wa Serikali Mtandao ilifanya mapitio ya tovuti ya sasa ya Baraza na kutoa ushauri kwamba itengenezwe upya ili iendane na sifa muhimu zinazohitajika kwa ajili ya tovuti za Serikali.

Baraza vilevile limeanza kutengeneza tovuti kwa ajili ya mawasiliano ya utekelezaji wa programu ya ushiriki wa watanzania (Local Content) kwenye miradi mbalimbali ya serikali. Mfano wa miradi hii ni kama; Bomba la Mafuta kutoka Uganda mpaka Tanga, Ujenzi wa Bandari Bagamoyo, Miradi yote ya mafuta na gesi, Ujenzi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge Railway), Mradi wa Umeme wa Rufiji (Stiglers Gorge) ujenzi wa Fylovers, Uchimbaji wa Madini n.k.

Baraza lilijiunga na huduma ya intaneti ya Mkongo wa Taifa tangu mwaka 2014. Mkongo wa Taifa wa mawasiliano ambao unatoa huduma ya intaneti inayosimamiwa na Wakala wa Serikali Mtandao ikishirikiana na TTCL ambayo husambaza huduma hiyo. Imesaidia Baraza kujiunga na Mfumo wa Barua Pepe Serikalini mwaka huohuo.



# UKUAJI WA UCHUMI

# 2.0. UKUAJI WA UCHUMI

Dira ya maendeleo ya Taifa ya 2025 ni kuona kwamba ifikapo mwaka 2025 Tanzania inakuwa na uchumi wa kati na unaomilikiwa na watanzania wengi zaidi wenye maisha bora, amani, utulivu, ustawi, ubunifu na wenye elimu. Ili kufikia maono hayo Serikali ya Tanzania iliandaa Sera, Sheria na Mikakati mbalimbali yenye lengo la kuwezesha ukuaji wa uchumi na kuwawezesha watanzania kuboresha maisha yao. Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 ni moja ya sera ambazo zinahakikisha kwamba wananchi wanashiriki na kunufaika na fursa mbalimbali za kiuchumi zilizopo nchini kwa kuwapatia upendeleo zaidi katika uwekezaji, utoaji wa zabuni za serikali pamoja na kutunga sera za kisekta, kanuni na mikakati mbalimbali ili kuwezesha utekelezaji wa dira ya taifa yenye lengo la kuwawezesha watanzania kumiliki sehemu kubwa ya uchumi wa nchi yao. Baadhi ya mikakati iliyowekwa na Serikali kwa lengo la kuwawezesha wananchi kiuchumi ni pamoja na kuwawezesha wananchi kuzalisha bidhaa bora kwa gharama za chini au zinazolingana na za ushindani; kuzielekeza sera za kisekta katika kuwawezesha wananchi kushiriki kikamilifu katika uchumi; kuweka na kutekeleza sera na mikakati madhubuti ya kuendeleza mauzo katika masoko ya Kanda ya Afrika na masoko ya dunia; kujenga uwezo wa wananchi ili waweze kumudu uwekezaji katika mazingira ya soko huria na ushindani na kuvutia wawekezaji kuingia nao ubia; kutenga maeneo maalum kwa kila sekta kwa ajili ya shughuli za kiuchumi zitakazofanywa na wananchi pamoja na kuweka mazingira rafiki ya kuwawezesha watanzania kupata mitaji ya uwekezaji.

## 2.1. HALI YA SASA YA UCHUMI

Ukuaji wa uchumi unamaanisha kuongezeka kwa pato la taifa na uzalishaji wa bidhaa na huduma katika kipindi husika. Upimaji sahihi wa ukuaji wa uchumi hauzingatii mfumuko wa bei. Ukuaji wa uchumi unawawezesha wawekezaji na wajasiriamali kupata faida kubwa katika biashara pamoja na ukuaji wa mitaji. Ukuaji wa uchumi unaongeza ajira miongoni mwa wananchi na kuboresha maisha ya jamii kwa ujumla. Mojawapo ya vigezo vinavyopima ukuaji wa uchumi katika nchi ni Pato la Taifa.

Ukuaji wa Pato la Taifa ni badiliko la thamani ya bidhaa na huduma zilizozalishwa kutokana na shughuli mbalimbali za kiuchumi katika nchi zilizofanyika katika kipindi husika ikilinganishwa na kipindi sawia

cha nyuma. Shughuli za kiuchumi zinajumuisha kilimo cha mazao, misitu, ufugaji na uvuvi; uzalishaji viwandani; biashara; ujenzi wa nyumba na barabara; huduma za fedha; habari na mawasiliano; usafiri na usafirishaji; huduma za utalii; na utoaji wa huduma nyingine kwa jamii ikiwa ni pamoja na afya, elimu na maji. Kiashiria hiki ni cha msingi kwa sababu kina uhusiano wa moja kwa moja na viashiria vingi vya mwenendo wa uchumi.

Kwa taarifa iliyotolewa na Wizara ya Fedha na Mipango, katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 (Januari – Juni), Pato la Taifa (kwa bei za mwaka husika) liliongezeka na kufikia shilingi milioni 25,535,852 ikilinganishwa na shilingi milioni 23,915,750 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Hata hivyo, katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka 2017, Pato la Taifa lilikua kwa asilimia 6.8 ikilinganishwa na asilimia 7.7 katika kipindi kama hicho mwaka 2016.


Aidha, taarifa ya Kongamano la Uchumi la Dunia (2018) inaonesha kuwa Tanzania inaongoza kwa kuwa na uchumi jumuishi miongoni mwa nchi za Afrika zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. Hii imechangiwa na utekelezaji wa Sera na mipango mbalimbali iliyowawezesha watanzania kushiriki vema na kunufaika na shughuli mbalimbali za kiuchumi. Tanzania pia inashika nafasi ya 48 miongoni mwa nchi zenye uchumi unaokua kwa kasi zaidi duniani kwa sasa. Nchi nyingine kati ya nchi 10 bora zenye uchumi jumuishi duniani pamoja na nafasi zao katika mabano ni Ghana (52), Cameroon (53), Burundi (55), Namibia (56), Rwanda (57), Uganda (59), Mali (60), Senegal (61) na Nigeria (63).

Tanzania ilikuwa ya kwanza katika uchumi jumuishi miongoni mwa nchi za Afrika kwa sababu Tanzania imefungulia fursa za ujasiriamali ambapo kuna zaidi ya biashara za wajasiriamali 3,000,000 kila mwaka. Vilevile mtandao wa miundombinu ya barabara ni mkubwa kiasi cha kuwawezesha wananchi wengi kujishughulisha na shughuli za kiuchumi, huduma za fedha jumuishi ni kigezo ambacho kimeiweka Tanzania mahala pazuri kwenye uchumi jumuishi ambapo zaidi ya watanzania milioni 30 wanajishughulisha na fedha kupitia simu za mkononi na hivyo kuongeza huduma za fedha kufikia asilimia 65%. Vilevile huduma za msingi kama vile elimu na afya pamoja na kupungua kwa rushwa katika utoaji huduma za umma ni kigezo kingine kilichozingatiwa.

Kulingana na taarifa za Shirika la Fedha Duniani (2017) uchumi wa Dunia ulitegemewa kukua kwa viwango vya 3.6% mwaka 2017 na 3.7% mwaka 2018 kutoka 2.6% mwaka 2016. Uchumi wa Ethiopia ulikua kwa kasi zaidi duniani mwaka 2017 kwa kiwango cha 8.3% ambacho ni kiwango cha juu ya wastani wa ukuaji wa uchumi duniani katika kipindi hicho ikifuatiwa na Uzbekistan (7.6%), Nepal (7.5%), India (7.2%), Djibout na Laos (7%), Cambodia, Filipino na Myanmar (6.9%) na China (6.5%).

Ukuaji wa uchumi katika nchi za Africa Mashariki ulikuwa wa wastani wa 5.9% na ulitegemewa kukua kwa kiwango hicho katika mwaka 2018 ukichangiwa zaidi na sekta za kilimo (5%), viwanda na uzalishaji kwa 10.5%. Wachangiaji wakubwa katika ukuaji huu katika nchi za Afrika Mashariki ni Ethiopia, Tanzania, Djibout, Rwanda, Seychelles na Kenya. Mchango wa Tanzania, Kenya na Rwanda katika uchumi wa nchi za Afrika Mashariki unategemea kuendelea kukua katika mwaka 2018 kutokana na kuimarika kwa ushirikiano kati ya nchi hizi kupitia Umoja wa Nchi za Afrika Mashariki, Soko la Pamoja la COMESA pamoja na kugunduliwa kwa mafuta na gesi asilia katika nchi za Tanzania, Kenya, Uganda na Ethiopia (Benki ya Maendeleo ya Afrika, 2017).

***Mchoro 1: Hali ya ukuaji wa uchumi kwa kulinganisha mwaka 2016 na 2017***




***Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu; na CIA World Factbook***

Aidha, katika kipindi cha Januari hadi Desemba 2017, mfumuko wa bei ulipanda hadi 5.3% kutoka 5.2% katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Kupanda kwa mfumuko wa bei huku kulichangiwa na kuongezeka kwa bei za vyakula na bidhaa zisizokuwa vyakula (NBS, 2017).

## 2.2. PATO LA TAIFA

Pato la Taifa katika mwaka limekuwa kwa wastani wa 6.8% katika nusu ya kwanza ya mwaka 2017 kiwango ambacho ni chini ya kiwango cha ukuaji wa wastani wa 7.0% katika mwaka 2016 pamoja na maoteo ya Serikali ya ukuaji wa Pato la Taifa kwa 7.2%. Ukuaji mdogo wa Pato la Taifa umechangiwa na ukuaji mdogo wa shughuli za uzalishaji na za kiuchumi katika kipindi hiki kama vile kilimo, biashara, mauzo ya nje ya bidhaa mbalimbali na ungizaji wa bidhaa toka nje (Benki Kuu, 2017).

## 2.3. MCHANGO WA KISEKTA KATIKA PATO LA TAIFA

Sekta zilizochangia katika ukuaji wa uchumi katika kipindi hiki ni pamoja na ujenzi, usafirishaji, uzalishaji, madini, teknolojia na mawasiliano ambazo kwa pamoja zimechangia ukuaji wa uchumi kwa 67.4% (Benki Kuu, 2017). Msingi mkubwa wa ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote ni matokeo yake yaonekane kwa wananchi wake. Ili kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi iweze kuwanufaisha wananchi wengi sharti wananchi wengi wawe wanafanya kazi katika sekta zinazokua haraka ili kujipatia kipato. Lakini ilivyo hapa nchini kwa sasa wananchi wengi wanaishi vijijini na wanategemea kilimo ambacho kasi ya ukuaji wake bado ni ndogo (asilimia 2.1 mwaka 2016) kutokana na tija ndogo na kutegemea mvua. Sekta zinazokua haraka (Ujenzi 13%, Habari & Mawasiliano 13%, Usafirishaji na Uhifadhi wa Mizigo 11.8%, Uchimbaji wa Madini na Mawe 11.5%, Shughuli za Fedha na Bima 10.7%) haziajiri wananchi wengi. Vilevile kasi ya ongezeko la watu hapa nchini ni kubwa (2.7% kwa mwaka) na hivyo inatengeneza idadi kubwa ya watu kugawana Pato dogo la Taifa.



# SERA NA SHERIA

# 3.0. SERA NA SHERIA

Sera na Sheria zina nafasi kubwa ya kuhakikisha kuwa mipango na mikakati ya nchi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na kuinua uchumi wa nchi inatekelezwa. Katika kipindi cha Julai 2017 hadi Machi 2018 Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa imepitisha na kufanyia marekebisho Sheria zifuatazo:-

1. **Sheria ya Mamlaka ya Nchi Kuhusiana na Umiliki wa Maliasili ya mwaka 2017**

   Sheria hii ilitungwa ili kulinda maliasili ya Taifa. Sheria imeainisha kwamba mapato yote yanayotokana na utafutaji, uchimbaji, umiliki na utumiaji wa rasilimali za Tanzania yanahifadhiwa katika taasisi za kifedha za ndani ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Aidha, Sheria hii pia inazuia usafirishaji wa maliasili bila kuongeza thamani, lengo likiwa ni kuleta maendeleo na kutekeleza azma ya Serikali ya kuwa Tanzania ya viwanda.

2. **Sheria ya Mapitio na Majadiliano kuhusu Masharti Hasi katika Mikataba inayohusu Maliasili ya Mwaka 2017**

   Sheria hii ilitungwa ili kuhakikisha kuwa rasilimali na maliasili za Tanzania zinalindwa na kunufaisha wananchi kiuchumi na nchi kiujumla. Hivyo mikataba na makubaliano yoyote yanayohusu rasilmali na maliasili inaweza kufanyiwa mapitio na Bunge ili kujiridhisha kwamba masharti yaliyomo kwenye mikataba pamoja na mambo mengine imezingatia maslahi ya watanzania. Masharti hayo yatachukuliwa kuwa hasi iwapo pamoja na mambo mengine yatakuwa yamewanyima watanzania haki ya kunufaika kiuchumi kutokana na rasilmali na maliasili inayopatikana hapa nchini.

3. **Sheria ya Madini ya mwaka 2010** imefanyiwa marekebisho na ***Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act, 2017*** ambayo imeongeza tafsiri ya *Local Content* na kutoa kipaumbele kwenye ununuzi na utoaji huduma kwa watanzania au makampuni ya kitanzania, ajira na kujenga uwezo wa watanzania katika sekta ya madini. Sheria hii imeelekeza kwamba wenye leseni ya

uchimbaji madini wanatakiwa kutoa kipaumble kwenye ununuzi wa bidhaa au huduma kwa kampuni au wananchi wa kitanzania. Kama kampuni ya kitanzania haina uwezo wa kutosha basi bidhaa au huduma zitolewe na kampuni ya kitanzania iliyoingia ubia na kampuni ya nje ambapo hisa za kampuni ya kitanzania haitapungua 25% au vinginevyo kama itakavyoainishwa kwenye Kanuni. Aidha, Tume ya Madini imepewa jukumu la kufuatilia ushiriki wa watanzania katika sekta ya madini na masuala ya *Corporate Social Responsibility*.

4. Kanuni za Ushiriki wa Watanzania kwenye sekta ya madini "*The Mining (Local Content) Regulations, 2018*" zimeeleza kwa ufasaha jukumu la mwekezaji kwenye sekta ya madini kushirikisha watanzania. Malengo ya Kanuni hii ni pamoja na:-
   - Kuongeza thamani kwenye uchumi wa nchi kutokana na utumiaji wa bidhaa, huduma na nguvu kazi za kitanzania katika mnyororo mzima wa thamani katika sekta ya madini;
   - Kuongeza ushindani wa biashara za ndani,
   - Kuweka mfumo wa wazi wa ufuatiliaji;
   - Kuongeza ujuzi wa watanzania katika sekta ya madini;
   - Kuanzisha viwanda vinavyohusu sekta ya madini hasa katika uongezaji wa thamani ya madini n.k.

**5. Sheria ya Bima ya mwaka 2009** imefanyiwa marekebisho na sheria ya ***Written Laws (Miscellaneous Amendment) Act, 2017,*** marekebisho hayo yamelenga kuhakikisha kwamba janga lolote la mtanzania au kampuni iliyopo Tanzania linakatiwa bima na kampuni ya bima ya kitanzania. Marekebisho haya yataongeza ushiriki wa kampuni za bima Tanzania katika uwekezaji unaofanyika hapa nchini. Pia Kampuni za Madalali wa Bima zinatakiwa kuwa na angalau moja ya tatu ya hisa za kampuni zinazomilikiwa na watanzania na Menejimenti ya kitanzania ili kuwajengea uwezo watanzania katika kufanya kazi za bima.

6. Kanuni za Ushiriki wa Watanzania katika Tasnia ya Mafuta na Gesi ilikamilika na kutangazwa kwenye Gazetti la Serikali kwa Tangazo namba 197 ya tarehe 5 Mei 2017. Kanuni hizi zimeanza kutumika rasmi mwezi Novemba, 2017 zikiwa na malengo yafuatayo:-
   - Kuhakikisha thamani inaongezwa kwenye uchumi wa nchi kupitia ajira ya watanzania, ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwenye kampuni za kitanzania kwenye mnyororo mzima wa thamani kwenye sekta ya mafuta;
   - Kuendeleza ujuzi wa watanzania kwenye mnyororo mzima wa thamani wa mafuta kupitia elimu, uhamishaji wa tekinolojia, utafiti na ubunifu;
   - Kuhakikisha malengo yaliyoainishwa kwenye kanuni kuhusu ajira na ununuzi wa bidhaa na huduma yanatekelezwa kikamilifu;
   - Kuongeza uwezo na ushindani wa biashara za watanzania; na
   - Kuanzisha viwanda vinavyohusu sekta ya mafuta ili kujenga uchumi endelevu.

**7. Sheria ya Tanzania Shipping Agencies Cooperation Act, 2017** ilipitishwa na Bunge Novemba 2017 ili kusimamia Sekta ya usafiri wa majini Tanzania bara. Katika sheria hii kifungu cha 13 kinaelezea kwamba mtu yeyote atapewa leseni ya Wakala wa Meli kama mtu huyo ni raia wa Tanzania na kama ni kampuni basi iwe imesajiliwa Tanzania chini ya Sheria ya Makampuni na 60% ya hisa za umiliki ziwe zinashikiliwa na raia wa Tanzania.

## 3.1. SERA ZINAZOFANYIWA MAPITIO HIVI SASA

Sera zifuatazo zinafanyiwa mapitio zikiwa na malengo pamoja na mambo mengine kuwawezesha wananchi kiuchumi:-

1. Sera ya Ujenzi, 2003 (The Construction Industry Policy, 2003)
2. Sera ya Taifa ya Utalii, 1999 (The National Tourism Policy, 1999)
3. Sera ya Taifa ya Maliasili, 1998 (Tanzania National Forestry Policy, 1998)
4. Sera ya Wanyamapori 2007 (The Wildlife Policy of Tanzania, 2007)




# MAZINGIRA YA BIASHARA

# 4.0. MAZINGIRA YA BIASHARA

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2017/18 Serikali ya Tanzania imechukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuboresha mazingira ya biashara ili kuwawezesha watanzania kufanya biashara kwa urahisi zaidi. Taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka 2018 imepima mazingira ya biashara kwa nchi za kiafrika katika maeneo ya idadi ya siku katika kuanzisha biashara mpya, utoaji wa vibali vya ujenzi, kupata umeme kwenye eneo husika, kusajili ardhi au mali, kupata mkopo, kulinda uwekezaji, kulipa kodi, kufanya biashara mipakani, kuingia mikataba na muda wa kumaliza masuala ya ufilisi. Taarifa hiyo inaiweka Tanzania katika nafasi ya 137 (alama za ubora 54.04%) kati ya nchi 190 duniani kwenye vigezo vya wepesi wa kufanya biashara ikilinganishwa na nafasi ya 132 (alama za ubora 54.48%) katika mwaka 2017 na nafasi ya 139 (alama za ubora 51.62%) mwaka 2016. Matokeo haya yanaonesha kuwa, Tanzania imefanya vizuri zaidi (54.04%) juu ya wastani wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (50.43%) kwa ubora katika mazingira ya biashara kwa mwaka 2018 ikilinganishwa na matokeo ya mwaka 2016 ambapo ilifikia viwango vya ubora 51.62% juu ya wastani wan chi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (49.66%) katika kipindi hicho. Katika kigezo cha urahisi wa kuanzisha biashara Tanzania imeshika nafasi ya 162 ikiwa na alama 73.03% kuelekea ubora zaidi wa mazingira ya kufanyia biashara. Kiwango hiki ni chini ya kiwango cha wastani 76.82%) cha nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara.


***Mchoro 2: Vigezo vya upimaji mazingira ya biashara***




*Chanzo: Taarifa ya Benki ya Dunia*

Aidha, Tanzania imepanda kwa nafasi 108 kwa ubora zaidi katika urahisi wa kufanya biashara kutoka nafasi ya 152 hadi 44 katika urahisi wa kupata mikopo miongoni mwa wajasiriamali katika mwaka 2017. Hii imechangiwa na ongezeko la taasisi zinazotoa mikopo kutumia huduma za kanzi data ya taarifa za wakopaji (*credit bureau)* katika kuongeza ufanisi wa utoaji wa mikopo. Matumizi ya kanzi data ya taarifa za wakopaji (*credit bureau)* yameongeza idadi ya wakopaji kutoka 4.97% hadi 6.48% ya watanzania watu wazima. Matumizi ya kanzi data pia yamewezesha kusainiwa kwa makubaliano kati ya taasisi kubwa za fedha na wakopeshaji wadogo (retailers and merchants). Pia, katika mwaka 2017, Tanzania imefanikiwa kuongeza ufanisi katika kuingiza na kusafirisha bidhaa nje ya nchi kwa kuanzisha Mfumo wa Kielectroniki wa kuwezesha kupokea na kutoa mizigo/bidhaa nchini kupitia Mamlaka ya Mapato (TRA). Pia, Serikali imerahisisha ufanyaji wa biashara kwa kurahisisha upatikanaji wa leseni kwa biashara zinazoanza na kushika nafasi ya 87 duniani katika kigezo cha kupata huduma ya umeme. Hata hivyo, katika mwaka 2017, Tanzania haikufanya vizuri kwenye uboreshaji wa mazingira ya biashara kwa kuanzisha tozo za kodi kwenye masuala ya fedha (*money transfers*) pamoja na kuongeza gharama ya upatikanaji wa vibali vya ujenzi (Benki ya Dunia, 2017). Aidha, mwaka 2018 Tanzania haikufanya vizuri kwenye kigezo cha uanzishaji wa biashara kwa kushika nafasi ya 162 na kupata alama za ubora 73.03% ambazo ni chini ya wastani wa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara (76.82%).

***Mchoro 3: Nafasi ya kila nchi kwenye mazingira ya biashara***




*Chanzo: Benki ya Dunia, 2018.*

Serikali ya Tanzania sasa hivi inafanya utaratibu wa kuboresha mazingira ya biashara kwa kufuata mwongozo ambao umetengenezwa (*blue print*) ili kuongoza utaratibu mzima wa maboresho ya kimfumo kwenye mazinigra ya biashara. Mwongozo huu vilevile utasaidia kuelekeza katika utengenezaji wa programu ambazo zitatekeleza na kufuatilia maboresho hayo. Mwongozo huu kama utatumika vizuri utaiwezesha Tanzania kuwa na mageuzi makubwa ya kisheria na kisera yatakayowezesha uendeshwaji bora wa biashara pamoja na kuweka ushindani mzuri wa kibiashara. Wakala wa Usajili wa Biashara (BRELA) tayari imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa kusajili biashara ambao utazinduliwa hivi karibuni. Vilevile Kituo cha Uwekezaji cha Tanzania (TIC) kimeboresha utendaji wa usajili wa wawekezaji kwa kuleta pamoja taasisi zote (*one stop centre*) ambazo zinahusika na kuwezesha na kurahisisha usajili wa wakezeji hapa nchini.



# SEKTA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

# 5.0. SEKTA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ina mchango mkubwa siyo tu katika kufanikisha utekelezaji wa dhana na misingi ya kuwezesha wananchi kiuchumi bali hata kuongeza ushiriki wa watanzania kunufaika na huduma za sekta ya ardhi, nyumba na maendeleo ya makazi. Kwa kutambua umuhimu huu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa II wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2015-2020; Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (2004) pamoja na miongozo mbalimbali ya Serikali.

Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha wa 2017/18, Sekta ya Ardhi imetekeleza shughuli mbalimbali za kuwezesha wananchi kiuchumi katika sekta ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.

## 5.1. MAPITIO YA SERA

Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995 na kuandaa Rasimu ya marekebisho ya Sera hiyo kwa kushirikiana na wataalam washauri kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Ardhi na sekta binafsi. Kwa ujumla, madhumuni ya mapitio ya Sera hiyo ni kuweka misingi ya kukabiliana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ardhi ya mwaka 1995. Lengo la marekebisho hayo ni kuimarisha usalama wa milki, kuboresha mazingira ya uwekezaji katika sekta ya ardhi, kudhibiti migogoro ya matumizi ya ardhi pamoja na uhakikisha kwamba kila kipande cha ardhi kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa.
Kadhalika, Wizara inaendelea na mapitio ya Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Makazi ya mwaka 2000 ili kuihuisha na kutayarisha rasimu ya Sera ya Nyumba. Wizara imepanga kuendelea kuelimisha umma kuhusu sera, sheria, kanuni na taratibu zinazosimamia sekta ya ardhi.

Sekta ya Ardhi inakabiliwa na baadhi ya changamoto za kasi ya ongezeko la idadi ya watu na mifugo ikilinganishwa na upatikanaji wa ardhi iliyopangwa na kupimwa; ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia

stahiki kwa ardhi iliyotwaliwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo; na uelewa mdogo wa wananchi kuhusu sera na sheria za ardhi.

Wizara imeainisha mikakati mbalimbali itakayotekelezwa ili kukabiliana na changamoto hizo. Katika kuimarisha usalama wa milki pamoja na kuongeza kasi ya kupima na kupanga ardhi, Wizara imekamilisha mapitio ya Sera ya Taifa ya mwaka 1995 kwa kushirikiana na wadau mbalimbali nchini. Kwa ujumla, madhumuni ya mapitio ya Sera hiyo ni pamoja na kuziba mianya au viashiria vya migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya watumiaji nchini, kuongeza kasi ya upimaji, upangaji na umilikishaji wa kila kipande cha ardhi na kuwawezesha wananchi wasio na ardhi vijijini kumiliki ardhi kwa shughuli za kilimo na ufugaji na kujenga mazingira bora yanayovutia uwekezaji nchini.

Vilevile, ili kupunguza au kudhibiti migogoro inayosababishwa na ucheleweshaji wa ulipaji wa fidia stahiki na kwa wakati, Serikali imeunda Bodi ya Mfuko wa Fidia ya Ardhi kwa ajili ya kuratibu masuala yote ya fidia nchini yakayofanywa na wizara na taasisi mbalimbali.

## 5.2. UMILIKISHAJI WA ARDHI MIJINI NA VIJIJINI

Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi imeendelea kuhakikisha kuwa kila kipande cha ardhi nchini kinapangwa, kupimwa na kumilikishwa. Halmashauri mbalimbali kwa kushirikiana na sekta binafsi zimekamilisha miradi ya upimaji wa viwanja katika miji, takriban asilimia 60 ya wananchi wanaoishi mijini wanaishi katika maeneo ambayo hayajapangwa. Hali hii imewafanya wananchi kutofikiwa na miundombinu ya kiuchumi na hivyo wananchi kukosa usalama wa miliki.
Katika mwaka wa fedha 2017/18 Serikali imeendelea kuhimiza ushiriki wa sekta binafsi katika kupanga na kupima ardhi ili kuongeza kasi ya utoaji wa milki za ardhi nchini. Ushiriki wa sekta binafsi unaongeza fursa za ajira, kuongeza mapato ya Serikali yatokanayo na kodi ya pango la ardhi na kukuza pato la Taifa.

Kuna programu mbalimbali ambazo zipo kwenye mipango na mikakati ya kutekelezwa kwa lengo la kufanikisha utekelezaji wa masuala ya uwezeshaji wananchi kiuchumi. Baadhi ya programu hizo ni pamoja na Programu ya Kurasimisha na Kuzuia Ujenzi Holela Mijini (2013–2023) na Mpango wa Kupanga, kupima na kumilikisha ardhi Vijijini (2014 – 2019)

## 5.3. PROGRAMU YA KURASIMISHA NA KUZUIA UJENZI HOLELA MIJINI (2013–2023)

Programu hii ina miradi ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambapo jukumu la Wizara ni kuandaa mipango ya Urasimishaji, upimaji na umilikishaji ardhi katika maeneo yaliyojengwa kiholela kwa kushirikiana na wananchi.
Katika utekelezaji wa programu hii mafanikio yamepatikana kwa jumla ya viwanja 120,000 vimepimwa katika Halmashauri mbalimbali. Kati ya hivyo viwanja 18,000 tayari vimemilikishwa na mchakato wa kuhakikisha maeneo mengi yamepimwa unaendelea. Mbali na mafanikio pia kuna changamoto mbalimbali zinazokabili miradi ya uwezeshaji wananchi baadhi ya hizo changamoto ni gharama za kupanga, kupima na kumilikisha ardhi bado zipo juu hususan malipo ya tozo ya mbele (*Premium*). Katika mapendekezo ya maboresho, Wizara inakusudia kupunguza tozo ya mbele (kiwango cha Premium) ambayo hutozwa wakati wa kumilikisha ardhi kutoka asilimia 7.5 mpaka asilimia 2.5 ya thamani ya ardhi.

## 5.4. PROGRAMU YA KUWEZESHA UMILIKISHAJI ARDHI VIJIJINI (2014 – 2019)

Mpango wa kuwezesha kupanga, kupima na kumilikisha ardhi vijijini 2014 – 2019 (*Land Tenure Support Programme*). Unatekelezwa katika Wilaya za mfano za Kilombero, Ulanga na Malinyi na kuwezesha Umilikishaji Ardhi chini ya ufadhili wa Serikali ya nchi za Uingereza, Sweden na Denmark kupitia Mashirika yao ya Maendeleo ya DFID, SIDA na DANIDA.

Katika mwaka wa fedha 2017/18 Wizara kupitia Programu hii inaendelea kufanya uhakiki wa vipande

vya ardhi 80,000 na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya vijiji 37; kujenga ofisi za ardhi katika wilaya za Kilombero (1), Ulanga (1) na Malinyi (1); na kuandaa vyeti vya ardhi vya vijiji 15 katika wilaya za Kilombero, Ulanga na Malinyi.
Aidha, katika usimamizi wa ardhi ya wawekezaji, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imefanya ukaguzi wa mashamba ya uwekezaji 121 yenye ukubwa wa ekari 552,139.21 yaliyopo katika Mikoa ya Tanga, Morogoro, Pwani, Njombe na Kagera na kuingiza taarifa zake katika kanzidata ya Wizara. Kati ya mashamba haya, 63 yameendelezwa na 58 yametelekezwa. Kwa mashamba ambayo hayajaendelezwa, hatua za kisheria zitaendelea kuchukuliwa. Katika mwaka wa fedha 2017/18. Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Taifa ya Takwimu itafanya uhakiki wa mashamba ya uwekezaji nchini.

Katika utekelezaji wa programu hii jumla ya Viwanja 17,696 Vimepangwa na kupimwa katika vijiji 20 katika Wilaya za Kilombero (16) Ulanga (4) Wananchi Wametumia Hati ya Hakimiliki za Kimila (CCRO) kupata mikopo yenye jumla ya Tzs 49.62 bilioni kutoka Benki mbalimbali zikiwemo NMB Plc, CRDB Plc, Stanbic Bank Plc, PSPF, Agriculture Trust Fund Bank, Meru Community Bank na Mfuko wa Pembejeo. Changamoto inayokabili programu hii ni upungufu wa Wataalamu katika Halmashauri, na vitendea kazi.

Wizara ina mpango wa kuongeza idadi ya wataalamu katika Halmashauri kwa kutumia wahitimu kutoka Chuo Kikuu Ardhi, Chuo cha Ardhi Tabora na Morogoro

## 5.5. UPATIKANAJI WA ARDHI KWA AJILI YA KILIMO NA UFUGAJI

Katika Vijiji 12,545 vilivyosajiliwa, asilimia kumi na tatu (13%) tu ya vijiji vimendaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi.
Kupitia mradi wa Land Tenure Support Programme (LTSP- 2014 -2019) Wizara ipo katika mchakato wa kuandaa Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi kwa Vijiji vyote.

Licha ya changamoto zinazoikabili sekta ya ardhi, wizara imefanikiwa kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya jumla ya vijiji 1,764 sawa na 13 %. Aidha, zaidi ya Halmashauri za Wilaya 110 zimepatiwa mafunzo ya namna ya kuandaa Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ili kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kilimo na ufugaji.

Sekta ya Ardhi inapanga kuboresha Mamlaka za Upangaji kuweka katika mipango ya maendeleo tengeo kwa kazi husika, kusogeza huduma kwa wananchi kupitia Ofisi za Ardhi za Kanda nane zilizoanzishwa na Tume ya Matumizi Bora ya ardhi kukamilisha Mkakati wa Kitaifa wa kuongeza kasi ya uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi.

## 5.6. MIKOPO YA UJENZI WA NYUMBA

Kwa sasa wananchi walio wengi wanajenga nyumba kupitia akiba zao binafsi katika ujenzi na wanatumia muda mrefu takriban miaka kumi (10). Aidha, uelewa wa wananchi bado ni mdogo kwenye eneo la mikopo ya ujenzi wa nyumba.

Mipango na mikakati iliyopo kwa sasa inaonyesha kuna programu mbili (2) zinazotekelezwa ambazo kwa Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC) na Mikopo Midogo midogo ya nyumba (Housing Micro financing Fund).

**a) Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC)**

Kuundwa kwa Tanzania Mortgage Refinancing Company (TMRC) inayokopesha Benki za Biashara mtaji kwa ajili ya mikopo ya nyumba kunatafsiriwa kama ni jitihada za makusudi zinazolenga kuwezesha wananchi kunufaika na fursa za mikopo ya ujenzi wa nyumba. Ujenzi

wa nyumba za kuuza na kupanga (Real Estate Development Projects) utawezesha wananchi kuboresha hali za maisha na hatimaye kuendelea kuchangia mapato kwa maendeleo ya Taifa.

Mikopo ya ujenzi wa nyumba imefanikiwa kwa benki za biashara 54 kwa sasa zinatoa huduma ya mikopo nyumba kwa wananchi. Kati ya hizo benki 30 zimetoa mikopo ya nyumba yenye jumla ya Tshs. bilioni 446.33 kwa wananchi wapatao 3,915. Changamoto zilizopo ni Riba kubwa inayotozwa na Benki za Biashara (18%-19%), Kipato kidogo cha wananchi walio wengi, Ukosefu wa ajira na kipato cha uhakikika kwenye kufanya marejesho ya mikopo, na uelewa mdogo na uthubutu wa wananchi.

**b) Mfuko wa Mikopo Midogo midogo ya nyumba (Housing Micro financing Fund)**

Katika mwaka wa fedha 2017/18 kupitia mradi wa Housing Micro Financing Project ilipata mtaji wa kutoa mikopo midogo midogo ya nyumba Kiasi cha Dolla za Marekani 18.0 chini ya Usimamizi wa Benki Kuu ya Tanzania. Mradi huu unalenga kuboresha kanzidata ya nyumba nchini kwa kujumuisha taarifa za soko la nyumba kama vile bei za nyumba na kodi ya pango la nyumba. Aidha, Wizara inaratibu uandaaji wa mwongozo na viwango vya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu (Guidelines and Standards for Affordable Housing) lengo ni kuwa na viwango vya ujenzi wa nyumba za watu wa kipato cha chini nchini.

Mpaka kufikia Aprili 2018, jumla ya taasisi za fedha tano (5) zimekuwa zikitoa huduma ya mikopo midogo midogo ya nyumba kupitia mradi huu kwa lengo la kuwawezesha wananchi kunufaika kiuchumi kupitia sekta ya nyumba. Taasisi hizo za fedha ni Benki ya **DCB, Yetu Microfinance, EFC Bank, MUCOBA Bank PLC**, na **Mkombozi Commercial Bank**. Jumla ya wananchi wapatao 574 wamepatiwa na kunufaika na mikopo yenye jumla ya Tsh. 10.0 Bilioni. Kwa upande wa changamoto zinazokabili mradi huu ni Riba inayotozwa na Taasisi za fedha bado ni kubwa (17-18%), Masharti ya mkopo bado magumu hususan dhamana kwa Taasisi za Fedha na wananchi wanaokopeshwa na Uelewa mdogo wa wananchi.

**c) Mikopo ya nyumba kwa watumishi wa Serikali**

Wizara inasimamia Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali ulioanzishwa kupitia Waraka wa Serikali Na. 8 wa mwaka 1992. Lengo la Mfuko huo ni kuwawezesha watumishi kupata mikopo ya kujenga, kukarabati ama kununua nyumba. Katika mwaka 2017/18 Wizara inaendelea kupokea na kushughulikia maombi mapya na kukusanya marejesho kulingana na taratibu za mfuko.

Mfuko huu ulianzishwa kwa lengo la kukopesha Watumishi 500 kila mwaka. Ni wastani wa Watumishi 100 wanaweza kupatiwa mikopo kwa mwaka, Kiwango cha juu cha mkopo ni Tsh. 20 milioni, riba asilimia tatu na muda wa juu wa marejesho ni miaka 30.

Mfuko umejielekeza katika kufuatilia marejesho kutoka kwa wakopaji ili kuongeza mtaji utakaowezesha kuongeza wigo wa kuwafikia wanufaikaji walio wengi. Aidha, watumishi wamenufaika na mikopo ingawaje kiasi ni kidogo kikilinganishwa na gharama halisi za ujenzi.

Jumla ya Watumishi wapatao 1,669 wamenufaika na kupatiwa mikopo yenye jumla ya Tsh. 12.55 bilioni hadi kufikia Aprili 2018. Changamoto ni ukosefu wa mtaji wa kutosha kulipa watumishi wanaostaili kupatiwa mikopo pamoja na kiasi kinachotolewa kwa wakopaji ni kidogo ikilinganishwa na gharama za ujenzi wa nyumba.

## 5.7. UJENZI WA NYUMBA BORA NA ZA GHARAMA NAFUU

Kutokana na kutopangwa vizuri, maeneo mengi yaliyojengwa nyumba yanakosa huduma za miundombinu ya msingi ikiwemo barabara, maji safi na uondoshaji wa majitaka, taka ngumu na

umeme. Nyumba zinazojengwa katika maeneo hayo ni duni na za bei ya juu.

Halmashauri zote hapa nchini zimeelekezwa kutenga ardhi na kuweka miundombinu ya msingi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za makazi. Pia Serikali imeanzisha Benki ya Ardhi (Land Bank) pamoja na kuanzishwa kwa Mfuko wa Fidia. Hii yote ni katika kufanikisha malengo ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ambapo sekta binafsi itaendelea kuishirikishwa (kampuni za kupanga na kupima ardhi) katika upangaji na upimaji ardhi.

Kadhalika, tafiti mbalimbali za vifaa vya ujenzi wa gharama nafuu zimefanyika. Teknolojia hizi zimezingatia teknolojia ya ujenzi wenye kupunguza gharama na zimeanza kutumika nchini. Taasisi ya National Housing and Building Research Agency (NHBRA) itaendelea na utengenezaji wa mashine za kutengeneza tofali za kufungamana, vigae vya mkonge vya kuezekea na ujenzi wa dari isiyotumia nondo nyingi (ladies and waffles).

Miradi mbalimbali ya kupanga, kupima na kumilikisha ardhi katika Halmashauri mbalimbali nchini imeendelea kufanyika. Aidha, mashine 133 za tofali za kufungamana na vigae 53,359 zimetengenezwa na Wananchi 173 wamepatiwa mafunzo ya kutumia mashine hizo katika wilaya mbalimbali. Baadhi ya changamoto za jumla zilizoanishwa ni pamoja na:-

- Mawasiliano hafifu na udhibiti kati ya Sekta Binafsi na Mamlaka za upangaji
- Wamiliki wa ardhi kutokuwa tayari kutoa ardhi kwa ajili ya huduma za jamii
- Mamlaka za Upangaji kukosa fedha kwa ajili ya uwekaji wa miundombinu ya msingi ikiwemo barabara, maji na umeme
- Mwitikio mdogo wa wananchi kutumia vifaa vya ujenzi vinavyozalishwa na kutengenezwa
- Uhaba wa rasilimali fedha na watu kufanya tafiti na kusambaza matokeo ya tafiti husika.

### 5.8. NYUMBA ZA GHARAMA NAFUU ZA SHIRIKA LA NYUMBA LA TAIFA

Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya mwaka 2004 kwa vitendo umehakikisha Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) linajenga nyumba kwa ajili ya kupangisha (30%) na kuuza (70%) kwa wananchi. Kadhalika, sekta ya ardhi imetekeleza ujenzi wa nyumba za gharama nafuu katika maeneo mbalimbali nchini na Shirika la Nyumba la Taifa. NHC liliweka Mpango Mkakati wa kujenga nyumba 50,000 (2010 – 2015)

Mafanikio yalipatikana kwenye mradi wa nyumba za gharama nafuu zinazojengwa na shirika la nyumba la Taifa ambapo:

- Jumla ya nyumba 1,686 za matumizi mbalimbali zimejengwa
- Miradi 14 ya nyumba za gharama nafuu yenye nyumba 492 imeendelea kutekelezwa
- Miradi 10 ni ya nyumba za gharama ya kati na juu yenye nyumba 881;na miradi 4 ni ya nyumba za biashara na nyumba 229
- Jengo moja la matumizi mchanganyiko lenye nyumba 84.
- Jumla ya miradi 25 yenye jumla ya nyumba 4,126 inaendelea kujengwa nchini
- Nyumba za gharama nafuu 300 zinajengwa Iyumbu Dodoma

Changamoto kubwa ni pamoja na riba kubwa ya mikopo kutoka Benki za Biashara ambazo ndio zinaendesha mikopo ya nyumba, vipato vidogo vya wananchi kumudu gharama za mikopo ya nyumba kutoka Benki washirika wa NHC na ukosefu wa miundombinu katika maeneo ambayo NHC wanajenga nyumba hivyo hufanya gharama za nyumba kuwa kubwa.

Mapendekezo ya Maboresho ni pamoja na majadiliano ya kupunuza riba katika mikopo yanaendelea, Halmashauri kutenga ardhi na kuweka miundombinu muhimu ikiwemo barabara na Mamlaka za huduma ya maji na umeme zipeleke huduma hizo katika maeneo yanayoendelezwa na Shirika.



# MAENDELEO YA USHIRIKA

# 6.0. MAENDELEO YA USHIRIKA

Hadi kufikia mwezi Februari 2018 Tanzania Bara ilikuwa na jumla ya vyama vya ushirika vya aina mbalimbali 10,620. Kati ya hivyo vyama vya ushirika vya mazao (AMCOS) vilikuwa 3338, vyama vya ushirika vya wafugaji nyuki vilikuwa 56, vyama vya ushirika vya walaji (consumer cooperatives) 132, vyama vya ushirika vya wavuvi 85 na vyama vya ushirika vya wenye nyumba vilikuwa 33. Aidha vyama vya ushirika vya wenye viwanda vilikuwa 118, vyama vya ushirika vya umwagiliaji vilikuwa 78, vyama vya ushirika vya muungano vilikuwa 32, vyama vya wafugaji vilikuwa 207, vyama vya wachimba madini vilikuwa 204 na Huduma vyama 157. Vingine ni vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) 5,737, Usafirishaji 24, Benki 13, Muungano (Union) 40, shirikisho (Federation) 2 na vyama vya aina vyingine 364.

## 6.1. HALI YA VYAMA VYA USHIRIKA NA IDADI YA WANACHAMA

Hadi kufikia mwezi Februari 2018 Tanzania Bara ilikuwa na wanachama 2,246,331 kati yao wanaume ni 1,647,100 (73%) na wanawake 599,231 (27%). Aidha kati ya vyama 10,620, vyama 5,291 (49.8%) vilikuwa hai na 5,329 (50.2%) vilikuwa vinasinzia au vimekufa kabisa. Asilimia 56 ya vyama vya ushirika vinavyosinzia nchini ni SACCOS na asilimia 14 ni AMCOS. Pia asilimia 63 ya wanachama wote wa vyama vya Ushirika Tanzania Bara wapo katika SACCOS.


*Jedwali 1: Taarifa ya Vyama vya Ushirika hadi kufikia Februari 2018*

| NA | AINA YA USHIRIKA | WANACHAMA | | JUMLA | HALI | | JUMLA YA VYAMA VYA USHIRIKA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | **Me** | **Ke** | | **Hai** | **Sinzia/ Mfu** | |
| 1 | AMCOS | 636,992 | 134,966 | **771,958** | 1,806 | 1,532 | **3,338** |
| 2 | SACCOS | 963,508 | 445,576 | **1,409,084** | 2,782 | 2,955 | **5,737** |
| 3 | HUDUMA | 1,572 | 796 | **2,368** | 76 | 81 | **157** |
| 4 | MADINI | 8,951 | 3,306 | **12,257** | 148 | 56 | **204** |
| 5 | MIFUGO | 6,879 | 2,596 | **9,475** | 100 | 107 | **207** |
| 6 | MULTPURPOSE | 1,204 | 528 | **1,732** | 52 | - | **52** |
| 7 | NYUKI | 1,995 | 618 | **2,613** | 19 | 37 | **56** |
| 8 | NYUMBA | 2,100 | 348 | **2,448** | 11 | 22 | **33** |
| 9 | UMWAGILIAJI | 8,991 | 4,243 | **13,234** | 40 | 38 | **78** |
| 10 | VYAMA VIKUU | - | - | **-** | 38 | 2 | **40** |
| 11 | USAFIRISAJI | 1,009 | 337 | **1,346** | 8 | 16 | **24** |
| 12 | UVUVI | 1,511 | 706 | **2,217** | 38 | 47 | **85** |
| 13 | VIWANDA | 627 | 559 | **1,186** | 29 | 89 | **118** |
| 14 | WALAJI | 1,780 | 997 | **2,777** | 30 | 102 | **132** |
| 15 | APEX/TFC | - | - | **-** | 1 | 1 | **2** |
| 16 | BENKI | - | - | **-** | 1 | 12 | **13** |
| 17 | JOINT ENTERPRISE | - | - | **-** | 22 | 10 | **32** |
| 18 | VINGINE | 9,981 | 3,655 | **13,636** | 90 | 222 | **312** |
| **Jumla** | | **1,647,100** | **599,231** | **2,246,331** | **5,291** | **5,329** | **10,620** |

*(Chanzo: TCDC 2018)*

Katika chati hapo chini unaweza kuona kwamba vyama vingi vya ushirika ni vile vya kuweka akiba na kukopeshana (SACCOS), vikifuatiwa na vyama vya ushirika kwenye mazao ya kilimo (AMCOS). Ushirika ambao una vyama vichache kabisa ni ule ushirika wa kibenjki ambao una vyama 13 tu.


***Mchoro 4: Jumla ya Vyama vya Ushirika Tanzania Bara***




*(Chanzo: TCDC 2018)*

Katika mchoro hapo chini vyama vingi vya ushirika vinaonesha kusinzia au kufa kabisa.

***Mchoro 5: Hali ya Vyama vya Ushirika Tanzania Bara***





*(Chanzo: TCDC 2018)*

Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) kwa kushirikiana na shirika la ukaguzi wa vyama vya ushirika (COASCO) na Mradi wa MIVARF imeanza kazi ya kuhakiki hali halisi ya vyama vya ushirika Tanzania Bara ambapo hadi June 2017, mikoa 6 kati ya 26 ilikuwa imehakikiwa. Mikoa hiyo ni Dodoma, Kilimanjaro, Mtwara, Mwanza, Njombe na Tabora. Kazi ya uhakiki wa vyama vya ushirika inayoendelea nchini ina lengo la kupata takwimu sahihi za vyama nchini. Takwimu hizi zitapatikana mara baada ya kazi ya uhakiki kumalizika.

## 6.2. HALI YA VYAMA VYA USHIRIKA KATIKA MIKOA 6 ILIYOHAKIKIWA

Taarifa ya uhakiki wa vyama vya ushirika katika mikoa hiyo inaonesha kuwa vyama 2,842 vilihakikiwa. Kati ya hivyo, vyama 1,105 (39%) vilikuwa hai, vyama 962 (34%) vilikuwa vimesinzia (dormant) na vyama 775 (27%) havikupatikana. Aidha taarifa inaonesha kuwa idadi ya wanachama ilikuwa 438,790 kati yao wanaume ni 290,961 (66.3%), wanawake ni 137,148 (31.3%), vikundi 9,777 (2.2%) na taasisi 904 (0.2%). Vyama vilivyohakikiwa katika mikoa hii pia vilikuwa vimetoa ajira kwa watu 1,104 kati yao wanaume ni 580 na wanawake ni 524.


***Mchoro 6: Hali ya Vyama vya Ushirika vilivyohakikiwa***




*(Chanzo: TCDC na COASCO Uhakiki 2017)*

Katika mchoro hapo chini, kama ambavyo ingetegemewa wananchama wengi wapo katika SACCOS, ikifuatiwa na AMCOS. Vyama vya ushirika vyenye wanachama wachache kabisa ni vyama vya ushirika wa viwanda.


***Mchoro 7: Idadi ya Wanachama wa Vyama vya Ushirika Tanzania Bara***




*(Chanzo: TCDC 2018)*

Mchoro hapo chini unaonesha idadi ya wananchama kijinsia katika vyama vya ushirika, ambapo wanachama wengi ni wanaume kwa asilimia 73  na wanawake kwa asilimia 23.

***Mchoro 8: Idadi ya Wanachama wa Vyama vya Ushirika Kijinsia***




*(Chanzo: TCDC 2018)*

## 6.3. MAFUNZO KWA VYAMA VYA USHIRIKA

Hadi Februari 2018, Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini ilikuwa imefanya mafunzo mbalimbali kwa vyama vya ushirika nchini. Mafunzo hayo yaliyotolewa kwa wanachama na viongozi wa vyama vya ushirika 1,166 kati yao wanaume 777 na wanawake 389 yalijumuisha;

a) Dhana ya ushirika kwa vyama vya ushirika

b) Mfumo na muundo wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika

c) Maadili na Utawala Bora

d) Utunzaji wa vitabu vya ushirika kwa mujibu wa Sheria ya Ushirika Namba 6 ya mwaka2013

e) Mzunguko wa kiuhasibu (Accounting cycle)

f) Uwekezaji ndani ya ushirika kwa mujibu wa sheria ya vyama vya ushirika

g) Uundaji wa mpango mkakati wa Biashara

h) Ujasiriamali na uibuaji wa miradi

i) Utunzaji wa kumbukumbu ndani ya vyama vya ushirika.

## 6.4. CHANGAMOTO

Changamoto zinazovikabili vyama vingi vya ushirika nchini ni pamoja na ugumu wa upatikanaji wa takwimu sahihi unaotokana na utunzaji mbovu wa kumbukumbu za vyama, baadhi ya viongozi wa vyama kukosa elimu na ujuzi wa kutosha kusimamia vyama vya ushirika, migogoro kwa baadhi ya vyama baina ya viongozi na wananchama, kukosekana kwa uaminifu na uadilifu kwa baadhi ya viongozi na wafanyakazi, hali inayopelekea upotevu wa mali za wanaushirika, marejesho duni ya mikopo kwa baadhi ya wakopaji ndani ya vyama vya ushirika, ukosefu wa fedha za usimamizi wa vyama kwa maafisa ushirika katika mikoa husika na ukosefu wa masoko ya bidhaa zinazozalishwa na wanaushirika na hivyo kuchangia marejesho duni ya mikopo.




# UWEKEZAJI WA MITAJI KATIKA SOKO LA HISA (DSE)


# 7.0. UWEKEZAJI WA MITAJI KATIKA SOKO LA HISA (DSE)

Kama ilivyo kwa masoko ya hisa duniani kote, jukumu kuu la Soko la Hisa ni kuwezesha upatikanaji wa fedha za mitaji ya muda mrefu na za miradi ya umma na hivyo kutoa fursa ya uwekezaji na utekelezaji wa miradi kwa upande unaohitaji mtaji. Kwa kufanya hivyo, Soko linawezesha pia uuzaji na ununuzi wa dhamana (hisa na hatifungani) kwa njia ya uwazi kulinganisha namna nyinginezo zilizoko nje ya mfumo huu. Aidha, soko la hisa pia hutumika kama nyenzo ya utekelezaji wa sera za fedha na maendeleo na pia kuwapa wananchi fursa ya kushiriki katika umiliki wa uchumi wa nchi yao.

## 7.1. SHUGHULI ZA UENDESHAJI WA SOKO LA HISA KWA MWAKA 2017/18

Katika kipindi cha kuanzia Mwezi Julai mwaka 2017 hadi Mwezi Aprili mwaka 2018, shughuli za uendeshaji wa soko la hisa Dar es Salaam (DSE PLC) ziliendelea kama kawaida, jukumu kuu likiwa ni kuwezesha upatikanaji wa fedha za muda mrefu za mitaji na utoaji wa fursa za uwekezaji kwa wawekezaji wa ndani na nje ya nchi.

Hadi kufikia Mwezi Aprili 2018, jumla ya **kampuni 27** zilikuwa zimeorodheshwa; 20 zikiwa ni kampuni za ndani na saba **(7) kampuni za nje.**




*Jedwali 2: Orodha ya Kampuni zilizoorodheshwa Sokoni*

| KAMPUNI ZA NDANI | KAMPUNI ZA NJE |
|---|---|
| CRDB Benki | ACACIA |
| MuCoBa Bank PLC | |
| Benki ya biashara ya DCB | KCB Group |
| Kampuni ya Sigara (TCC), | |
| YETU microfinance bank, | Uchumi Supermarket |
| Mkombozi Commercial Bank Plc (MKCB) | |
| Mwalimu Commercial Bank PLC | Jubilee Holdings Limited |
| TOL Gas limited | |
| VodaCom Tanzania | East African Breweries Limited (EABL) |
| Precision Air Services Plc | |
| Tanzania Breweries, | Nation Media Group (NMG) |
| TCCIA Investment PLC | |
| Kampuni ya TATEPA | Kenya Airways Limited |
| The Dar es Salaam Stock Exchange (DSE) | |
| Maendeleo Bank Plc (MBP), | |
| Kiwanda cha Cement cha Twiga | |
| Swiss port Tanzania PLC | |
| Swala Oil and Gas (Tanzania) plc ("Swala"), | |
| National Microfinance Bank Plc (NMB), | |
| Tanga Cement Company | |

*Chanzo: Soko la Hisa la DSM*

Kwa upande wa Hatifungani za Serikali (Government bonds), katika kipindi hiki, Serikali iliorodhesha hatifungani zenye thamani ya **shilingi bilioni 2,453** hii ni sawa na **ongezeko la asilimia 50** kulinganisha na hatifungani za Serikali za **shilingi bilioni 1,635** zilizoorodhoshwa Mwaka 2016. Kwa ujumla, hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa sokoni hadi Mwezi wa **Aprili 2018 ni shilingi bilioni 8,613.**




*Chanzo: Soko la Hisa la DSM*

Kwa upande wa hatifungani za Makampuni binafsi (corporate bonds), hadi kufikia Mwezi Aprili 2018, hatifungani za Kampuni zenye thamani ya **shilingi bilioni 122** zilikuwa zimeorodheshwa katika soko.


Kuhusu thamani ya hisa zilizopo sokoni (Total Market Capitalization) ilikuwa ni **shilingi bilioni 23,435.** Kati ya hizi, jumla ya **shilingi bilioni 10,751** ni kwa makampuni **20** ya ndani.

## 7.2. UUZAJI NA UNUNUZI WA DHAMANA

Uuzaji na ununuzi wa dhamana (hisa na hatifungani) hufanywa kwa uwazi na huru hivyo kuwezesha utambuzi wa thamani ya uwekezaji kwa wawekezaji wa aina mbalimbali.

Kwa kipindi hiki hadi Mwezi Aprili 2018, hisa zenye thamani ya **shilingi bilioni 516 ziliuzwa na kununuliwa.** Hii ni sawa na ongezeko la **asilimia 23** ikilinganishwa na hisa zenye **thamani ya shilingi bilioni 421** zilizouzwa na kununuliwa katika Mwaka wa 2016.

*Chati : Ununuzi wa Hisa*




*Chanzo: Soko la Hisa la DSM*

Kwa upande wa hatifungani, katika Mwaka 2017 hatifungani zenye thamani **ya shilingi bilioni 981** ziliuzwa na kununuliwa. Hili ni ongezeko la takribani **asilimia 130** ikilinganishwa na hatifungani zenye thamani ya **shilingi bilioni 426** zilizouzwa na kununuliwa katika kipindi cha Mwaka 2016.

## 7.3. ONGEZEKO LA IDADI YA WAWEKEZAJI

Hadi kufikia Aprili 2018, DSE ilikuwa na jumla ya **akaunti za uwekezaji 530,182.** Hii ni ongezeko la **asimilia 12 ikilinganishwa na idadi ya 472,195 katika Mwaka 2016.**

Kwa ujumla mwenendo mzuri wa uendeshaji wa soko kwa mwaka 2017 ukilinganisha na mwaka 2016, pamoja na mambo mengine, mwenendo mzuri wa uchumi wa nchi na hali ya utulivu wa kisiasa ni vitu vilivyochangia kuendelea kwa shughuli za wawekezaji, hasa wawekezaji toka nje kuendelea kuwekeza katika soko letu.

## 7.4. UTEKELEZAJI WA SHERIA YA EPOCA

Kama sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya EPOCA, inayoyataka makampuni ya simu kuuza asilimia 25 ya hisa kwa umma na kujiorodhesha katika soko la hisa, DSE iliweza kuorodhesha kampuni ya Vodacom Tanzania Ltd iliyouza hisa zenye thamani ya **shilingi bilioni 476.**

Hisa hizo zimeuzwa kwa jumla ya **Watanzania 41,475** hiyo ni mpaka kufikia mwezi Aprili mwaka huu. Aidha, DSE ilipokea maombi mengine kutoka kampuni nne za simu (4) ambazo ni **Tigo, Zantel, Halotel na Airtel** maombi ambayo yako katika hatua mbalimbali za mchakato wa kupata ruhusa ya kuorodheshwa ikiwa ni baada ya kukamilisha zoezi la uuzaji wa hisa kwa umma kupitia soko la awali.

## 7.5. KUKAMILISHA UTAFITI WA BIDHAA NA HUDUMA MPYA SOKONI

Kwa kuzingatia uchache wa kampuni zilizoko sokoni, DSE kwa msaada wa Benki ya Dunia, kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, iliwezesha kufanyika utafiti wa namna ya kuongeza idadi ya kampuni, bidhaa na huduma mbalimbali katika soko. Lengo likiwa kuongeza mchango wa sekta ya masoko ya mitaji katika kukuza na kuendeleza uchumi. Utekelezaji wa mapendekezo ya utafiti huo unaanza mwaka huu wa 2018.

## 7.6. KUANDAA MPANGO MKAKATI

DSE iliweza kukamilisha uandaji wa Mpango Mkakati wa Miaka Mitano 2018 – 2022. Mpango huu pamoja na mambo mengine umeanisha maeneo ya mkakati ambayo utekelezaji wake utalifanya soko la hisa kutoa mchango zaidi katika utelekezaji wa sera za maendeleo ya uchumi wa nchi na kijamii. Kwa kuwezesha upatikanaji wa fedha za mitaji za muda mrefu na wakati kwa Sekta umma na Sekta binafsi.

## 7.7. KUANZISHA KAMPUNI TANZU

Ikizingatiwa kuwa Tanzania ni nchi inayohitaji mitaji toka nje na pia kwa kuzingatia matakwa ya taasisi inayosimamia shughuli za masoko ya mitaji ulimwenguni yaani International Organization Securities Commission (IOSCO), DSE iliweza kubadilisha idara yake ya Hifadhi za Dhamana (Securities Depository Department) kuwa kampuni kamili ili kutenganisha shughuli za uuzaji na ununuzi wa dhamana na hifadhi ya dhamana, kama inavyotakiwa na IOSCO.

## 7.8. ELIMU KWA UMMA NA UHAMASISHAJI

Soko la Hisa liliendelea na uendeshaji wa Shindano kuhusu uwekezaji kwa Wanafunzi waliopo vyuo vikuu – **DSE Scholar Investment Challenge.** Lengo la shindano hili ni kuleta uelewa na hamasa kuhusu uwekezaji kwa kada ya vijana wasomi ambao wanategemewa baadaye kuwa watungaji wa Sera, waendeshaji wa shughuli za biashara (makampuni) au wajasiriamali n.k. Programu hii iliendeshwa katika vyuo vikuu vyote vinavyotambulika na Serikali na **kunufaisha idadi ya vijana 12,455.**

❖ DSE iliendelea na kushirikiana na tasnia ya habari ikiwa ni nyenzo rahisi na madhubuti katika kufikisha elimu na hamasa ya uwekezaji kwa umma. DSE ilifanya hivyo kwa kutoa taarifa za kila wiki na pia kutoa machapisho na maandiko katika magazeti pamoja na kufanya vipindi vya radio na luninga.

❖ DSE iliendelea na mpango mkakati wake wa kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa (Local Government Authorities) kuhusu uwezekano wa Mamlaka hizi kutumia masoko ya hisa kupata fedha za miradi ya maendeleo kwa kutoa hatifungani za serikali za mitaa yaani *Municipal Bonds*. Mpaka kufikia mwezi April mwaka huu zoezi hili limeweza kuzifikia **Halmashauri 6 za Tanzania Bara ambazo ni Kinondoni, Tanga, Ilemela, Mwanza, Arusha na Ilala.**

❖ DSE iliendesha mafunzo kwa wanachama wake kuhusu shughuli za uendeshaji soko. Mafunzo haya yamefanywa **kwa makampuni 20** ya Tanzania ambayo yameorodheshwa kwenye soko la Hisa na mengine saba ya udalali (Brockers).

▪ Aidha, DSE iliendelea na juhudi ya kushirikiana na taasisi mbalimbali za kimataifa kama World Federation of Exchanges na United Nations Sustainable Stock Exchange lengo likiwa ni kujenga uwezo na kuongeza wigo wa muonekano (profiling) kwa wawekezaji kimataifa.




# MIFUKO YA UWEZESHAJI NA PROGRAMU ZA MITAJI

# 8.0. MIFUKO YA UWEZESHAJI NA PROGRAMU ZA MITAJI


Serikali inatekeleza mipango mbalimbali ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ili kuunga mkono juhudi zinazofanywa na wananchi kujiletea maendeleo. Moja ya jitihada zilizofanywa na Serikali ni kuanzisha mifuko au Programu mbalimbali za uwezeshaji ambazo zinawawezesha wananchi kwa kuwawekea mazingira mazuri ili waweze kujikwamua kiuchumi pindi wanapojishugulisha katika shughuli mbalimbali. Hivyo hata utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi unafanywa na sekta zote, kutokana na ushirikiano huu, pamoja na kutegemeana kwa taasisi mbalimbali, Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi kama msimamizi wa Sera hii Kisheria, linaratibu Taasisi hizi katika Sekta zote za Serikali na Binafsi ili kuhakikisha kuwa, malengo ya Sera yanatekelezeka kwa mujibu wa uanzishwaji wa Taasisi hizo.

Uratibu unaofanywa na Baraza ni pamoja na kukusanya taarifa kutoka katika Sekta hizo na kuziwasilisha katika Mamlaka za juu kwa utoaji wa maamuzi. Aidha Baraza linatoa ushauri, maoni ama mapendekezo kwa Taasisi hizo pale inapobidi ili kuboresha ufanisi pamoja na kuongeza tija.


Mifuko/Programu za Uwezeshaji zilizoanzishwa na Serikali pamoja na Taasisi binafsi na kuratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi iko 39 ambayo imegawanyika katika majukumu yafuatayo:-

1. Mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja
2. Mifuko inayotoa dhamana
3. Mifuko inayotoa Ruzuku
4. Mifuko inayoongeza ukwasi kwenye Benki za Biashara
5. Programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi

*Mchoro 10: Mifuko inayotoa mikopo moja kwa moja*





*Mchoro 11: Mifuko inayotoa mikopo kupitia mabenki kwa dhamana*




*Mchoro 12: Mifuko inayotoa Ruzuku*



*Mchoro 13: Mifuko inayoongeza Ukwasi kwenye Benki*




Programu za Uwezeshaji ni pamoja na:

| Na. | Programu za Uwezeshaji |
|---|---|
| 1. | Mpango wa kuendeleza sekta binafsi za fedha Tanzania (Financial Sector Depening Trust- FSDT) |
| 2. | Programu ya miundombinu ya masoko na Huduma za kifedha Vijijini (MIVARF) |
| 3. | Mpango wa Kurasimisha Rasilimali za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) |
| 4. | Unit Trust of Tanzania Asset Management and Investor Services (UTT – AMIS) |

## 8.1. MAELEZO KUHUSU MIFUKO

| MFUKO WA KUWAENDELEZA WAJASIRIAMALI WANANCHI (NEDF)- SIDO | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa mikopo kwa wenye viwanda vidogo na wafanyabiashara wadogo Tanzania Bara, ili kuondoa umaskini kwa kuanzisha na kuendeleza miradi yao katika sekta ya uzalishaji inayohusika na viwanda vidogo, kilimo na kusindika vyakula (matunda na mboga), ufugaji, uvuvi na madini n.k. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Umetoa mikopo ya shilingi bilioni 62.8 kwa wajasiriamali 85,982 (KE-44,947; ME 39,570 Ubia 1,465) na kutoa ajira 174,067. |

| MFUKO WA UWEZESHAJI WA MWANANCHI (MEF) – NEEC | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Dhamana za mikopo |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kutoa dhamana za mikopo kwa SACCOS 58 , Vikundi vya VICOBA 172 na makampuni 2 katika mikoa 16 na Halmashauri za Wilaya 52 kupitia Taasisi shiriki za CRDB Microfinance, TPB Benki, Benki ya Maendeleo ya TIB na UTT Microfinance. Aidha wananchi wajasiriamali wapatao 17,638 wamefanikiwa kupata mkopo kutoka katika makundi hayo ambapo miongoni mwao wanawake ni 9,234 na wanaume ni 8,404. Jumla ya mikopo iliyodhaminiwa kutoka katika Taasisi shirikishi zote za mfuko ni 12,990,849,413 |

| SELF MICROFINANCE FUND (SELF-MF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa Mikopo kwa Asasi Ndogondogo za Kifedha |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umetoa mikopo ya masharti nafuu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 94.0 kwa Asasi Ndogo na za Kati za fedha zipatazo 479 ili kuwakopesha wajasiriamali wadogo wadogo. Wajasiriamali wadogo wadogo hao ni 119,231 wakiwemo wanawake ni 66,822 (56%) na 52,409 (44%) ni wanaume walinufaika katika Asasi hizo na kutengeneza Ajira 254,972 |

**Kuimarika kwa shughuli za Kilimo na Viwanda vidogo**

Mfuko wa SELF umeweza kuimarisha shughuli za Kilimo na Ufugaji kwa kutoa mikopo yenye masharti nafuu kwa Asasi za Fedha zenye kutoa mikopo ya Kilimo. Walengwa wa Mfuko wa SELF, wameweza kuboresha na kuongeza thamani kwenye bidhaa wanazozalisha na kufanya kuwa na uhitaji mkubwa wa bidhaa wanazozalisha.

***Picha Na.2:2 Inaonyesha Kiwanda cha Kusindika Mvinyo wa Zabibu***



Bwana Archard Kato ambaye ni Mwanachama wa Mwashita SACCOS (Mwenye miwani), akitoa maeleazo kwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji, jinsi anavyokamua na kutunza maji ya zabibu kwenye kiwanda chake cha kutengeneza – Mvinyo (Dodoma Wine).

| UTT-MICROFINANCE FUND | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa mikopo kwa wajasiriamali Wadogo na wa Kati |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo ya shiilingi bilioni 34.99 kwa wanawake 26,743 na wanaume 14,946 |

| MFUKO WA RAIS WA KUJITEGEMEA (PTF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa Mikopo kwa Wanawake, Vijana na watu wenye ulemavu (PWDs). |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umetoa jumla ya mikopo 3,853 ambapo miongoni mwao vijana ni 784, wanawake 2,989 na kundi maalum la vijana na wanawake walemavu na waishio katika mazingira magumu 80. Mikopo iliyotolewa ina thamani ya Sh. 2,786,900,000 ambapo kwa vijana imetolewa sh 658,900,000, wanawake Sh. 2,090,150,000 na kundi maalumu Sh.37, 850,000. |

| MFUKO WA PEMBEJEO WA TAIFA (AGITF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Utekelezaji wa Sera ya Serikali kuhusu upatikanaji wa pembejeo za kilimo, mifugo na uvuvi kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wadogowadogo kwa wakati unaofaa na kwa bei nafuu. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo kwa wananchi 3,020 (wanaume 2,416 na wanawake 604). Yenye jumla ya shilingi 76,724,641,481 |

| MFUKO WA MAENDELEO YA WANAWAKE (WDF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa mikopo yenye masharti nafuu hasa kwa wanawake wasio na vigezo au sifa za kukopesheka katika taasisi za fedha ili waweze kujikwamua kiuchumi na kupambana na changamoto mbalimbali zinazowakabili kulingana na nafasi yao katika familia na jamii. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo ya shilingi 3,347,598,846 kwa vikundi 5,169 vyenye jumla ya wanawake 772,075 kutoka katika Halmashauri 153 zilizopo katika mikoa yote 26 ya Tanzania Bara. |

| MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA (YDF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuwawezesha vijana wote nchini (Tanzania Bara) kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha au kuendeleza miradi yao ya uzalishaji mali |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umetoa mikopo yenye thamani ya shilingi 6,564,607,120 kwa vikundi vya vijana 6,332 vyenye wanachama 44,338 |

| MFUKO WA HIFADHI ZA MISITU (TAFF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuwezesha uhifadhi, usimamizi na uendelezaji wa rasilimali misitu hapa nchini kwa kutoa ruzuku. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefadhili miradi 424 ya shilingi bilioni 4.9 katika sekta ya misitu na nyuki katika mikoa 26 Tanzania Bara, kati ya miradi hiyo, miradi 254 ya kuboresha kipato cha jamii, miradi 127 ya uhifadhi wa misitu, na miradi 43 ya utafiti katika misitu. |

| MFUKO WA KUWASAIDIA MAKANDARASI (CAF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa Dhamana za Mikopo kwa Makandarasi Wazawa. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umetoa dhamana ya shilingi 29,907,681,599 kwa Makampuni **1,612,** Kati ya makampuni yaliyofaidika, makampuni 26 yanamilikiwa na kuongozwa na wanawake na 1,586 yanaongozwa na wanaume. |

| MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuwezesha Kaya Maskini kuongeza kipato na kuzifikia fursa na kuongeza uwezo wa kugharamia mahitaji muhim, kujenga rasilimali watu ya watoto kwa kuwezesha kaya maskini kuwekeza kwenye lishe, afya na elimu, kupunguza umaskini wa kipato kwa kaya maskini kwa kuzipatia fursa ya ajira ya muda na kutekeleza miradi ya kuongeza kipato, kuimarisha upatikanaji wa huduma za kijamii katika sekta za elimu, afya, maji. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kuandikisha kaya Masikini 1,118,751 zenye jumla ya watu 5,222,309 ambapo kati ya hao wanawake ni asilimia 54 na wanaume ni asilimia 46. Watoto wa Shule (miaka 6-18) ni asilimia 38.9 na watoto wanaohudhuria Kliniki (miaka 0-5) ni asilimia 16.1<br>Mfuko umefikisha mizunguko 26 ambapo shilingi bilioni 755.7 zimelipwa kwa walengwa wote<br><br>Mfuko umefanikiwa kuwalipa walengwa 1,099,289 kupitia mfumo wa kielektroniki (e payment), kiasi kilicholipwa kupitia mfumo huo ni shilingi 4,773,555,633<br><br>Walengwa 253,117 wamefanya kazi kupitia ajira za muda (PWP) na kulipwa jumla ya shs 53,050,579,600. Aina ya miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji, uanzishwaji wa vitalu vya miche, ujenzi na ukarabati wa barabara za vijijini, kujenga makinga tuta, kulinda na kuhifadhi mazingira n.k<br><br>Jumla ya vikunid 5,136 vya kuweka akiba na kuwekeza vimeundwa vyenye wanachama 111,907 |

| MFUKO WA DHAMANA ZA MIKOPO KWA WAJASIRIAMALI WADOGO NA WA KATI (SME-CGS) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Wajasiriamali wadogo na wa kati |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko huu umefanikiwa kutoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi 10,521,225,230 kwa wajasaraliamali wadogo na wakati. |

| MFUKO WA UDHAMINI WA MAUZO NJE YA NCHI (ECGS) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kukuza mauzo ya bidhaa nje ya nchi |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko huu ulianza na mtaji wa shilingi bilioni 25 ambapo mtaji huu umekuwa hadi kufikia Shilingi 101,006,881.37<br>Mfuko umefanikiwa kutoa dhamana ya mikopo yenye thamani ya shilingi 1,643,240,669,148.08. Tangu mfuko huu ulipoanzishwa mwaka wa fedha wa 2002/3 ambapo sehemu kubwa ya udhamini uliotolewa ulikwenda katika sekta 5 tu, Kilimo ilichukua asilimia 92.8 ya udhamini wote |

| ASASI YA KUSAIDIA SEKTA BINAFSI YA KILIMO (PASS) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuchochea uwekezaji na kukuza kilimo cha biashara |
| **Mafanikio ya Mfuko** | PASS imewezesha uwekezaji katika sekta ya kilimo kiasi cha shilingi bilioni 491.3 kwa zaidi ya miradi 5,603 na kuwezesha zaidi ya watanzania 1,822,436 kuajiriwa; |

| MFUKO WA KILIMO KWANZA (KKCF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa Mikopo kwa ajili ya Kukuza Sekta ya Kilimo |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi 62,712,914,920 kwa miradi ipatayo 189 katika mikoa 23, wilaya 76 ambapo miradi hiyo ilijumuisha matrekta 252, power tillers 145, Mitambo ya umwagiliaji zaidi ya 15 (irrigation equipment) mashine za uvunaji zaidi ya 8 (combine harvesters),ujenzi wa maghala, magari ya kubeba mazao/ nafaka. |

| MFUKO WA ELIMU TANZANIA (TEF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kufadhili miradi ya elimu katika ngazi zote ili kuinua viwango cha ubora wa elimu na kuongeza upatikanaji wake kwa usawa |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umeweza kufadhili na kutekeleza miradi 2018 yenye thamani ya TZS bilioni 105,821,206,022. |

| MFUKO WA NISHATI VIJIJINI (REF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuwezesha upatikanaji na matumizi ya nishati bora kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii vijijini kama vile afya, elimu, maji na mawasiliano |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kutekeleza Mradi Kabambe wa Umeme Vijijini Awamu ya Pili (Rural Electrification under Turnkey Phase II) na ulihusisha ujenzi wa vituo sita vya kuongeza msongo wa umeme (11/33kV) katika miji ya Kigoma, Kasulu, Kibondo, Ngara, Mbinga na Tunduru; ujenzi wa takribani kilomita 13,810 za njia ya msongo wa 11/33kV; kilomita 7,128 za njia za usambazaji wa msongo wa 0.4kV; |

| MFUKO WA MAWASILIANO KWA UMMA (UCSAF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuleta msukumo na ushiriki wa watoa huduma za mawasiliano katika kukuza na kusukuma maendeleo ya kijamii na uchumi kwa kutumia mawasiliano hususani katika maeneo ya vijijini na maeneo ambayo hayana mvuto wa kibiashara. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | i. Mfuko umezifikia kata 518, zenye vijiji 1,939 ambapo wananchi zaidi ya milioni 3.1 wamenufaika, jumla ya dola za Kimarekani 41.5 milioni zimetumika kukamilisha miradi hiyo<br>ii. Mfuko umeendesha mafunzo mbalimbali ya TEHAMA kwa walimu 309 wa shule za msingi na sekondari kutoka katika kila mkoa<br>iii. Mfuko, kwa kushirikiana na kampuni ya Star Media umewezesha wananchi 2,500 kuunganishwa na matangazo ya televisheni ya kidigitali ambapo Mfuko ulitoa ruzuku ya ving'amuzi 2,500 katika mikoa ya Songwe, Geita, Simiyu, Njombe na Katavi;<br>iv. Mfuko kwa kushirikiana na wadau mbalimbali umefikisha vifaa vya TEHAMA na kuunganisha mtandao wa intaneti katika shule 300; |

| UTT- AMIS | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuhamasisha utamaduni wa kuweka akiba miongoni mwa Watanzania na kuanzisha na kuendesha Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | i. Thamani au ukubwa wa mifuko umeongezeka kutoka shilingi bilioni 120.148 mpaka bilioni 256.5<br>ii. Imewalipa wawekezaji wapatao 85,604 kwa mauzo ya vipande vya thamani ya Shilingi bilioni 198.9<br>iii. Thamani ya kipande imekua kwa Tsh. 473.00 kutoka Tsh. 70.00 ambayo bei ya kununulia vipande Mfuko ulipoanza hadi Tsh. 543.00<br>iv. Mfuko wa kujikimu umeongezeka kutoka Tsh. 1.17 Bilioni hadi kufikia Tsh. 21.68 bilioni |

| MFUKO WA MIKOPO MIDOGO YA NYUMBA (HOUSING MICROFINANCE FUND) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa mikopo ya ujenzi, ukarabati au ununuzi wa nyumba kwa gharama nafuu na masharti rahisi ya dhamana kwa kushirikiana na Taasisi za fedha |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko huu umefanikiwa kutoa dhamana za mikopo yenye thamani ya shilingi 11,500,000,000 kwa wananchi zaidi ya 1,000 kwa ajili ya ujenzi, ukarabati au ununuzi wa nyumba kwa gharama nafuu na masharti rahisi. |
| **MFUKO WA FIDIA YA ARDHI TANZANIA** | |
| **Lengo la Mfuko** | Kuratibu masuala yote ya ulipaji wa fidia ya ardhi |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Tangu kuanzishwa kwa ofisi ya Mfuko wa fidia mwezi Machi, 2017 bado uzinduzi rasmi wa Mfuko haujafanyika. Hivyo shughuli za kuratibu ulipaji wa fidia kwa kushirikiana na wadau wa fidia (watwaaji wa ardhi) hazijaanza rasmi. |
| **MFUKO WA MIKOPO YA NYUMBA KWA WATUMISHI WA SERIKALI** | |
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa mikopo kwa watumishi wa Serikali walioajiriwa na kuthibitishwa kazini ambao ni raia wa Tanzania ajili ya kujenga, kukarabati au kununua nyumba, kwa masharti ya kudumu. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umetoa jumla ya mikopo 1669 kwa watumishi wa Serikali na malipo ya watumishi 302 yanaendelea kufanyika. Kwa wastani mfuko hukusanya jumla ya shilingi 600,000,000 kama marejesho ya mkopo kwa mwaka. |
| **MFUKO WA NISHATI JADIIFU** | |
| **Lengo la Mfuko** | Kuziwezesha benki za biashara kuweza kutoa mikopo kwa ajili ya uzalishaji wa nishati vijijini *(Refinancing)* na mikopo ya nishati asilia. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kutoa dhamana za Mikopo ya shilingi bilioni 9.176 kwa Miradi minne ya umeme katika mikoa ya Iringa, Ruvuma, Pwani na Manyara ya umeme ambayo inazalisha umeme kiasi cha 7.64 MW na kusambazwa katika vijiji vya karibu kuzunguka miradi na kiasi kingine kununuliwa na TANESCO chini ya mkataba maalum. |
| **BODI YA MIKOPO YA ELIMU YA JUU** | |
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji waliodahiliwa katika taasisi za elimu ya juu kwa ajili ya masomo ya Shahada au Stashahada ya juu na kukusanya marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa wanafunzi wa taasisi za elimu ya juu tangu mwaka 1994. |

| | |
|---|---|
| **Mafanikio ya Mfuko** | Jumla ya wanafunzi **122,623** wamepata mikopo yenye thamani ya **TZS 422.45 bilioni**. Kati yao, wanafunzi **33,244** ni wa mwaka wa kwanza waliopata mikopo yenye thamani ya **TZS 110.37 bilioni** na wengine **89,379** ni wanaoendelea na masomo ambao wamepata mikopo yenye thamani ya **TZS 312.16 bilioni**.<br><br>Katika mwaka wa masomo (2016/2017), Jumla ya wanafunzi **112,409** walipangiwa mikopo yenye thamani ya TZS 409.61 bilioni. Kati ya hao, wanafunzi **28,383** walikuwa wa mwaka wa kwanza na wengine **86,688** walikuwa wanaendelea na masomo.<br>Hadi kufikia **Desemba 31, 2017**, kiasi cha **TZS 85 bilioni** kilikuwa kimekusanywa huku lengo la makusanyo kwa mwaka mzima wa fedha utakaomalizika Juni 30, 2018 ni **TZS 130 bilioni.** |
| **MFUKO WA BARABARA** | |
| **Lengo la Mfuko** | Mfuko ulianzishwa ili kugharimia matengenezo ya barabara kuu, mikoa, wilaya, miji na ujazio(feeder roads) kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Barabara ya Mwaka 2007 |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi Bilioni 604,489,346,576 sawa na asilimia 65.88 kulinganisha na kiasi kilichokadiriwa kukusanywa ambacho ni shilingi bilioni 917,548,000,000 |
| **MPANGO WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (JK FUND)** | |
| **Lengo la Mfuko** | Kutoa dhamana za Mikopo kwa Wajasiramali wadogo na wakati katika sekta zote za Uchumi ( Kwa sasa Mpango huu unafatilia Marejesho, hivyo hautoi mikopo mipya) |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mpango huu (kwa awamu zote mbili) ulikuwa umetoa mikopo yenye thamani ya **shilingi bilioni 50.06** na kuwanufaisha Wajasiriamali **76,546** ambapo urejeshaji wa mikopo ulikuwa asilimia **84** |
| **MFUKO WA UBUNIFU VIJIJINI (RIF)** | |
| **Lengo la Mfuko** | Kuendeleza Miradi ya ubunifu itakayoleta Tija Vijijini |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko huu umezinduliwa Februari, 2018; hivyo bado haujaanza kutoa uwezeshaji kimtaji |
| **MFUKO WA DHAMANA ZA MIKOPO KWA WAKULIMA WADOGOWADOGO (SMALLHOLDERS' CREDIT GUARANTEE SCHEME)** | |
| **Lengo la Mfuko** | Kuhamasisha matumizi ya teknolojia na mbinu bora za kilimo kwa wakulima wadogo wadogo kwa kuboresha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa lengo la kuchagiza kilimo cha kibiashara, kuongeza ajira na kuhakikisha usalama wa chakula |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko huu umezinduliwa Februari, 2018; hivyo bado haujaanza kutoa uwezeshaji kimtaji |

| MPANGO WA KUENDELEZA SEKTA BINAFSI ZA FEDHA TANZANIA (FINANCIAL SECTOR DEPENING TRUST- FSDT) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Umejikita (pamoja na wadau mbali mbali) katika kutafuta njia za kuhakikisha upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha unaongezeka na kuwa endelevu ili Watanzania wengi wapate fursa ya kuzitumia huduma bora za kifedha kwa ajili ya kujiletea maendeleo yao, kuongeza tija katika uzalishaji na ujasiliamali, hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi kwa ujumla |
| **Mafanikio ya Mfuko** | i. FSDT imesaidia Upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha nchini kwa ujumla. Tanzania imepiga hatua kubwa katika kipindi cha miaka minne (2013-2017). Kwa mfano idadi ya watanzania wanaotumia huduma za kifedha imekua kutoka asilimia 58% hadi 65% kati ya mwaka 2013 na 2017 kulingana na taafira ya FinScope Tanzania 2017.<br>ii. FSDT imetoa mawazo na fedha katika utengenezaji wa Sera mpya ya Huduma Ndogo za Kifedha (National Microfinance Policy 2017) iliyozinduliwa mwezi Octoba 2017.<br>iii. FSDT imetoa mchango wa mawazo, fedha na utaalamu katika kubuni na ketekeleza utafiti wa FinScope Tanzania 2017 unaoangazia maendeleo katika upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha. Matokeo ya utafiti huu yalizinduliwa mwezi Septemba 2017 na ulifanyika kwa kushirikiana kwa karibu na Idara ya Takwimu ya Taifa (NBS), Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania. Tafafiti zingine ni kama MSME Survey 2012, Financial Capability 2014, Financial Access Points (2010 & 2014).<br>iv. FSDT imetoa mchango wa mawazo, fedha na utaalamu katika kubuni na kutengeneza Mkakati wa Huduma Jumuishi za Kifedha uliozinduliwa mwezi Desemba 2017 na ule ambao muda wa utekelezaji wake umeishia Desemba 2016<br>v. FSDT imeshirikiana vizuri na serikali pamoja na wadau wengine katika mchakato wa kuandaa na kutunga sheria ya mifumo ya malipo nchini pamoja na kanuni zake (NPS Act, Licensing rules and regulations) na kutengeneza Mpango wa Elimu ya Fedha kwa wananchi (Financial Education Framework).<br>vi. FSDT imetoa mchango wa mawazo, fedha na utaalamu katika kubuni na ketekeleza utafiti wa FinScope Tanzania 2017 unaoangazia maendeleo katika upatikanaji na utumiaji wa huduma za kifedha. Matokeo ya utafiti huu yalizinduliwa mwezi Septemba 2017 na ulifanyika kwa kushirikiana kwa karibu na Idara ya Takwimu ya Taifa (NBS), Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania. Tafafiti zingine ni kama MSME Survey 2012, Financial Capability 2014, Financial Access Points (2010 & 2014). |

| SAGCOT-CATALYTIC TRUST FUND | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Mfuko umelenga kutoa msaada wa kifedha kwa ajili ya kuanzisha na kuwezesha kilimo biashara kwa kuwaunganisha wakulima wadogo na masoko ya mazao katika ukanda wa kilimo wa kusini pamoja na kutoa misaada kwa wakulima hao katika mifumo yao ya kibiashara. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umetoa mafunzo kwa wakulima 2,600 katika ukanda wa kusini mwa Tanzania |

| MFUKO WA MADINI KWA WACHIMBAJI WADOGO NCHINI | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuendeleza wachimbaji wadogo nchini kwa kuwapa ruzuku na mikopo kwa ajili ya shughuli uchimbaji, uchenjuaji, uongezaji wa thamani na shughuli nyingine zinazohusiana na uchimbaji mdogo wa madini. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | i. Umewafikia wachimbaji wadogo nchini wapatao 124 ambapo shs milioni 345.2 zilitolewa kama mkopo na shs million 7.2 kama ruzuku<br>ii. Umechochea kuongezeka kwa matumizi ya vifaa bora vya uchimbaji kwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya fedha imetumika kununulia vifaa vya uchimbaji; na<br>iii. Mfuko unazingatia jinsia katika uwezeshaji. Wanawake katika shughuli za madini kwa awamu zote mbili (awamu ya kwanza 36% ya pili 10%). |

| PROGRAMU YA MIUNDOMBINU YA MASOKO NA HUDUMA ZA KIFEDHA VIJIJINI (MIVARF) | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Programu hii ilianzishwa ili kufanikisha azma ya Serikali ya kuongeza kipato na uhakika wa chakula kwa kaya zenye kipato cha chini hasa maeneo ya vijijini kupitia kuboresha miundo mbinu ya masoko (ikiwa ni ukarabati wa barabara za vijijini, ujenzi wa maghala ya kuhifadhia mazao na ujenzi wa masoko), kuwawezesha wananchi waishio vijijini kuongeza thamani mazao ya kilimo, kuwajengea wananchi hao uwezo wa kuyafikia masoko na kupanua wigo wa huduma za kifedha zipatikanazo vijijini. |
| **Mafanikio ya Mfuko** | i. Umefanikiwa kukarabati barabara zenye urefu wa Km 1078 ambapo kwa Zanzibar (Unguja 68 na Pemba 80km).<br>ii. Umekarabati maghala 6 na Kujenga masoko 9.<br>iii. Jumla ya vikundi 36 vimefanikiwa kupata ruzuku za asilimia 75% za kununua mitambo ya kuongeza mazao<br>iv. Jumla ya minyororo ya thamani ishirini na moja inaendelezwa na Programu. Minyoro hii ni pamoja na Alizeti, Choroko, Kitunguu Maji, Kitunguu Saumu, Korosho, Ufuta, Mahindi, Majimbi, Mananasi, Maparachichi, Matunda mbali mbali na Mboga mboga, Maziwa, Mifugo, Mpunga, Muhogo, Ndimu, Ndizi, Samaki, Samaki -madagaa, Tangawizi na Ufuta.<br>v. Jumla ya wananchi 3,497,674 (57% wanawake) wamefikiwa na huduma za kifedha kupitia asasi mbalimbali za kifedha zilizo rasmi na zisizo rasmi zinazofanya kazi na Programu. Asasi hizi zimeweza kukusanya akiba zenye thamani ya shillingi bilioni 16 na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 6.6. |

| MKURABITA | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wizara za Kisekta kwa Zanzibar, ili kuwezesha urasimishaji wa rasilimali ardhi vijijini na mijini pamoja na biashara kwenye Mikoa, Wilaya, Kata, Shehia na Vijiji |
| **Mafanikio ya Mfuko** | i. Wafanyabiashara 8,736 wamepata mafunzo ya jinsi ya kuendesha biashara zao, na 4,413 wamesajili biashara zao kwa Tanzania Bara na Zanzibar. Wafanyabiashara 6,136 wamepata mafunzo Tanzania bara na 2,600 Zanzibar. Aidha, wafanyabiashara 3,124 Tanzania Bara na 1,289 Zanzibar wamesajili biashara zao.<br>ii. Mashamba 110,174 yamepimwa Tanzania bara na Zanzibar ambapo mashamba 105,617 yamepimwa Tanzania Bara katika Kata 105 kwenye Vijiji 221 na Hati za Hakimiliki za Kimila 71,088 zimeandaliwa na kutolewa kwa wananchi. Kwa upande wa Zanzibar mashamba 4,557 yamepimwa katika Kata nne(4) kwenye Shehia nne (4).<br>iii. Kuwezesha Halmashauri za wilaya kupata vifaa vya urasimishaji ambapo kompyuta 63, vifaa vya upimaji (GPS) 380 na shajala mbalimbali zimetolewa;<br>iv. Ujenzi wa Ofisi za Masjala ya ardhi katika Vijiji 21 umekamilika katika Halmashauri za Wilaya 10 za Handeni, Bagamoyo, Mpwapwa, Manyoni, Moshi, Meru, Serengeti, Mbinga, Musoma na Wete. Aidha, ujenzi wa masjala za ardhi za vijiji 22 unaendelea katika Halmashauri za wilaya 13. Vilevile, MKURABITA imewezesha kukamilika kwa ujenzi wa masjala mbili (2) za Wilaya ya Bagamoyo na Nachingwea.<br>v. Viwanja 10,518 vimepimwa Tanzania Bara ambapo Hati Miliki 2,129 zimeandaliwa na Viwanja 4,600 vimepimwa Zanzibar ambapo Hati Miliki zinaendelea kuandaliwa |

| MFUKO WA MAENDELEO YA MAJI | |
|---|---|
| **Lengo la Mfuko** | Mfuko huu ulianzishwa ili kuwa na chanzo endelevu cha fedha za uwekezaji katika miradi ya maji |
| **Mafanikio ya Mfuko** | Mfuko umefanikiwa ujenzi wa Miradi 71 ya Maji iliyofikia Vijiji 366 |




# VIKUNDI VYA KIFEDHA VYA KIJAMII


# 9.0. VIKUNDI VYA KIFEDHA VYA KIJAMII

Mchango wa vikundi vya kifedha vya kijamii katika kuongeza huduma jumuishi za kifedha nchini umeendelea kuongezeka. Utafiti wa hali ya huduma za kifedha Tanzania (FinScope) wa mwaka 2017 ambao ulifanywa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi ya Kuboresha huduma za Kifedha Tanzania (FSDT) unaonesha kuwa upatikanaji wa huduma za kifedha kupitia vikundi vya kifedha vya kijamii uliongezeka kutoka asilimia 12 ya watazania wenye umri wa miaka 16 na kuendelea (mwaka 2013) hadi asilimia 16 (mwaka 2017). Hali hii inamaanisha kuwa hadi mwaka 2017 watu zaidi ya 4,450,000 walikuwa wanapata mitaji kwa ajili ya kuendesha shughuli zao za kiuchumi kupitia vikundi vya kifedha vya kijamii ikilinganishwa na watu 2,900,000 mwaka 2013.

## 9.1. UKUAJI WA VIKUNDI VYA KIFEDHA VYA KIJAMII

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linafanya kazi na miavuli ya kitaifa ya vikundi vya kifedha vya kijamii ambayo ni VICOBA-Federation of Tanzania (VICOBA-FETA, Tanzania Informal Microfinance Association of Practitioners (TIMAP) na Inter-Religious VICOBA (IR VICOBA). Wanachama wa miavuli hiyo ni taasisi (promota) zinazojihusisha na kuanzisha na kuendeleza vikundi vya kifedha ya kijamii (VICOBA, VSLAs, n.k). Hadi kufikia Aprili 2018 VICOBA-FETA ilikuwa na taasisi wanachama 19. Kati ya wanachama hao 14 waliweza kuwasilisha taarifa za vikundi vyao, wanachama 5 hawakuweza kuwasilisha taarifa za vikundi vyao. Taasisi wanachama wa VICOBA-FETA ambao waliwasilisha taarifa za vikundi vyao kulikuwa na jumla ya vikundi 57,197 vyenye jumla ya wanavikundi 781,027 kati yao 225,723 ni wanaume na 555,004 ni wanawake. Vikundi hivyo vilikuwa na jumla ya mtaji wa shilingi bilioni 153.24 viliweza kutoa jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 141.77 kwa wanachama wake.


***Mchoro 14: Taasisi Mwavuli ya VICOBA (FETA)***




*Chanzo: Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)*

Hadi kufikia Aprili 2018 Taasisi ya TIMAP ilikuwa na taasisi wanachama 15 zenye jumla ya vikundi 26,670 vyenye jumla ya wanavikundi 627,952 kati yao 221,748 ni wanaume na 406,204 ni wanawake. Vikundi hivyo vilikuwa na jumla ya mtaji wa shilingi bilioni 64.59 viliweza kutoa jumla ya mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 62.50 kwa wanachama wake.


***Mchoro 15: Watekelezaji wa Sekta Isiyo Rasmi (TIMAP)***




*Chanzo: Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)*

Hadi kufikia Aprili 2018 Taasisi ya IR VICOBA ilikuwa na jumla ya vikundi 4,652 vyenye jumla ya wanavikundi 98,632 kati yao 33,504 ni wanaume na 65,128 ni wanawake. Vikundi hivyo vilikuwa na jumla ya mtaji wa shilingi bilioni 50.43. Hivyo, kwa ujumla taasisi hizi miavuli zilikuwa na vikundi 88,519 vyenye jumla ya wanavikundi 1,596,130 ambapo kati yao 480,975 ni wanaume na 1,026,336 ni wanawake. Aidha, kwa pamoja vikundi katika taasisi hizo zilikuwa na jumla ya mtaji wa shilingi bilioni 268.26.


***Mchoro 16: VICOBA vya Dini mbalimbali***




*Chanzo: Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)*

Aidha, Baraza la Taifa la Uwezeshaji wananchi Kiuchumi linapokea takwimu za vikundi vya kifedha vya kijamii kutoka kwenye mikoa yote ya Tanzania Bara. Takwimu za maendeleo ya vikundi vya kifedha vya kijamii zilipokelewa na Baraza hadi Mwezi Aprili 2018 kutoka katika mikoa 21 (Halmashauri 147) kati ya mikoa 26 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni Arusha, Kigoma, Katavi, Pwani, Simiyu, Lindi, Shinyanga, Singida, Ruvuma, Iringa, Manyara, Tabora, Mbeya, Geita, Morogoro, Dodoma, Mara, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Kagera na Njombe. Takwimu hizo zinaonesha kuwa katika Mikoa hiyo kuna jumla ya vikundi vya kifedha vya kijamii 56,536 vyenye jumla ya wanachama/wanavikundi 859,656. Kati ya wanavikundi hao 365,147 ni wanaume na 542,337 ni wanawake. Vikundi hivyo vinasajiliwa katika Halmashauri za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ambapo katika vikundi vilivyotolewa taarifa vikundi 41,020 vilikuwa vimesajiliwa na vikundi 13,589 vilikuwa bado havijasajiliwa.

***Mchoro 17: Halmashauri za Wilaya***




*Chanzo: Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC)*

Hadi kufikia Aprili 2018 vikundi hivyo kwa ujumla vilikuwa na mtaji wa shilingi bilioni 84.91 na viliweza kutoa mikopo ya shilingi bilioni 44.46 kwa wanavikundi.

## 9.3. SERA YA TAIFA YA HUDUMA NDOGO ZA KIFEDHA YA MWAKA 2017

Sera ya Taifa ya Huduma Ndogo za Kifedha ya Mwaka 2017 imevitambua vikundi vya kifedha vya kijamii kama moja ya nyenzo muhimu ya kufikisha huduma za kifedha kwenye jamii, hususan maeneo ya vijijini. Sera hiyo imetoa jukumu kwa Wizara inayohusika na Masuala ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kusimamia na kuwezesha vikundi hivyo kutekeleza malengo na majukumu yake kwa ufanisi. Majukumu katika kuendeleza vikundi hivyo yamegawanywa kama ifuatavyo:

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

1) Kutoa miongozo na kufuatilia masuala ya huduma ndogo za kifedha kuhakikisha yanajumuishwa kwenye mipango na sheria ndogo za Serikali za Mitaa;
2) Kuendeleza na kusimamia kanzidata ya vikundi vya kifedha vya kijamii; na
3) Kuandaa taarifa za vikundi vya kifedha vya kijamii.

**TAWALA ZA MIKOA**

1) Kutoa miongozo na kufuatilia masuala ya huduma ndogo za kifedha kuhakikisha yanajumuishwa kwenye mipango na sheria ndogo za Serikali za Mitaa;
2) Kuendeleza na kusimamia kanzidata ya vikundi vya kifedha vya kijamii katika ngazi ya mkoa;
3) Kuratibu shughuli za huduma ndogo za kifedha katika ngazi ya mkoa; na
4) Kuandaa taarifa za vikundi vya kifedha vya kijamii

**MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA**

1) Kusajili, kusimamia na kudhibiti vikundi vya kifedha vya kijamii;
2) Kuendeleza na kusimamia kanzidata ya vikundi vya kifedha vya kijamii;
3) Kuendelea kuhamasisha urasimishaji wa watoa huduma za fedha wasio rasmi;
4) Kuanzisha Kamati ya Huduma ndogo za fedha;
5) Kufuatilia na kutathmini maendeleo ya watoa huduma za fedha kwenye vikundi; na
6) Kuandaa taarifa za vikundi vya kifedha vya kijamii

**BARAZA LA TAIFA LA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI (NEEC)**

1) Kuratibu mifuko na programu za Serikali
2) Kusimamia na kutathmini mifuko na programu za serikali
3) Kuanzisha na kusimamia kanzidata za mifuko na programu za Serikali
4) Kuandaa taarifa kwa vipindi tofauti kuhusu mifuko na programu za Serikali

## 9.4. MAADHIMISHO YA SIKU YA VICOBA TANZANIA

Tarehe kumi na saba mwezi wa kumi kila mwaka inajulikana kuwa ni Siku ya Kutokomeza Umaskini Duniani. Mataifa mbalimbali ulimwenguni kote huadhimisha siku hiyo. Kutokana na mchango mkubwa wa vikundi vya kifedha vya kijamii katika kutoa huduma za kifedha kwa wananchi na kuwezesha kuchangia katika kupambana na umaskini Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi liliona ni vema Siku hiyo ya Kimataifa ya Kutokomeza Umaskini Duniani iwe pia **Siku ya VICOBA Tanzania**. Pamoja na kuwa vikundi vya vya kifedha vya kijamii vinatumia mifumo inayotambulika kwa majina mbalimbali, jina maarufu kwa wananchi wengi ni VICOBA. Hivyo, kwa maana ya maadhimisho hayo iliamuliwa iitwe Siku ya VICOBA Tanzania lakini ikijumuisha vikundi vyote vya kuweka akiba na kukopeshana. Ujumbe wa siku hiyo ulikuwa **''VICOBA kwa Uwezeshaji na Kuondoa Umaskini''.** Lengo la kuwa na maadhimisho hayo lilikuwa ni kutambua, kuhamasisha na kuendeleza mifumo ya vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana kwa ajili ya kupata mitaji ya kufanya shughuli za kiuchumi na kutokomeza umaskini nchini.

Madhumuni ya kuwa na siku ya VICOBA Tanzania ni:

a. Kutumia siku hiyo maarufu duniani kutoa fursa kwa wadau wa vikundi vya kifedha vya kijamii kukutana, kubadilisa uzoefu na kuhamasishana kujiunga katika vikundi vya kuweka akiba na kukopeshana;
b. Kuwawezesha vijana na wanawake kuelewa umuhimu wa mapambano dhidi ya umaskini kwa kujenga tabia ya kujiwekea akiba kupitia vikundi.
c. Kutoa fursa kwa watoa huduma mbalimbali kuonesha huduma na bidhaa zao kwa vikundi vya kuweka na kukopa kwa lengo la kuongeza kasi ya kupambana na umaskini.
d. Kutoa nafasi kwa vyombo vya Serikali na vya kimataifa kuonesha ushirikiano wao na jitihada zinazofanywa katika kutokomeza umaskini.

Siku ya VICOBA Tanzania iliadhimishwa siku ya hiyo na ilianza kwa maonesho ya biashara za wana VICOBA kwa siku tatu na baadaye kuhitimishwa siku yab kilele ambapo jumla ya wanaVICOBA 1,000 walihudhuria.



# USHIRIKIWA WATANZANIA KATIKA UWEKEZAJI (LOCAL CONTENT)

# 10.0. USHIRIKIWA WATANZANIA KATIKA UWEKEZAJI (LOCAL CONTENT)

Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 suala la ushiriki wa watanzania katika uwekezaji limekuwa na mwamko zaidi na uelewa mkubwa zaidi umejengeka kati ya Taasisi za Umma na Binafsi kuhusu umuhimu wake katika kukuza uchumi wa nchi. Aidha, Serikali imetunga Sheria na Kanuni za kuhakikisha kwamba utekelezaji na ufuatiliaji wa masuala ya ushiriki wa watanzania katika uwekezaji yanapewa kipaumbele.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limeendelea kufanya kazi ya kuratibu, kusimamia, na kufuatilia suala la ushiriki wa watanzania katika uwekezaji hasa katika miradi ya kimkakati inayoendelea hapa nchini. Baraza limetengeneza rasimu ya mkakati wa ushiriki wa watanzania katika uwekezaji kwa utakaotumika katika miaka 10 ijayo. Vilevile Baraza limetengeneza mwongozo ambao utatumiwa na watekelezaji wote kutoka sekta ya umma na binafsi. Baraza limekuwa likifuatilia suala la Sheria, mikataba, ajira, ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka kwa kampuni za kitanzania, uongezaji ujuzi, uhamishaji wa tekinolojia na ushiriki wa jamii inayozunguka eneo la uwekezaji.

## 10.1. UJENZI WA UBORESHAJI WA BARABARA YA JUU (FLYOVER) TAZARA:

Mradi wa ujenzi wa Uboreshaji wa Barabara ya Juu (Flyover) TAZARA ipo katika hatua za ujenzi. Hadi kufikia Februari 2018 mradi huo ulishirikisha watanzania kama ifuatavyo:-

**a) Ajira**

Kampuni ya Mkandarasi ya imeajiri wafanyakazi 87 ambao kati yao 60 ni watanzania na 27 ni wageni. Mkandarasi Msaidizi ameajiri watanzania tu ambao ni 150. Ajira mbalimbali kwenye maeneo mengine zimetolewa kwa watanzania wapatao 379, Wasimamizi (Foreman) 19 wakitanzania, Wasimamizi Wasaidizi (Leadman) 5 watanzania, wafanyakazi wenye ujuzi 136 na wasio na ujuzi 219 wote wakiwa watanzania.

**b) Manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali**

Kati ya manunuzi 15 yaliyofanyika ya huduma, kampuni za kitanzania zilikuwa 14 na kampuni 1 ya nje tu. Kiasi cha Shs. 5,763,836,000 zimetumika kwam manunuzi ya bidhaa kutoka kwenye kampuni zilizopo Tanzania na kiasi cha Dola za kimarekani 1,498,000 zimetumika kwa manunuzi kutoka kwenye kampuni zilizopo nje ya Tanzania au kampuni za nje zenye ubia na kampuni ya kitanzania. Manunuzi ya bidhaa mbalimbali yalifanywa kwa kampuni 28 kati ya hizo kampuni zilizopo Tanzania ni 24, kampuni za nje 3 na kampuni yenye ubia kati ya kampuni ya kitanzania na ya nje ni 1.

**c) Mafunzo**

Wafanyakazi wote wakiwemo mameneja, wasimamizi, makandarasi, wenye ujuzi na wasio na ujuzi walipata mafunzo mbalimbali yakiwemo; Mafunzo ya matumizi ya vifaa watu 612, Mafunzo ya awali watu 730, Mfunzo ya usalama watu 580, mafunzo ya moto na uokoaji watu 80, na mafunzo ya kuongoza kwenye ajali watu 15.

**d) Ushirikishwaji wa jamii inayozunguka mradi**

Jamii ilipewa elimu ya maambukizo ya virusi vya UKIMWI pamoja na wafanyakazi wa Makandarasi na wasaidizi wa makandarasi. Aidha kundi hili pia lilipewa mafunzo ya jinsi ya kukusanya na kutunza uchafu.

## 10.2. UJENZI WA BARABARA ZA JUU UBUNGO (UBUNGO INTERCHANGE)

Mradi huu bado upo katika hatua za awali za maandalizi (Utility Relocation). Katika hatua hii ushiriki wa watanzania ulikuwa kama ifuatavyo:-

**a) Ajira**

Jumla ya ajira zilizotolewa katika hatua hii ya mradi ni 319. Aidha nafasi za ajira zilizohitaji ujuzi wa juu (skilled) watanzania waliajiriwa 60 na wageni 50, ajira za ujuzi wa kati (semiskilled) ziliajiri watanzania tu ambao walikuwa 129 na ajira za ujuzi wa chini (unskilled) ziliajiri watanzania tu ambao walikuwa 80.

**b) Manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali**

Katika manunuzi ya bidhaa na huduma 8 yaliyofanyika katika hatua hii kampuni za kitanzania 7 zilitoa huduma na bidhaa na kampuni moja tu kutoka nje ilitoa huduma. Manunuzi ya bidhaa na huduma kutoka kwa kampuni za ndani yaligharimu kiasi cha Shs. 2,509,375,320 na manunuzi yaliyofanyika nje ni kiasi cha Shs. 663,159,824.

**c) Mafunzo**

Mafunzo yalitolewa kwa watu wenye ujuzi wakati ikiwemo Mafunzo ya matumizi ya vifaa, Mafunzo ya awali na mafunzo ya kuongoza watu kwenye ajali. Pia mafunzo yaliyotolewa kwa wafanyakazi wa ujuzi wa juu pamoja na wa kati ni mafunzo ya usalama kutokana na ajali ya moto na uokoaji.

**d) Ushirikishwaji wa jamii inayozunguka mradi**

Elimu ya ugonjwa wa UKIMWI ilitolewa kwa wafanyakazi na kata zote zinazozunguka eneo la mradi. Mafunzo ya njia za usuluhishaji wa migogoro ilitolewa kwa Ofisi za Serikali za mitaa katika Manispaa ya Ubungo na kwa jamii inayozunguka mradi. Kampeni za kujenga uelewa kuhusu mradi ilitolewa kwa wafanyabiashara wadogo na wakazi wa eneo la Ubungo Darajani. Elimu ya kipindupindu ilitolewa kwa wauzaji wa chakula katika eneo la Ubungo na wafanyakazi katika mradi. Elimu kuhusu masuala ya uzoaji taka ilitolewa kwa wananchi katika eneo la Riverside Ubungo.

### 10.3. MRADI WA PILIPILI WELL-1

Mradi wa kisima cha Pilipili ambao unafanywa na Kampuni ya STATOIL. Katika mradi huo watanzania walishiriki kama ifuatavyo:-

**a) Ajira**

Jumla ya ajira zilizotolewa ni 598, ajira 395 zilienda kwa watanzania na ajira 203 zilienda kwa wageni. Watanzania wenye ujuzi wa juu walikuwa 270, wenye ujuzi wa kati 28, na wasio na ujuzi 97. Wageni walipata ajira zenye ujuzi wa juu pekee kwa idadi hiyo ya 203.

**b) Manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali**

Manunuzi ya huduma na bidhaa yalifanyika kwa kampuni za kitanzania 4 na kampuni za kigeni 4.

**c) Mafunzo**

Ufadhili wa masomo umetolewa kwa ajili ya Shahada ya Uzamili kwa watu 26, Aidha mafunzo yamekuwa yanatolewa kwa wadau mbalimbali kutoka kwenye wizara mbalimbali, taasisi za umma na binafsi kuwajengea uwelewa kuhusu mradi wa LNG.

**d) Ushirikishwaji wa jamii**

Jamii zilizopo katika mikoa ya Lindi na Mtwara zilipatiwa huduma ya afya ambapo zaidi ya wagonjwa 500 walitibiwa, 205 walifanyiwa upasuaji na vifaa mbalilmbali vya matibabu vilitolewa.

### 10.4. MRADI WA UJENZI WA RELI (STANDARD GAUGE RAILWAY)

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajenga reli ya kisasa (*Standard Gauge Railway)* kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro katika awamu ya kwanza ya mradi. Utekelezaji wa mradi huu ni mpango wa Serikali wa kujenga reli ya kisasa kutoka Dar es Salaam mpaka Mwanza na Isaka na mpaka Rwanda. Reli hii itaunganisha bandari ya Dar es Salaam na Tanzania bara na vilevile nchi zisizopakana na bahari kama Rwanda, Burundi, Congo na Uganda. Mradi huu ukikamilika unatarajiwa kuchangia kwa kiwango kikubwa kukuza uchumi wa nchi. Hadi kufikia Februari 2018, watanzania walikuwa wameshiriki katika mradi huu kama ifuatavyo:-

**a) Ajira**

Katika mradi huu Mkandarasi anatakiwa kuhakikisha nafasi za ajira muhimu katika mradi (Key Personnel) wanapata Watanzania kazi kwa kwa 20% na Wageni 80%. Hadi kipindi tajwa watanzania walikuwa wameshika nafasi za muhimu 31.1% na wageni 68.7%.

Kwa zile nafasi ambazo si za juu (Non key Staff Personnel) watanzania wanatakiwa kupata 80% za kazi na wageni 20%. Katika kipindi tajwa watanzania walipatakazi 96.3% na wageni 3.7%.

**b) Manunuzi ya Bidhaa na Huduma**

Katika mradi huu mkandarasi anatakiwa kuhakikisha kwamba bidhaa zinazopatikanakwa urahisi Tanzania zinanunuliwa hapa Tanzania. Bidhaa hizi ni kama mchanga, kokoto*, ballast au earthworks*. Ununuzi wa bidhaa hizi nje ya Tanzania utaruhusiwa pale tu ambapo jitihada za kuzipata Tanzania imeshindikana.

### 10.5. MTAMBO WA KUZALISHA GESI WA MNAZI BAY

Uendeshaji wa mtambo wa kuzalisha gesi wa Mnazi Bay unasimamiwa na kampuni ya ***Maurel el Prom Production Tanzania Ltd (M&P)***. Katika mradi huu watanzania wameshirikishwa kikamilifu katika ajira na ununuzi wa bidhaa na huduma.

**a) Ajira , Mafunzo na ununuzi wa Bidhaa na Huduma**

Watanzania walioajiriwa katika mradi huu ni 88 na wageni 8, hivyo ajira kwa watanzania ni 93.2%.

Aidha mafunzo yamekuwa yanatolewa kwa waajiriwa wakiwa kazini (on job training) na M&P wamewezesha chuo cha VETA kwenye kutoa mafunzo ya welding, upakaji rangi na mafundi wa umeme. Ununuzi wa bidhaa na huduma kwa kiwango kikubwa kilifanywa na kampuni za kitanzania isipokuwa kwenye huduma iliyohitaji ujuzi wa hali ya juu.

## 10.6. MRADI WA SONGAS

Uendeshaji wa Mradi wa Songas unasimamiwa na kampuni ya Pan African Energy. Katika kipindi cha robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2017/18 watanzania walishiriki katika mradi huu kama ifuatavyo:-

**a) Ajira na Ununuzi wa bidhaa na Huduma**

Watanzania walioajiriwa katika mradi huu ni 85.4% na wageni 4.6%. kwenye mtambo wa kuzalisha gesi katika kiwanda kilichopo Songosongo wameajiriwa watanzania 97.5% na wageni 2.5%, Watanzania hao wanafanya kazi za uhandisi, HSE na Mafundi (Technicians). Aidha, ununuzi wa bidhaa an huduma ulifaanywa kwa kiwango kikubwa kwa kampuni za ndani.

## 10.7. MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI KUTOKA HOIMA UGANDA MPAKA CHONGELEANI TANGA

**a) Ajira**

Ajira zaidi ya 200 zimetolewa katika kazi za awali ambazo zimefanywa katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Uganda mpaka Tanzania (EACOP). Ajira nyingi zilikuwa zile ambazo zinahitaji ujuzi wa kati ukilinganisha na zile zilizokuwa zinahitaji ujuzi wa juu. Aidha, ajira za ujuzi wa kati na ujuzi wa chini zimetolewa kwa kiwango kikubwa cha 80% kwa watanzania. Ajira zenye ujuzi wa juu (*Seniorpositions*) kwa kiwango kikubwa zimetolewa kwa wageni (Foreigners).

**b) Manunuzi ya Huduma na Bidhaa**

Kazi za awali zilizofanywa katika mradi wa EACOP ni pamoja na *Survey* ya njia ya bomba (MKUZA) kutoka Tanga mpaka Kagera. Katika kazi hiyo Mkandarasi Mkuu ni kampuni kutoka nje lakini kampuni nne zilizotoa huduma za usafirishaji, malazi na huduma za chakula zilikuwa ni za kitanzania. Katika kazi za awali za mradi kampuni za kitanzania zimepata kazi kwa zaidi ya asilimia 70.

**c) Kanzi Data**

Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) imetengeneza Kanzi Data ya kusajili kampuni za watoa huduma na bidhaa za kitanzania katika tasnia ya mafuta kwenye mkondo wa kati na wa chini. Hadi sasa zaidi ya kampuni 160 zimesajiliwa na kampuni zaidi zitapata fursa ya kujisajili pindi awamu ya pili ya usajili itakapofunguliwa.

Wakala wa Ajira Tanzania (TaESA) wameanza kusajili watanzania wenye ujuzi katika sekta ya mafuta ili kutengeneza Kanzi Data ya nguvu kazi iliyopo Tanzania. Mpaka sasa watanzania ambao wamejiandikisha katika kanzi data ya TaESA ni 6,500.

## 10.8. KAMPUNI YA WILLIAMSON DIAMONDS LIMITED

**a) Ajira**

Jumla ya ajira zilizotolewa kwa watanzinia wenye ujuzi wa juu ni 280**,** watanzania wenye ujuzi wa kati ni 174 na watanzania wasio na ujuzi ni 103. Aidha, ajira za kigeni zilikuwa 12 na ni za ujuzi wa juu tu.

**b) Mafunzo**

Mafunzo yaliyotolewa na Kampuni ya Williamson Diamonds ni kama ifuatavyo:

- ❖ Mafunzo ya Afya, Usalama na Mazingira. Mafunzo haya yalitolewa kwa wafanyakazi wote ambao jumla yao ilikuwa 250.
- ❖ Mafunzo ya Uendeshaji wa Magari kwa wenye ujuzi wa juu na wa kati ambao idadi yao ilikuwa 20.
- ❖ Mafunzo ya bodi ya Wahandisi kwa wenye ujuzi wa juu ambao idadi yao ilikuwa 10.
- ❖ Mafunzo ya NBAA na ATE kwa wenye ujuzi wa juu ambao idadi yao ilikuwa 7.
- ❖ Mafunzo ya matumizi ya *Software* yaliyofanyika Afrika Kusini kwa wenye ujuzi wa juu ambao idadi ya ni 2.
- ❖ Mafunzo ya matumizi ya umeme, pampu, mitambo, na uchunguzi kwa wenye ujuzi wa juu na wa kati ambao idadi yao ilikuwa 60.

**c) Ushirikishwaji wa Jamii Husika**

Katika kipindi husika Kampuni ya Williamson Diamond ilishirikisha jamii katika shughuli zifuatazo:-

- ❖ Kuibua vyanzo vya maji na uenezaji wa maji katika kata ya Songwa. Mradi huo uligharimu kiasi cha shs. 28,000,000/-. Waliofaidika na mradi huu ni wakazi wa vijiji vya Songwa, Mpumbula, Seseko.
- ❖ Kutoa huduma za kiafya ikiwemo kuelimisha jamii juu ya uenezaji wa virusi vya UKIMWI, njia zipi za kuzuia maambukizi na namna ya kuishi baada ya maambukizi. Zoezi hili lilifanikishwa siku iliyotambulika kama Siku ya UKIMWI ambapo wanavijiji walishandania kombe kupitia mashindano ya mpira wa miguu. Zoezi hili lilihusisha wilaya ya Kishapu na kijiji cha Mwadui.
- ❖ Ujenzi wa ofisi mbili za Serikali za mitaa kwa Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga.
- ❖ Ujenzi wa jumla ya Madarasa 5, Ofisi 3 za walimu, madawati yasiyopungua 5,919 kwa kata za Songwa, Maganzo na Idukilo.

## 10.9. KAMPUNI YA SHANTA MINING CO. LTD

**a) Ajira**

Kampuni ya Shanta Mining Co. Ltd. ilitoa ajira kwa watanzania wenye ujuzi wa juu 254 watanzania wenye ujuzi wa kati 293 na watanzania wasio na ujuzi 141. Ajira kwa wageni zilikuwa ni 17 ambao wote walikuwa na ujuzi wa juu.

**b) Manunuzi ya Huduma na Bidhaa**

Manunuzi ya huduma na bidhaa yaliyofanywa kwa mwaka 2017 yalikuwa 8. Katika manunuzi hayo kampuni za kitanzania zilikuwa 5, za nje 2 na zenye ubia kati ya kampuni ya nje na ya ndani 1. Kampuni za kitanzania zilitoa huduma za afya, PPE, vifaa vya ujenzi na matengenezo.

**c) Mafunzo**

Mafunzo yaliyotolewa katika kipindi husika na Kampuni ya Shanta ni kama ifuatavyo:-

- ❖ Mafunzo yaliyohusisha wafanyakazi wa aina zote ni mafunzo ya huduma ya kwanza, kupambana na moto, utunzaji wa mazingira, kutambua hali hatarishi, kutambua kemikali za aina mbalimbali, n.k
- ❖ Mafunzo yaliyotolewa kwa wafanyakazi wenye ujuzi wa juu yalihusisha mafunzo ya matumizi ya mashine za uchimbaji wa mashimo marefu, Mafunzo ya usimamizi wa kazi, Sera na Taratibu za mashauri ya Nidhamu Kazini, uokoaji kwenye migodi ya madini n.k

**d) Ushirikishwaji wa Jamii**

Kampuni ilishirikiana na jamii za Mbangala, Mkwajuni, Maleza, Saza n.k kuwasaidia kujiendeleza katika maswala ya elimu, kilimo na upatikanaji wa huduma za maji.

## 10.10. KAMPUNI YA ANGLO GOLD ASHANTI- GEITA GOLD MINE (AGA-GGM)

**a) Ajira**

Ajira zilizotolewa na kampuni ya Geita Gold Mine kwa watanzania wenye ujuzi wa juu ni 898, wenye ujuzi wa kati ni 796 na wasio na ujuzi ni 21. Ajira zilizotolewa kwa watu wa nje ni 68 na wote ni wenye ujuzi wa juu tu.

**b) Manunuzi ya Huduma Na Bidhaa**

Manunuzi ya huduma na bidhaa yaliyofanywa mwaka 2017 yalizingatia masuala ya kutoa kipaumbele kwa kampuni za Kitanzania ambazo zimeshiriki zaidi katika kutoa huduma za afya, usafi, mawasiliano, chakula, tafiti za kihandisi, tafiti za mazingira na usalama, usalama na moto, kambi na malazi ya muda n.k.

**c) Mafunzo**

Kampuni ya Geita Gold Mine iliwezesha mafunzo ya wachimabji wadogo (*Artisan Training Program)*, VETA. Pia ilitoa mafunzo ya Ujuzi wa Kuongoza, uelewa wa usalama kazini, kudhibiti majanga na kudhibiti gharama na rasilimali.

## 10.11. KAMPUNI YA STAMIGOLD BIHARAMULO MINE

**a) Ajira**

Ajira zilizotolewa kwa watanzania wenye ujuzi wa juu ni 2, ujuzi wa kati 19, wasio na ujuzi ni 12.

**b) Manunuzi ya Huduma na Bidhaa**

Katika manunuzi ya huduma na bidhaa kampuni hii ilitumia gharama nyingi zaidi kwa kampuni za ndani ukilinganisha na kampuni za nje.

**c) Mafunzo**

Mafunzo yaliyotolewa ni mafunzo ya usalama ambayo yalishirikisha wafanyakazi wote.

**d) Ushirikishwaji wa Jamii**

- ❖ Kuwapatia wanafunzi kutoka vyuoni mafunzo ya kazi *(Internship)*
- ❖ Kutengeneza madawati zaidi ya 2,500 kwa ajili ya matumizi ya shule 30 za mkoa wa Kagera.
- ❖ Kuwezesha uundaji wa vikundi 3 vya ujasiriamali na kusaidia upatikanaji wa masoko kwa vijana na wanawake katika wilaya ya biharamulo.
- ❖ Ujenzi wa miundombinu
- ❖ Ujenzi wa miundombinu mbalimbali ya shule katika wilaya ya Biharamulo

## 10.12. KAMPUNI YA BULYANHULU GOLD MINE LTD

**a) Ajira**

Kampuni ya Bulyanhulu Gold mine ilitoa ajira kwa watanzania wenye ujuzi wa juu 107, ujuzi wa kati 152 na wasio na ujuzi 53. Ajira kwa wageni zilitolewa 26 kwa wenye ujuzi wa juu na 2 wa ujuzi wa kati.

**b) Manunuzi ya huduma na bidhaa**

Manunuzi ya huduma na bidhaa yalifanyika kwa kampuni za kitanzania 115 na kampuni za nje 247.

**c) Ushirikishaji wa jamii**

Jamii zilizopo katika eneo la Bulyanhulu zilinufaika kwa ujenzi wa vituo vya afya katika kijiji cha Bugarama, Wilaya ya Msalala, ujenzi wa vyoo na vyumba vya madarasa, programu za huduma za afya kwa kina mama na watoto, uboreshaji wa huduma za maji katika kijiji cha Kakola, Kuwezesha vikundi vya wachimbaji wadogo, kuwezesha biashara za kati, ujenzi wa vyoo 3 vya

jumuiya, michezo, na huduma za upasuaji kwa wagonjwa.

## 10.13. KAMPUNI YA NORTH MARA GOLD MINE LTD

**a) Ajira**

Kampuni ya North Mara Gold Mine ilitoa ajira kwa watanzania wenye ujuzi wa juu 182, ujuzi wa kati 267, wasio na ujuzi 276. Aidha, ajira kwa wageni wenye ujuzi wa juu zilitolewa 29 na ujuzi wa kati 8.

**b) Manunuzi ya Huduma na Bidhaa**

Manunuzi ya huduma na bidhaa yalifanyika kwa kampuni za kitanzania 169 na kampuni za kigeni 326.

**c) Ushirikishaji wa jamii husika**

Kampuni iliweza kuanzisha miradi mbalimbali kama vile ya kuibua vyanzo vya maji katika eneo la Nyamwaga, ujenzi wa madarasa katika shule ya msingi Bong'eng'e, ujenzi wa ofisi ya kata ya Nyarokoba, ujenzi wa kituo cha afya cha Nyamwaga, n.k.

## 10.14. KAMPUNI YA PANGEA MINERALS LIMITED

**a) Ajira**

Kampuni ya Pangea Minerals Limited ilitoa ajira kwa watanzania wenye ujuzi wa juu 83, ujuzi wa kati 96 na wasio na ujuzi 118.

**b) Manunuzi ya huduma na bidhaa**

Manunuzi ya huduma na bidhaa yalifanyika kwa kampuni za kitanzania 137 na kampuni za kigeni 225.

**c) Ushirikishaji wa jamii**

Kampuni imeboresha barabara ya ndege kwenye kiwanja cha ndege cha Kahama, ujenzi wa madarasa manne katika shule ya msingi Mwendakulima B, ujenzi wa bweni katika shule ya sekondari Mwendakulima linaloweza kuhifadhi wanafunzi 100, kuanzisha mradi wa kupanda miti ya matunda ambapo mbegu 180,000 zilipandwa, utoaji wa michango mbalimbali ya kifedha ya kusaidia jamii zilizokumbwa na maafa au wenye mahitaji maalum, huduma za upasuaji, michezo n.k

Kazi nyingine iliyofanyika ni "*Marine Oil Terminal Storage and Export Jetty*". Katika kazihii Mkandarasi Mkuu ni kampuni ya nje. Huduma zote za usafirishaji, magari ya wagonjwa na huduma za afya eneo la kazi, *Surveyor Technicians* na usafiri wa majini, ajira za muda (Casual Labour) zilifanywa na kampuni na taasisi za Tanzania.

## 10.15. TAFITI NA MIKUTANO

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limefanya Tafiti Bainifu kuhusu Ushiriki wa Watanzania katika sekta ya Ujenzi, Kilimo na Uzalishaji. Tafiti hii imetoa mapendekezo ya masuala muhimu ya kuzingatia ili kuongeza ushiriki wa watanzania katika sekta hizo tatu katika mnyororo mzima wa thamani. Sekta hizi tatu ni muhimu sana katika kuchangamsha uchumi wa Tanzania wakati huu ambapo tunatekeleza miradi mablimbali ya kimkakati. Kwa kuwa Miradi yote ambayo inatekelezwa hapa nchini inahitaji ujenzi, mazao ya kilimo vikiwemo viwanda ambavyo vinahitaji mali ghafi na vilevile shughuli za uzalishaji kwa ujumla.

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi likishirikiana na taasisi zingine za Serikali lilifanya Kongamano la Ushiriki wa Watanzania katika mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Uganda hadi Tanzania (EACOP). Kongamano hili lilikuwa na lengo la kuwafahamisha wadau mbalimbali hasa sekta

binafsi fursa zilizopo katika mradi huu. Kongamano hili lilihudhuriwa na wafanyabiashara wapatao 450. Baraza linafanyia kazi mapendekezo yaliyotolewa kwenye mkutano huo ikiwemo kutengeneza tovuti itakayotoa taarifa ya fursa zilizopo katika miradi mbalimbali ya kimkakati inayotekelezwa hapa nchini.

Kwa ujumla Serikali imeweka mazingira mazuri ya ushiriki wa watanzania katika uwekezaji hasa katika sekta ya uziduwaji. Aidha, miradi mbalimbali imetumia nguvu kazi, huduma na bidhaa za kitanzania. Hata hivyo bado kuna haja ya kufuatilia na kupima ongezeko la thamani katika uchumi wa nchi kutokana na ushiriki huo katika miradi iliyopo kwenye sekta mbalimbali.



# UWEZESHAJI WA WAKULIMA NA VIWANDA

# 11.0. UWEZESHAJI WA WAKULIMA NA VIWANDA

Katika kipindi cha Julai, 2017 hadi April, 2018 Baraza limeendelea kuwezesha wananchi kiuchumi kwa kuainisha maeneo yenye matokeo ya haraka na kutekeleza kama ifuatayo:

## 11.1. KURATIBU WAKULIMA WA NJE WA MIWA KWA AJILI YA KIWANDA CHA MKULAZI

Baraza liliwezesha wananchi katika kata sita ambazo ni Mbigili, Magole, Dumila, Kitete, Msowero na Mvumi zinazozunguka kiwanda cha Mkulazi wilayani Kilosa ili waweze kushiriki katika kilimo cha miwa kwa mfumo wa wakulima wa nje (Out growers scheme). Ilionekana kuwa kuna haja ya wakulima wa maeneo yanayolima miwa kwa ajili ya Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi wawe kwenye Vyama vya Ushirika vya Kilimo. Hii ni kwa mujibu wa matakwa ya marekebisho ya Sheria ya Sukari ya mwaka 2016. Hivyo, Baraza limeshirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC) pamoja na Mkulazi – Holding Company (MHC) ambayo ni Kampuni hodhi inayomilikiwa na NSSF na PPF katika kuhamasisha, kuunda na kusajili AMCOS (*Agricultural Marketing Cooperative Societies*- AMCOS) tatu ambazo ni Msowero; Mbigili na Makiwami.

Baraza pia liliwezesha upimaji wa mashamba ya wakulima wa miwa ili kupata vipimo halisi vya mashamba ya wakulima hao. Zoezi hili lilifanywa kwa kushirikiana na MHC, Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa na ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Kilosa. Wapimaji wa Ardhi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ndiyo waliohusika katika zoezi hilo. Katika kutekeleza zoezi la kupima mambo yaliyozingatiwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa mashamba yanayopimwa hayana migogoro kati ya wakulima kwa wakulima; wakulima na wafugaji; wakulima na vijiji; Vijiji na Vijiji; na Vijiji na Taasisi za Serikali kama vile Jeshi la Magereza. Maeneo yenye hati tayari hayakupimwa bali yalifanyiwa uhakiki tu kwani vipimo vyake vinaeleweka na hata matumizi yake yameoneshwa kwenye nyaraka za umiliki. Jumla ya mashamba 79 yenye ukubwa wa ekari 6890.33 yalipimwa. Serikali ya Wilaya imewapatia Vijana wa chama cha Msowero ekari 300 ili waziendeleze kwa kilimo cha Miwa.

Wakulima wa nje wameanza kuandaa mashamba ambapo mpaka April, 2018 jumla ya ekari 1500 zililimwa. Mpango ni kuendelea hadi kufikia ekari zote zilizopimwa iwapo hakutakuwa na kikwazo cha kufikia kutokana na mvua. Mpango uliopo ni kumilikisha ardhi kwa wakulima wa nje kwa ajili ya Mkulazi, kwa kushirikiana na MKURABITA ambao watahusika katika utoaji wa Hati za Kimila (Customary Certificate of Right of Occupancy-CCRO). MKURABITA itafanya kazi hii kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa ili baadae Halmashauri iendelee na kazi ya utoaji wa Hati za kimila. Mkurabita ilishajenga uwezo wa upimaji wa ardhi wa Halmashauri ya Kilosa na jinsi ya kutoa na kusajili Hati za Kimila. Baraza litafuatilia utoaji wa hati hizo ili ziweze kutumika na wadau mbalimbali ikiwemo kuombea mikopo kwa ajili ya kilimo cha miwa.

Baraza lilitakiwa kuwezesha wakulima hawa kwa kuwapatia fedha kwa ajili ya Mkopo kwa njia ya dhamana kupitia Mfuko wa Uwezeshaji wa Mwananchi. Baraza liliamua kutumia fursa hii kwa kuhusisha taasisi za fedha na mifuko mingine ya uwezeshaji. Baraza liliwaunganisha wakulima na Benki ya Kilimo na Benki ya Azania ili kuwezesha Kilimo hiki kwa kuwa riba ya Benki hizi ni ndogo ukilinganisha na vyanzo vingine vya fedha. Hadi Aprili, 2018 Azania Benki ilikuwa imekwishatoa mikopo yenye thamani ya ziadi ya bilioni nne. Mikopo hii imetolewa kupitia watoa huduma za mashambani (Makandarasi) kuanzia ukatuaji wa kwanza, ukatuaji wa pili, uwekaji wa matuta na mbegu pamoja na upandaji. Uwezeshaji huo umetolewa kwa njia ya wakulima kupewa huduma na pembejeo husika na siyo fedha. Taasisi nyingine za fedha zimejitokeza ili zifanye uwezeshaji. Taasisi hizo ni pamoja na CRDB- Benki.

## 11.2. KUUNGANISHA WAKULIMA WA MAENBE NA KIWANDA CHA AZAM

Baraza limeendelea kutafuta masoko ya kilimo kwa kuwashirikisha TanTrade na wawekezaji wakubwa wanaosindika mazao hapa nchini. Kampuni ya Azam-Bakhresa imeonesha nia ya kununua Maembe kwa ajili ya kusindika Juisi. Maembe ambayo yatakuwa kwenye mpango huu yatalimwa kwa mikataba na mashamba yanatakiwa kuwa na eneo kuanzia eka mia moja (100) na kuendelea.

Baraza limewasiliana na Ofisi nane za Mikoa yenye mazingira yanayofaa kwa kilimo cha maembe. Mikoa hiyo ni Morogoro, Ruvuma, Singida, Simiyu, Shinyanga, Lindi, Tabora, Kigoma, Tanga na Dodoma. Mkoa wa Ruvuma umeweza kuainisha idadi ya hekta **77,238.6 ambazo** zinafaa kwa kilimo cha Maembe ili utaratibu uendelee kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| a. Mbinga Vijijini Hekta | 211 |
| b. Mbinga Mji Hekta | 2,086 |
| c. Songea MC Hekta | 1,241.6 |
| d. Songea DC Hekta | 72,580 |
| e. Tunduru DC Hekta | 635 |
| f. Nyasa DC Hekta | 105 |
| g. Namtumbo DC Hekta | 130 |
| h. Madaba DC Hekta | 250 |
| **Jumla Hekta** | **77,238.6** |

Baraza kwa kushirikiana na Mkoa wa Ruvuma limeainisha mahitaji ya rasilimali zinazohitajika katika utekelezaji wa mradi huu ambao unalenga kuongeza kipato cha kaya na taifa kwa ujumla ili mpango huu uanze. Malengo ni kuhakikisha kuwa kilimo hiki kinaanza mapema mwaka 2019. Baraza linafuatilia ili kuhakikisha kuwa mikataba inamnufaisha Mwananchi na kuleta tija kwa mkulima atakayeshiriki katika mpango huu.

### 11.3. KUSHIRIKIANA NA TASAF KUWAINGIZA WANANCHI KUTOKA KAYA MASKINI KWENDA SHUGHULI KIUCHUMI

Baraza limeshirikiana na TASAF katika kutekeleza mpango wa matokeo ya haraka. Kwa kupitia Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP) walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini katika maeneo ya majaribio (Kibaha, Halmashauri ya Mtwara na Unguja) wamehamasishwa kulima zao moja ambalo linastawi katika eneo husika ambapo, Kibaha na Halmashauri ya Mtwara ni Mihogo na Chamwino ni Alizeti. Walengwa wameunganishwa na huduma za ugani kwa maafisa kilimo wa vijiji na kata ili waweze kupata utaalamu wa jinsi ya kulima zao husika. Mpango huu utagharamia eneo ambalo limetengwa kwa ajili ya jaribio kuanzia kuandaa shamba hadi kuvuna wakati mashamba ya walengwa watajigharamia wenyewe. Madhumuni ya mpango huu ni kuwajengea walengwa wa mpango wa kunusuru kaya masikini ili wazalishe wenyewe kwa kutumia utaalamu ili wafanye kilimo chenye tija. Nia ni kuanza kuwaondoa taratibu katika mpango wa kupata fedha za kujikimu pasipo kufanya shughuli yeyote. Kazi ya Baraza katika mpango huu ni kushiriki kuanzia mwanzo ili kuweza kuwaunganisha na huduma mbalimbali za uwezeshaji. Mpango umeanza mwezi Desemba, 2017 na unatarajia kukamilika mwishoni mwa mwezi Novemba, 2018 mara baada ya mavuno ya mazao husika. Lengo la Mpango huu ni kuyasambaza matokeo mazuri kwenye maeneo mengine ya Tanzania.



# UJASIRIAMALI

# 12.0. UJASIRIAMALI

Ujasiriamali ni moja ya nguzo tisa za Sera ya Taifa ya Uwezeshaji ambayo inalenga kuinua viwango vya ujuzi na uzoefu ili kuendeleza ujasiriamali. Sera imeweka mikakati inayolenga kujenga wananchi wenye kujiamini, wabunifu na wenye ari ya kuzalisha mali. Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi limeendelea kuratibu Ujasiriamali kama ilivyoanishwa katika Sera ya Taifa ya Uwezeshaji na Sheria ya Uwezeshaji za mwaka 2004. Katika kipindi cha kuanzia Julai 2017 mpaka Mei 2018 majukumu yafuatayo ya uratibu wa ujasiriamali yametekelezwa:

## 12.1. KAMATI YA TAIFA YA MAENDELEO YA UJASIRIAMALI

Ili kuendelea kuimarisha uratibu wa ujasiriamali nchini Serikali limeunda Kamati ya Kitaifa ya Maendeleo ya Ujasiriamali. Kamati hii inajumuisha wataalamu kutoka sekta ya umma na binafsi. Lengo kuu la Kamati ni kuleta wataalamu wa ujasiriamali pamoja ili kuimarisha ujasiriamali na kushauri fursa za ujasiriamali zenye tija. Hii italiwezesha Baraza kuweza kutumia utaalam huo ili kuweza kuishauri serikali kuhusu fursa za ujasiriamali. Aidha, Kamati itashauri uratibu mzuri ili kuondokana na changamoto zinazoikumba sekta ya ujasiriamali nchini.

## 12.2. MKAKATI WA TAIFA WA UJASIRIAMALI

Pamoja na juhudi za Serikali kuboresha mazingira ya ujasiriamali bado kumekuwepo na changamoto zinazoikumba sekta ndogo za ujasiriamali na maendeleo ya biashara. Ili kupambana kikamilifu na changamoto hizo Serikali kwa kushirikiana na wadau iliandaa Mkakati wa Taifa wa Ujasiriamali ambao umejikita katika maeneo muhimu yaliyotafitiwa ili kuhakikisha kuwa Tanzania inaimarisha ujasiriamali kwa kuondokana na changamoto inayoikumba sekta hii. Mkakati huo ulizinduliwa tarehe 12 Desemba, 2017.

Mkakati umeainisha maeneo matano yafuatayo:

i. **Kuboresha Sheria na kanuni za kuendeleza ujasiriamali.**
   Kupunguza changamoto za kiutawala wa uanzishaji na uendelezaji wa biashara na ujasiriamali hasa katika urasimishaji, upatikanaji wa taarifa, gharaza za urasimishaji na mikataba;

ii. **Kuimarisha Elimu ya Ujasiriamali**
Kuutambua ujasiriamali kama somo na kulihuisha katika ngazi zote za elimu rasmi na vyuo vya ufundi. Aidha, mkakati unasisitiza kuimarisha elimu ya ujasiriamali isiyo rasmi na maendeleo ya ujuzi kwa vitendo.

iii. **Kuwezesha Teknolojia na ubunifu.**
Kuwezesha sekta ya umma na binafsi kubadilishana utaalam, kuendeleza tafiti za viwanda na ubunifu kwa ajili ya maendeleo na kuimarisha biashara na huduma kwa njia ya TEHAMA.

iv. **Kuboresha upatikanaji wa mitaji**
Kutoa huduma za kimtaji kwa makundi maalum kama wanaoanza biashara na biashara zinazogusa wanufaika wengi kwa makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Aidha, eneo hili linashauriwa kuimarisha sekta ya fedha ili kuhudumia sekta binafsi kwa kuongeza utoaji wa huduma mbalimbali za kifedha kwa gharama nafuu.

v. **Kuimarisha Uhamasishaji na Mitandao ya Kibishara**
Kujenga utashi wa kijasiriamali huku tukizikabili changamoto za kitamaduni hasa zile zinazokandamiza wanawake wajasiriamali.

Mkakati wa Taifa wa Ujasiriamali umeainisha majukumu ya taasisi mbalimbali za umma na za binafsi ambayo yakitekelezwa kwa ufanisi yatawezesha kumaliza changamoto zinazoikumba sekta ndogo ya ujasiriamali na maendeleo ya sekta binafsi.

Aidha, Serikali imefanya jitihada za kimkakati kuboresha mazingira ya ujasiriamali na biashara kwa kufanya mageuzi katika uboreshaji wa mazingira ya kufanyia biashara na ujasiriamali. Baadhi ya maboresho ni kuboresha upatikanaji wa leseni za biashara; kuboresha mazingira ya uwekezaji katika kituo cha Uwekezaji Tanzania ambapo huduma mbalimbali za kiuwekezaji zinatolewa kituoni na kwa haraka, Wakala wa Usajili wa Biashara (BRELA) imeanzisha mfumo ya usajili na huduma nyingine kwa mtandao. Pamoja na juhudi hizo bado suala la urasimishali limekuwa na changamoto. Ni kwa misingi hii kuwa Mkakati wa Taifa ya Ujasiriamali umeainisha nguzo ya **Kuboresha Sheria na kanuni za kuendeleza ujasiriamali kama eneo la kimkakati ili kufanyia kazi changamoto zinazozuia ufanisi katika eneo la urasimishaji. Mkakati utajikita katika maeneo yafuatayo:**

| KIKWAZO | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|
| Kukosekana utaratibu mahususi wa kuchambua mchakato na gharama za kuanzisha biashara | ❖ Kulinganisha gharama na muda unaotumika kuanzisha biashara rasmi katika serikali za mtaa.<br>❖ Kuanzisha utaratibu wa kisheria wa kuchambua kwa mapana athari za mabadiliko ya sera na sheria kwa biashara kabla hazijapitishwa.<br>❖ Kushawishi upande wa serikali kuheshimu majukwa ya kujadiliana na sekta binafsi katika ngazi ya wilaya, mkoa, sekta na taifa. |
| Mchakato mrefu na gharama kubwa za kuandikisha biashara na kupata leseni | ❖ Kuboresha na kurahisisha taratibu za kuandikisha, kutoa leseni na kulipa kodi ikiwemo kuboresha matumizi ya mtandao.<br>❖ Kutekeleza kwa ukamilifu na makini Mpango wa Kuboresha Sheria na Kanuni za Biashara (Blueprint on business regulatory licensing reforms).<br>❖ Kuanzisha vituo vya huduma (One Stop Centres) kwenye serikali za mitaa kuweka taratibu za uandikishaji na utoaji leseni pamoja. |

| KIKWAZO | HATUA ZA KUCHUKUA |
|---|---|
| Kutofautiana taratibu na kukosekama uwazi na miongozo katika ulipaji kodi | ❖ Kuondoa utaratibu wa kulipa kodi ya mapato kabla ya kuanza biashara.<br>❖ Kuanzisha utaratibu wa kusuluhisha migogoro ya kibiashara ambao unaweza kutumiwa na biashara ndogo na za kati.<br>❖ Kuanzisha utaratibu wa kutoa elimu kuhusu haki miliki na utatuzi wa migogoro ya kibiashara kwa njia ya usuluishi. |
| Kutokuwepo utaratibu wa kusheria na kikanuni unaotekelezeka na biashara ndogo kabisa (Zaidi ya asilimia 90 ya biashara zote) ambazo haziwezi kurasimishika kwa utaratibu wa kawaida | ❖ Kuanzisha utaratibu wa kutoa elimu ya kuandikisha, kupata leseni na kutimiza masharti mengine ya kisheria ya kuendesha biashara kwa kutumia mtandao.<br>❖ Kuanzisha sera maalumu kutoa vivutio kwa biashara kurasimishwa.<br>❖ Kuanzisha mfumo maalumu wa kisheria kwa ajili ya kurasimisha biashara ambazo hazijafikia kiwango cha kupata leseni ya kawaida.<br>❖ Kuimarisha Madawati ya Uwezeshaji kwenye halmashauri za Wilaya. |

## 12.3. KURATIBU MAENDELEO YA BIASHARA YA SEKTA NDOGO NA YA KATI

Baraza limeendelea kuratibu maendeleo ya Biashara ndogo na za Kati (MSMEs) kwa lengo la kuwezesha watanzania kumiliki sehemu kubwa ya uchumi kwa kuwekeza katika fursa mbalimbali.

### a. *Kutambua Watoa Huduma za Maendeleo ya Sekta Ndogo na za Kati*

Sekta ya biashara ndogo na za kati imekuwa ikikumbana na changamoto nyingi ikiwemo ukosefu wa huduma bora za maendeleo ya biashara. Watoa huduma hizo hawana mfumo rasmi wa kuwaratibu ili kuhakikisha ubora wa huduma wanazotoa sambamba na kutambua mahitaji na idadi halisi. Baraza linaratibu utambuzi wa watoa huduma hao ili kuweza kuandaa kanzi data ya watoa huduma. Serikali inahimiza watoa huduma wote wa kuendeleza sekta ndogo na kati waweze kujisajili kwenye Baraza ili kuweza kutambuliwa. Kanzi data ya watoa huduma za kuendeleza biashara itaiwezesha serikali kutambua huduma mbalimbali zilizopo ili kuweza kuwatumia watoa huduma hao katika kuwajengea uwezo watanzania ambao watakua na sifa za kutoa huduma katika miradi mikubwa inayoendelea nchini.

Lengo kubwa ni kuhakikisha kuwa watoa huduma wa Maendeleo ya Sekta Ndogo na za Kati wanawezesha kutatua changamoto za kujengea uwezo wajasiriamali na wafanyabiashara hasa katika eneo la urasimishaji wa Biashara. Urasimishaji wa biashara katika sekta ndogo na za kati umekuwa na changamoto kubwa kama ilivyobainishwa katika Taarifa ya Kitaifa ya kuainisha mfumo mzima wa Uwezeshaji wa Wajasiriamali (***Mapping and Assessment of the Entrepreneurship Ecosystem in Tanzania***), ambapo ilibainika kuwa **asilimia 89%** ya Biashara katika Sekta Ndogo na za Kati hazijarasimishwa. Kukamilika kwa utambuzi wa watoa huduma za maendeleo ya biashara kutaiwezesha Serikali kuratibu huduma zinazotolewa pamoja na kuwajengea uwezo wafanyabiashara na wajasiriamali katika sekta isiyo rasmi ili kuimarisha shughuli zao.

### b. *Kuhuisha kiongozi cha kitaifa cha Mafunzo ya Ujasiriamali Katika Mfumo Usio Rasmi*

Mwongozo wa Taifa wa Ufundishaji Ujasiriamali (***National Entrepreneurship Training Framework* – NETF**) umeainisha maeneo ya kipaumbele kwa sekta isiyo rasmi. Watoa huduma wamekuwa wakitumia mada zinazotofautiana katika kutoa huduma za maendeleo ya biashara. Baraza kwa

kushirikiana na wadau linaandaa *Standardized Entrepreneurship Training Guide* ambayo itafuata maelekezo ya NETF pamoja na rejea za mada ambazo tayari zinafundishwa katika sekta isiyo rasmi. Watoa huduma za kujengea uwezo wajasiriamali watatumia kiongozi hiki cha mafunzo katika kujengea uwezo wa wajasiriamali na wafanyabiashara katika mfumo usio rasmi. Lengo ni kuhakikisha kuwa watoa huduma wanatoa mafunzo ubora na linganifu ili kuweza kupima ufanisi na matokeo chanya kwa wajasiriamali na wafanyabiashara.

### *c. Kutambua na Kurasimisha Wafanyabishara Wadogo kwa Vitambulisho*

Kifungu cha 57(iii) cha Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2015 kimeazimia kuwarasimisha wafanyabiashara wadogo ili biashara zao ziweze kutambulika kisheria ili waweze kupata leseni na kujengewa uwezo kwa mafunzo na kuunganishwa na asasi za fedha ili kupata mikopo. Wadau mbalimbali wa umma na binafsi wanafanya jitihada za kuwezesha wafanyabiashara ndogondogo, mfano mojawapo ni Manispaa ya Ilala, mkoani Dar es Salaam wameanza kuwatambua na kuwarasimisha wafanyabiashara wadogo (wamachinga) kwa kuwapa vitambulisho. Lengo likiwa ni kuwa na kanzidata zao kwa ajili ya mahitaji mbalimbali ya kuwawezesha ikiwemo maeneo tengefu kwa ajili ya biashara, kurasimisha biashara zao pamoja na huduma nyinginezo. Hatua hii itasaidia kuondoa kero na malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara wadogo. Halmashauri ya Ilala imefanikisha mradi huu katika maeneo yafuatayo:

- ❖ Kuweka wafanyabiashara wadogo (wamachinga) pamoja na kuunda umoja wao ambao ulizinduliwa wakati wa mbio za mwenge mwaka 2017.
- ❖ Wamachinga kuchangia huduma za manispaa kama gharama za usafi, ulinzi na kodi.
- ❖ Vitambulisho vya Taifa ambavyo viliambatana na wamachinga kuwa na Kadi ya Mlipa Kodi (TIN) ambayo ina namba ya uraia, namba ya meza ili iwe rahisi kuwapanga.

Tayari Halmashauri zimeanza kutembelea Halmashauri ya Manispaa ya Ilala kujifunza kwa ajili ya kutekeleza katika Halmashauri zao.

### *d. Kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi Biashara Ndogo na za Kati na Kuanzisha Mfuko wa Wajasiriamali*

Ilani ya Chama cha Mapinduzi Sura ya 5 kipengele cha 57 (vi na v) vimeahidi kuwezesha wananchi Kichumi kwa kuanzisha Mamlaka ya Usimamizi wa Biashara ndogo na Kati (SMEs) na kuanzisha Mfuko Mkubwa wa kitaifa wa wajasiriamali wadogo na wa kati kwa kushirikiana na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na Asasi nyingine za Kifedha. Kwa sasa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na wadau wanaandaa mfumo wa uratibu wa SMEs na mwongozo wa Mfuko wa Kuwezesha Wajasiriamali Tanzania.



# UWEZESHAJI WA VIJANA

# 13.0. UWEZESHAJI WA VIJANA

Sera ya Vijana Tanzania ya mwaka **2007** inatambua kuwa vijana ni watu wote wenye umri wa kuanzia miaka **15 hadi 35** ambapo kulingana na Sensa ya mwaka **2012 ni asilimia 34.7** ya watu wote nchini. Kundi hili kubwa ndio nguvu kazi ya Taifa lakini pamoja na hayo limekuwa likiathiriwa na tatizo la ajira na dhamana ya mikopo hasa wanapozisogelea taasisi za kifedha ili kupata mitaji ya kuendesha shughuli za uzalishaji mali.

Serikali ya Awamu ya Tano kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa sekta binafsi imekuwa ikiendesha program za uwezeshaji kwa vijana ili kuwakwamua na tatizo sugu la ajira.

Uwezeshaji wa vijana umekuwa ukifanyika kwa njia kuu mbili ambazo ni mafunzo ya ujasiriamali na kupewa dhamana au mikopo kutoka kwenye taasisi za fedha au mifuko ya uwezeshaji inayoratibiwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Miongoni mwa programu zinazotekelezwa nchini ni kama inavyoelezwa hapo chini.

## 13.1. PROGRAMU YA KIJANA JIAJIRI

Programu ya **Kijana Jiajiri** imeanzishwa **mwaka 2015** inatekelezwa na Taasisi ya Ujasiriamali na Ushindani Tanzania (TECC) chini ya ufadhili wa makampuni ya mradi wa **Tanzania LNG na Benki ya Barclays** ambapo vijana wenye rika la kuanzia miaka 18-35 hupatiwa mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali, kuwekwa kwenye malezi na kuunganishwa na fursa za mikopo ili waweze kuanzisha miradi ya ujasiriamali. Programu hii inatekelezwa kwa mtindo wa kutoa mafunzo ya ujasirimali kwa kipindi cha miezi miwili, baada ya hapo vijana huunganishwa na wafanyabiashara wazoefu kwa kipindi cha mwaka mmoja, ambayo pia hujulikana kama **Malezi**. Baada ya hapo vijana wenye mahitaji ya mitaji huunganishwa na vyombo vya fedha kwa ajili ya mikopo nafuu. Programu kwa hatua za majaribio inatekelezwa kwenye Mikoa ya Dar es salaam, Morogoro, Lindi na Mtwara.

Utekelezaji wa Programu, kwenye mafunzo hufanywa na SIDO, kuunganishwa kwa vijana na wafanyabiashara wazoefu hufanywa (malezi) na TCCIA na mikopo mingi hutolewa na mifuko ya

uwezeshaji.

Tangu kuanzishwa kwake mpaka hivi sasa imeweza kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa **vijana 1030** sambamba na kuanzishwa kwa jumla ya **miradi 260 ya uzalishajimali** kwa njia za mikono ambapo 82% imeonyesha mwelekeo wa kukua. Mwezi Machi mwaka 2018 zoezi la utoaji wa mafunzo liliendelea katika mkoa wa Lindi na kuhudhuriwa na vijana 70 hivyo kuwa na jumla ya **vijana 1100** walionufaika na mafunzo ya Kijana Jiajiri. Vijana waliopatiwa mikopo kupitia mifuko ya Uwezeshaji mpaka hivi sasa ni vijana **61 yenye thamani ya Tshs 87,3000,000.** Mkoa wa Dar es salaam **vijana 11** kupitia mfuko wa PTF, Morogoro **vijana 38** (SIDO na PTF), Lindi (SIDO) vijana 8 na Mtwara SIDO vijana wanne (4).

*Glory Nyandindi* ana umri wa miaka 29, anaishi mtaa wa Chikongola Mkoani Mtwara. Alililewa na Shangazi ya baada ya mama yake mzazi kufariki mwaka 2008 wakati huo alisoma huku akifanya kazi kwenye duka la Shajala ili aweze kuwatunza wadogo zake.

*"maisha yalikuwa magumu sana, ilibidi nitafute kaziwakati nasoma ili tuweze kumudu maisha na wadogo zangu"*

Baada ya kumaliza chuo mwaka 2010, alijaribu kutafuta kazi ya kuajiriwa lakini hakupata. Hivyo mwaka 2013 Glory na kaka yake waliamua kufungua duka lao la Shajala, wakati huo wakiwa na mtaji wa shilingi 200,000, fedha hizi ni akiba aliyoweka kutokana na kazi ya mwanzo.

*Mafanikio*: Baada ya kuingia kwenye programu ya Kijana jiajiri mwaka 2015, alipata ujuzi wa kuendesha biasharana jinsi ya kutandaa na wenzake na pia kuunganishwa na taasisi za fedha (SIDO). Duka lake sasa hivi limekuwa sana mpaka kufikia mtaji wa shilingi 25,000,000 ameajiri wafanyakazi wawili na anawalipa shilingi 250,000 kwa mwezi. anategemea kufungua jingine Mkoani Lindi



## 13.2. PROGRAMU YA KIJANA JIANDALIE AJIRA

Programu hii ilianzishwa mwaka 2016 inatekelezwa na TECC kwa ufadhili wa **Shirika la Kimataifa la Vijana (International Youth Foundation)** likiwa na lengo la kuwajengea uwezo vijana wenye rika la umri wa miaka 18-25 kujiandalia ajira zinazotokana na ubunifu wao. Katika programu hii vijana pia hunufaika na malezi toka kwa washauri walioandaliwa kutoka Chemba za Biashara sambamba na kuunganishwa na fursa za mikopo kwa wahitaji. Programu hii inatekelezwa kama ya Kijana Jiajiri, isipokuwa jambo la msingi linaloongezeka kweye programu hii ni stadi za maisha kwa vijana. Halmashauri za Wilaya husika huhusishwa katika programu na VETA ili kupata uendelevu.

Kijana Jiandalie Ajira inatekelezwa katika mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Dodoma na Mtwara katika hatua za awali. Mpaka hivi sasa imeweza kuwafikia jumla ya vijana **1041 huku wanawake wakiwa ni 51%.**

Katika programu ya malezi mpaka hivi sasa imewafikia **vijana 222** ambapo **wanawake ni 45%** wakati vijana ambao wanaendelea kuwa chini ya malezi hayo wakiwa ni **117 ambapo wanawake ni 60%.**

## 13.3. WIKI YA VIJANA KITAIFA

Kupitia wiki ya vijana kitaifa ambapo mwaka huu jumla ya **vijana 1020** kutoka Tanzania Bara na Visiwani

walishiriki katika kongamano na kujadili masuala muhimu ikiwa ni pamoja na Maendeleo endelevu ya Dunia, Vijana katika kujenga amani, Vijana na Maendeleo ya viwanda pamoja na kupambana na ukatili wa Kijinsia. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na UNICEF kupitia mradi wa **U-Report** imeendelea kuwashirikisha vijana katika kutoa mawazo yao.

### 13.7. MAFUNZO KWA WAHITIMU WA VYUO

Ili kuwezesha wahitimu wa elimu ya juu kupata mikopo na kuanzisha makampuni, OWM- KVAU imetekeleza Program ya Kukuza Ujuzi ambapo jumla ya vijana **11,340** (wakiwemo wa elimu ya juu) wamepewa mafunzo mbalimbali ya stadi za kazi kwa lengo la kuhakikisha wanapata ujuzi wa kuajirika au kujiajiri wenyewe.

### 13.8. KUTENGA MAENEO YA VIJANA

Katika kutekeleza jukumu la kusimamia maendeleo ya vijana nchini, OWM imeendelea na kazi ya kuratibu utengaji wa maeneo ya kufanyia kazi kwa Vijana ambapo mpaka sasa, Mamlaka za Serikali za Mitaa **72** zimetenga maeneo yenye jumla ya **ekari 84,037** kwa ajili ya shughuli za kilimo, biashara, ufugaji na huduma kwa Vijana. Aidha, OWM imetoa maelekezo kwa Wakuu wa Mikoa kusimamia utekelezaji majukumu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizo chini yao.

### 13.9. PROGRAMU YA KUKUZA UJUZI

Katika Mwaka wa Fedha 2017/18 kiasi cha **shilingi 1,075,000,000/=** kimetengwa kwa ajili ya kutoa nyenzo za kazi kwa vijana walio katika vikundi mbalimbali kupitia programu ya kukuza ujuzi.

Pia, katika progamu ya kukuza ujuzi nchini, imetenga jumla ya **shilingi 7,237,000,000/=** kwa ajili ya kuwezesha mafunzo kwa vitendo kazini kwa **wahitimu 4,000** kwa kushirikiana na waajiri. Kuwawezesha Vijana wanaohitimu Vyuo Vikuu na Vyuo vya Kati kufanya kazi kwa kujitolea katika asasi mbalimbali kwa lengo la kuwapatia uzoefu na maadili ya kazi ili waweze kuajirika au kujiajiri wenyewe.

### 13.10. MFUKO WA MAENDELEO YA VIJANA (YDF)

Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) ulianzishwa na Serikali kwa lengo la kuwawezesha vijana kupata mitaji kwa njia ya mikopo yenye masharti nafuu ili kuanzisha au kuendeleza miradi ya uzalishaji mali. Kupitia utaratibu huu, vijana huwezeshwa kujitegemea, kupunguza umasikini wa kipato na kujiajiri wenyewe. Aidha, mikopo itolewayo kupitia mfuko huu huwasaidia vijana kujenga tabia ya kukopa kwa busara na kurejesha kwa wakati.

Mfuko huu pia husaidia kuratibu shughuli za mafunzo ya uzalishaji kwa vijana wa Tanzania Bara. Katika kipindi hiki jumla ya mikopo yenye thamani ya Shilingi **783,283,000.00** ilitolewa kwa vikundi vya **vijana 840** na kufanikisha uanzishwaji wa miradi **120** katika Halmashauri **37** .

Jumla ya shilingi **28,540,317,857.25** zilitengwa kwenye bajeti za Halmashauri zote kwa ajili ya mfuko wa vijana na kiasi cha shilingi **7,816,656,382.00** zimetolewa katika mwaka huu.

### 13.11. PROGRAMU YA MAFUNZO YA UJASIRIAMALI KWA VIJANA WA JKT

Jeshi la Kujenga Taifa nchini (JKT) mbali na kuwaandaa vijana kuwa wazalendo katika nchi yao lakini pia limeendelea kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana ili kwa wale wanaokosa sifa za kuajiriwa waweze kuingia moja kwa moja katika shughuli za uzalishajimali. NEEC kwa kushirikiana na JKT waliendesha mafunzo kwa walimu wote wa JKT nchini ili waweze kutoa elimu hiyo kwa vijana katika Kambi zote nchini na uwe ni utaratibu endelevu wa JKT kutoa mafunzo hayo.

Katika Opareshini Kikwete kwa vijana waliomaliza **Desemba mwaka 2017 JKT** imeweza kutoa

mafunzo kwa jumla ya **Vijana 4,605 ambao ni wahitimu** kutoka Mikoa yote ya Tanzania Bara.

Katika kundi hilo vijana waliofanikiwa kupata ajira walikuwa **3,000** ambao wameajiriwa na vyombo vya Ulinzi na usalama huku vijana **1,605** wakirejea majumbani na vyeti vya mafunzo lakini wakiwa na ujuzi wa biashara, ushirika, vikundi, masoko na ujasiriamali.

Mafanikio ambayo yametokana na Programu hii kwanza ni vijana wenyewe kuwa na uwezo wa kuanzisha shughuli zao za kiuchumi. Pili, vijana waliomaliza Kambi ya Mlale Ruvuma, wameanzisha kiwanda kikubwa cha kuchakata mahindi ambapo kiwanda hiki kimeanzishwa kwa kushirikisha vijana 30 pamoja na JKT wenyewe. Kambi zingine pia zimefanya shughuli mbalimbali kama vile Vikosi vya Rwamkoma Mara na Bulombora Kigoma wameanzisha uvuvi wa vizimba. Kikosi cha Itende Mbeya wanaandaa viwanda vidogo vya kuchakata nyanya, asali na kufyatua matofali. Kikosi cha Mafinga kimeanzisha kiwanda kidogo cha viatu.

## 13.12. MASHIRIKA YASIYOKUWA YA KISERIKALI

Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali pia yamekuwa na mchango muhimu katika kufanikisha uwezeshaji kwa vijana kupitia mafunzo mbalimbali ambayo yamekuwa yakiendelea kwa kushirikia na Taasisi za Serikali na sekta Mashirika ya Kimataifa.

Tanzania Youth Coalition (TYC) ndio mtandao wa muungano wa mashirika ya vijana yasiyokuwa ya kiserikali unaounganisha mashirika zaidi ya 120 nchini Tanzania. TYC ni moja ya mashirika yaliyochaguliwa kutekeleza mpango wa kubadilishana vijana kati ya nchi za Tanzania na Ujerumani kwa lengo la kujifunza stadi za kazi mbalimbali.

Mpaka hivi sasa mpango huu umewezesha jumla ya vijana **79 wa Tanzania** kwenda Ujerumani kujifunza kupitia programu ya **weltwärts South North component** katika kipindi hiki kati yao vijana wa kike ni 39 na wa kiume ni 40.

Muungano wa Mashirika ya Vijana (TYC) umefanikiwa kusaini mikataba miwili (2) ya **Corporation/ Technical Agreement na Financial Agreement** ambayo imesainiwa na **GIZ na Eschdorn** ili kuwezesha utekelezaji wa mpango huu nchini Tanzania



# UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

# 14.0. UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

Serikali imekuwa ikifanya jitihada za makusudi za kuwawezesha wanawake kiuchumi ambapo kwa mwaka 2018 Tanzania imeongozwa na kauli mbiu ya Kitaifa inayosema "Kuelekea Uchumi wa Viwanda; Tuimarishe Usawa wa Kijinsia na Uwezeshaji Wanawake Vijijini" ambapo Serikali imejipanga kuwafikia wanawake wengi walioko vijijini kupitia vikundi vya wanawake (SACCOS na VICOBA) na kuwaunganisha na fursa mbalimbali nchini kote sambamba na kuzihamasisha halmashauri zote kutenga asilimia nne (4) ya mapato yake ya ndani ili kuwawezesha wanawake kiuchumi. Takwimu za sasa ni 29% tu ya wanawake hapa Tanzania ambao wanashirki kwenye uchumi rasmi. Wanawake wengi wanajishughulisha zaidi kwenye sekta zinazozalisha kidogo na zenye kasi ya ndogo ya ukuaji, kama vile kilimo na biashara ambazo hazina kasi ya kukua kwa haraka. Sekta zenye kukua kwa haraka ni kama vile fedha, bima, usafirishaji, habari, mawasiliano, uhifadhi wa mizigo na uchimbaji madini.

Sasa hivi ni 4% tu ya wanawake ambao wako kwenye ajira ambazo zina mshahara, kwa wastani wanawake wanapata 35% pungufu ya kipato cha wanaume. Wanawake wengi wanapata taabu sana kupata mikopo kwenye taasisi za fedha, hii inatokana na upungufu wa kipato na kukosekana kwa elimu ya fedha. Matatizo mengine ya wanawake ni kuoanisha maisha ya kazi au biashara na masuala ya familia. Changamoto ya ukosekanaji wa ujuzi wa ujasiriamali, ni ya msingi sana ambapo tunaona kwamba wanawake wengi sana sasa hivi wanajishughulisha na ujasiriamali. Kwa ujumla zaidi ya 55% ya wajasiriamali wa kitanzania ni wanawake.

## 14.1. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UWEZESHAJI WANAWAKE KIUCHUMI

Serikali kwa kushirikiana na wadau kutoka sekta binafsi imewezesha uratibu utekelezaji wa shughuli za uwezeshaji wanawake kiuchumi hapa nchini. Wizara/taasisi za serikali kama Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, TWCC, VOWET, Purple Planet na taasisi ama mashirika mengine zimefanya kazi kubwa sana katika masuala ya uwezeshaji wa wanawake. Pia,

katika programu ya biashara za wanawake za kuvuka mipaka (Cross Border Women Forum) ya TWCC imefanikiwa kuwafikia wanawake **4000** kutoka katika mikoa ya Mtwara, Tanga, Kilimanjaro, Arusha, Mara, Mwanza, Kagera na Kigoma wakati katika Program ya Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi (WEEP) ya Purple Planet imefanikiwa kutoa mafunzo ya kujengea uwezo kwa wanawake zaidi ya **6500** nchini kutoka katika mikoa **14** na kuanzisha vikundi zaidi ya **430** vya kijasiriamali. Purple Planent vilevile inaratibu makampuni 63 ya wanawake.

Hapa chini tunaleta taarifa ya mafanikio ya mwanamke huyu ambaye amepitia vikwazo mbalimbali lakini hakukata tamaa. Bibi Jennifer Bash, ambaye ni mjasiriamali anayetekeleza Sera ya Viwanda na ya Uwezeshaji na ameweza kubadilisha maisha ya wanawake wengine wengi.

## *Vikwazo Mbalimbali Havijaweza Kuua Ndoto Yangu ya Kumiliki Kiwanda*



*Mjasiriamali Jennifer Bash (a.k.a. Mama Alaska) ni mama wa watoto watatu ambaye amekuwa na ndoto ya kuwa mfanyabiashara mkubwa hapa nchini. Jenifer anasimulia kuwa alijifunza na kuambukizwa hamasa ya kufanya biashara na wazazi wake ambao walikuwa wafanya biashara ya mchele na mahindi ndani na nje ya nchi wakati huo akiwa shule ya msingi hadi kidato cha sita ambapo alipenda kuwasaidia wazazi wake katika biashara zao mara anaporudi toka shuleni.Jennifer anaeleza kuwa kujihusisha kwake katika biashara za wazazi wake kulimpatia mbinu mbalimbali za kusimamia biashara kama vile kuzingatia ubora, kujali wateja, bidii ya kazi na kuipenda kazi yake.*

*Jennifer alianza kufuga kuku kwa kushirikiana na mume wake mwaka 2012. Anasema waliamua kufuga kuku kwa sababu waliona kwamba rasilimali kidogo walizokuwa nazo zingewawezesha kufanya biashara hiyo. Biashara hii haikuendelea vizuri sana kwa sababu ya kukosa vitendea kazi kama vile majokofu ya kuhifadhia kuku kabla ya kusambaza kwa wateja wakubwa na hivyo ikawalazimu kubadilisha biashara na kuanza kuuza mayai. Hata hivyo, biashara hii pia waliifanya kwa muda mfupi na kwenda masomoni Marekani pamoja na mume wake na kumuachia meneja aisimamie. Biashara iliyumba zaidi baada ya yeye na mume wake kuondoka. Akielezea changamoto walizopata katika kusimamia biashara hiyo alisema* ***"niweke wazi tu kuwa ilinipa shida sana kusimamia biashara hii nikiwa mbali kwani hata niliporejea nilikuta mambo mengi yameharibika kwa sababu ya kukosa usimamizi wa karibu. Hata hivyo, changamoto hii haikukatisha ndoto zangu bali ilinifanya nifikiri zaidi na kutafuta njia nyingine ya kufikia ndoto zangu. Nilitambua kwamba kutokukata tamaa, kujituma, nidhamu ya biashara na kuwa mbunifu ndiyo siri ya mafanikio".***

*Tuliporudi kutoka Marekani tulikuta biashara yetu inakufa ndipo nikaamua kuifufua. Jennifer kwa kushirikiana na mume wake waliamua kuachana na ufugaji wa kuku na kuanza kushirikiana na wafugaji wa kuku na kuuza mayai katika maduka makubwa (super markets) baada ya kuyaongezea thamani. Anaeleza zaidi kwamba wazo la kuongeza thamani mazao ya kilimo alilipata akiwa nchini Marekani ambapo alijifunza na kuona jinsi ambavyo bidhaa zinafungwa vizuri na kuuzwa katika maduka makubwa nchini humo (super markets). Alitamani kuona maduka makubwa ya Tanzania yakiuza bidhaa zinazozalishwa hapa nchini ambazo wakati huo hazikuwepo katika maduka hayo.*

*Wazo lake la kutamani kuona bidhaa za Tanzania zikiuzwa katika maduka makubwa lilimfanya kufungua kiwanda kidogo cha kuongeza thamani ya mazao ya chakula (mahindi, mpunga na mafuta ya alizeti) katika eneo la Boko Ununio jijini Dar es salaam. Jennifer pia anaongeza thamani ya mayai ya kuku na kuuza bidhaa zake katika maduka makubwa kwa kutumia nembo/chapa yake ya Alaska Tanzania.*

*Changamoto nyingi na kukatishwa tama hazikumzuia kukamilisha ndoto yake ya kuwa mjasiriamali mkubwa. Akieleza zaidi Jennifer anasema* ***"mpaka hapa tulipofika tulilazimika kubuni upya njia za uendeshaji wa kazi hii huku tukilenga soko kubwa zaidi, na huo ukawa mwanzo wa kuzalisha biashara zingine za vyakula".*** *"Ni kweli kuna changamoto nyingi za kimtaji katika hatua za awali lakini tulidhamiria kufunga mkanda na kuhakikisha kuwa ndoto ya*

*kusambaza bidhaa zenye nembo yetu ya Alaska Tanzania inatimia" Anaongeza.*


*Jennifer anafanya kazi hii kwa kushirikiana na wakulima na wafugaji ambao anawapatia elimu ya uzalishaji bidhaa zenye viwango vinavyokubalika katika soko. Mojawapo ya mafanikio makubwa aliyopata katika biashara zake ni kuuza bidhaa zenye nembo yake ya kibiashara pamoja na kutambuliwa na kualikwa katika mikutano mikubwa ya ndani na nje ya nchi ambayo imemtambulisha zaidi na kumuongezea mtandao wa kibiashara. Akieleza zaidi kwa maneno yake anasema* ***"sikuwahi kuota kama naweza kupata mialiko mikubwa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutoa elimu lakini kadri siku zivyonasonga mbele, naona nikiboresha biashara yangu zaidi na kujiimarisha ziadi"***

*Miongoni mwa mambo aliyodhamiria kufanya mwaka huu ni pamoja na kuendesha mafunzo kwa mama lishe wa Dar es salaam ili waweze kuboresha biashara zao na kutengeneza faida.* ***"Nahitaji kurudisha sehemu ya kile nilichokipata kwa jamii, nimepanga kuendesha mafunzo kwa mama lishe ili waweze kujikwamua kiuchuni na kuwa na mawazo mapana kwenye biashara ya chakula".*** *Bash alimalizia kwa kusema kuwa anashukuru Serikali ya awamu hii kwa kupunguza mlolongo wa vibali kwa wajasiriamali wanaoanza biashara kwani vimekuwa vikikwamisha wengi kufanikiwa.*

## 14.2. PROGRAMU YA KUSAIDIA WANAWAKE MKOA WA KIGOMA

Mashirika ya Umoja wa Mataifa yameshirikiana kuanzisha program ya uwezeshaji wa wanawake katika mkoa wa Kigoma. Mashirika haya ni pamoja na UNDP, UNCDF, ILO, ITC, UNWOMEN na UNHCR. Wilaya ambazo zimechaguliwa ni pamoja na Kasulu, Kibondo na Kakonko. Wanawake katika wilaya hizi wengi hujishughulisha na kilimo na biashara ndogondogo ambapo katika wilaya hizo sekta ya kilimo inaajiri wananchi kwa zaidi ya 85%. Kwa sasa familia zinamudu kupata milo miwili tu ambayo haitoshelezi na kiwango cha lishe ni duni. Hali hii inafanya, utapiamlo miongoni mwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano ambao uko juu kuliko wastani wa kitaifa.

***Mchoro 18: Mgawanyo wa majukumu wa programu ya uwezeshaji wanawake Kigoma***




Chanzo: Umoja wa Mataifa

Programu hii itawafikia wanawake wafanyabiashara 3,000 kwenye maeneo ya sokoni katika wilaya za Kasulu, Kakonko na Kibondo. Mpaka sasa vituo vya kijamii 3 vimejengwa katika maeneo ya Nduta, Nyarugusu na Mtendeli. Vilevile vifaa vya TEHAMA vilinunuliwa kwa ajili ya vituo hivi 3. Programu imeanza kujenga masoko mawili ya mpakani na kuanzisha vikundi 53 vya kuweka akiba vyenye wanachama 1246. Vikundi vilivyoanzishwa vitapatiwa mafunzo ya elimu ya fedha na TEHAMA.

Programu pia inalenga kuimarisha ushirika, usindikaji na upatikanaji wa masoko kwa kuwekeza kwenye vituo vya kukusanyia mazao na maghala ili kuboresha muda wa mazao kukaa kwenye maghala ambayo pia itahakikisha usalama wa chakula na malighafi.

Programu pia itajenga uwezo na kutoa msaada wa kiufundi na kifedha ili kuanzisha viwanda vidogo vya kuongeza thamani ya mazao. Pia imesaidia kuwezesha muungano wa wakulima na waongezaji thamani ya mazao ikiwamo kuanzisha kituo cha soko la mihogo huko Kigoma

### 14.3. UTEKELEZAJI WA MFUKO WA MAENDELEO WA WANAWAKE

Katika mwaka wa fedha **2017/2018** Halmashauri zimetenga jumla ya Shilingi **57,080,635,714.70** ambapo, hadi kufikia Februari, 2018 Jumla ya shillingi **15,633,312,764.91** zimetolewa kwa vikundi vya wanawake na Vijana. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Disemba 2017, **Halmashauri 130** kati ya **185** zilichangia **Shilingi bilioni 2.1** katika Mfuko wa Maendeleo ya Wanawake (WDF) kati ya kiasi cha**Shilingi bilioni 26.7** zilizopangwa kuchangiwa kwa mwaka wa fedha 2017/18. Fedha hizo zimetolewa kama mikopo kwa **vikundi 2,919** vyenye jumla ya **wanawake wajasiriamali 29,190.** Aidha, Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi linaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ili kuhakikisha kuwa fedha zinazotengwa zinawafikia vijana na wanawake wengi waliopo vijijini kwa kuainisha takwimu halisi ya wanawake na vijana wanaonufaika na fedha hizo.





# MANUNUZI YA UMMA

# 15.0. MANUNUZI YA UMMA

Baraza limeshirikiana kwa karibu sana na Mamlaka ya Udhibiti wa Manunuzi ya Umma (PPRA). Baada ya kusaini makubaliano ya utekelezaji wa kushirikisha watanzania wengi zaidi katika manunuzi ya umma hasa watanzania wenye kipato cha chini. Mambo mbalimbali yamefanyika.

## 15.1. MWONGOZO WA KUSHIRIKISHA MAKUNDI MAALUM KATIKA MANUNUZI YA UMMA

Mamlaka ya Usimamizi wa Manunuzi ya Umma (PPRA) imetayarisha na kutoa Mwongozo wa kuwezesha makundi maalum kuweza kushirikishwa katika Manunuzi ya Umma yakihusisha Wanawake, Vijana, Wazee na Watu wenye Ulemavu. Mwongozo huo umetoa maelekezo kwa Taasisi zote za umma zinazofanya Manunuzi kuhakikisha angalau asilimia 30 ya manunuzi ya umma yanafanywa na Makundi Maalum na hivyo kutanua wigo wa fursa za Uwezeshaji.

Mwongozo umetoa mgawanyo wa Manunuzi ya Umma kwa makundi maalum kama ifuatavyo;

i. Vijana -10%
ii. Wanawake-5%
iii. Wazee-5%
iv. Watu wenye ulemavu-10%

Mwongozo uliotolewa umeainisha sifa kwa Makundi Maalum yatakayoweza kunufaika (Mtu binafsi au Asasi) ni pamoja na;

i. Kufanya shughuli zao kwa utaratibu wa kisheria na kusajiliwa
ii. Kuwa na Sifa, Uwezo na Uzoefu
iii. Kuwa na uwezo kisheria kuweza kuingia katika mikataba ya Manunuzi
iv. Kusajiliwa na kutambuliwa na Taasisi husika inayosimamia Makundi maalum
v. Kutambulishwa na Taasisi husika inayosimamia makundi maalum kisha kuwekwa katika Daftari maalum la Orodha ya Asasi zinazotambuliwa na PPRA kwa ajili ya kushiriki katika Manunuzi ya Umma

vi. Kuwa na angalau asilimia 75 ya wanachama/wanahisa kutoka katika kundi maalum husika na pia iwe na kiongozi ambaye lazima awe ni wa kundi maalum husika

## 15.2. MFUMO WA MANUNUZI KWA MTANDAO "TANEPS"

Mfumo kamili wa Manunuzi ya Umma kwa njia ya mtandao unaojulikana kwa jina la ''TANePS" umeanza kwa awamu ya majaribio. Mfumo huu, unaojulikana kwa jina la ''TANePS" – yaani "Tanzania National e-Procurement System" unao uwezo wa kuwezesha hatua mbalimbali za manunuzi kufanyika, kuanzia utayarishaji wa mpango wa manunuzi hadi usimamizi wa mikataba. Mfumo huu unaaminika kuboresha manunuzi ya umma hapa nchini na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mfumo umetayarishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ununuzi wa Umma ya Mwaka 2011 na Kanuni za Ununuzi wa Umma chini ya Tangazo la Serikali Na. 446 la Mwaka 2013, ambapo mfumo unawezesha hatua mbalilmbali za manunuzi kufanyika. Mambo yatakayowezeshwa na mfumo ni pamoja na yafuatayo:-

i. Usajili wa watumiaji (User registration);
ii. Mchakato wa zabuni (e-Tendering);
iii. Ununuzi wa bidhaa (e-Purchasing);
iv. Mnada wa mtandaoni (e-Auction);
v. Malipo ya ada mbalimbali (e-Payment); na
vi. Usimamizi wa mikataba (e-contract management).

**Faida za Mfumo wa "TANePS"**

i. Mfumo utaongeza uwazi katika manunuzi ya umma;
ii. Mfumo utasaidia usimamizi wa tozo katika miamala inayohusiana na Zabuni;
iii. Mfumo utaokoa muda unaotumika katika kushughulikia taratibu za zabuni kwa njia ya kawaida (manual); na
iv. Mfumo utasaidia katika kufanikisha masuala ya zabuni kuendana na thamani ya fedha iliyotumika katika kazi husika (Value for money).

## 15.3. USHIRIKI WA WANANCHI KUPITIA MIRADI YA MATENGENEZO YA BARABARA VIJIJINI

Baraza la Taifa la Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi (NEEC) kwa kushirikiana na wadau limeratibu ushirikishwaji wa vikundi vya kiuchumi vya kijamii kuweza kufanya shughuli za ukandarasi wa matengenezo madogo madogo ya barabara hususani zile zilizo katika maeneo ya Vijijini.

Baraza lilishirikiana na Mradi wa IRRIP kupitia taasisi ya CDM-Smith kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Marekani (USAID) limeratibu na kuwezesha ushiriki wa vikundi vya kiuchumi vya kijamii vipatavyo 38 kwa ajili ya kazi za matengenezo ya barabara katika Halmashauri za Kongwa, Kiteto, Mvomero na Kilombero kwenye mradi wa majaribio. Vikundi vimeweza kusajiliwa na Bodi ya Usajili wa Makandarasi (CRB) kwa ajili ya kufanya kazi za matengenezo madogo madogo ya barabara pia vikundi hivyo vimeweza kuunganishwa na TARURA kwa ajili ya kupata kazi za matengenezo hayo kupitia utaratibu wa Manunuzi ya Umma.

Baraza lipo katika mazungumzo na PPRA ili kuona jinsi ya kuwezesha vikundi vingi zaidi vya kiuchumi hapa nchini kushirikishwa katika Manunuzi ya Umma kupitia kazi za matengenezo madogo madogo ya Barabara.

## 15.4. FAIDA ZA USHIRIKISHWAJI WA WANANCHI

i. Kuchochea ukuaji wa ajira kwa kuwa sehemu kubwa ya jamii hususani iliyo katika maeneo ya vijijini kuweza kushirikishwa katika kazi za matengenezo ya Barabara na hivyo kujipatia kipato;

ii. Kusaidia kupitika kwa Barabara hususani zile zilizo katika maeneo ya vijijini kwani shughuli za matengenezo zinaweza kufanyika kwa muda mfupi na kwa ukamilifu kutokana na jamii kuwa ni sehemu ya matunzo ya Barabara; na

iii. Kusaidia Serikali kupunguza Matumizi kutokana na shughuli za matengenezo ya Barabara kufanyika kwa kutumia gharama ndogo, kwa wakati na kwa kutumia teknolojia rahisi isiyohitaji rasilimali kubwa.

## 15.5. USHIRIKISHWAJI WA WADAU KATIKA DHANA YA USHIRIKI WA WANANCHI KATIKA MANUNUZI YA UMMA

Kushiriki kikamilifu kwa wananchi katika shughuli za kiuchumi ikiwamo za matengenezo madogo madogo ya Barabara na kuboresha miundombinu inayosaidia usafirishaji wa watu na mizigo ni kichocheo katika kukuza uchumi na kupunguza umaskini.

Baraza limeweza kuratibu mikutano ya kiufundi iliyowakutanisha wadau kutoka katika taasisi za Serikali na sekta Binafsi kwa ajili ya kujadili na kufanikisha namna bora ya ushiriki wa wananchi katika kazi za matengenezo ya Barabara kupitia vikundi vya kijamii. Taasisi hizo ni pamoja na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, TARURA, PPRA, TAMISEMI, Bodi ya Usajili wa Makandarasi pia baadhi ya Halmashauri zilizo katika mradi wa Majaribio wa IRRIP (Kongwa, Kiteto, Kilombero na Mvomero). Dhumuni kubwa likiwa ni kufungulia njia kwa Mfumo wa ushirikishwaji wa wananchi kupitia vikundi vya matengenezo ya Barabara za vijijini ili hatimaye taratibu za Manunuzi ya Umma ziwezeshe utolewaji wa Zabuni za kazi za Barabara kwa vikundi kupitia TARURA.

Katika makubaliano ambayo PPRA na Baraza ilifanya mwaka jana, yameleta mafanikio yafuatayo:

i. Nyenzo au vigezo vitakavyotumika kutathimini utekelezaji wa utolewaji wa vipaumbele kwa kampuni za ndani na makundi maalum katika shughuli za ununuzi wa umma tayari vimeshaandaliwa;

ii. PPRA kwa kushirikiana na Baraza pamoja na Chemba ya Wafanyabiashara Wanawake (TWCC) ilifanya Warsha ya siku moja kwa ajili ya kuwajengea uwezo wanawake wajasiriamali, ambapo wanawake 36 walishiriki. Huu ni utaratibu ambao utafanyika mara kwa mara ili kufanikisha utekelezaji wa programu za kujengea uwezo kwa makundi maalumu ya kijamii (wanawake, vijana, watoto na watu wenye ulemavu) ili waweze kushiriki kikamilifu katika ununuzi wa umma;

iii. PPRA inajukumu la kufanya tathimini ya hali halisi ya kiwango cha Ununuzi wa bidhaa na huduma zinazozalishwa na makampuni ya ndani na makundi maalumu ya kijamii inayofanywa na taasisi za umma. Tathimini hiyo inategemewa kukamilika mara baada ya ukaguzi wa mwaka wa fedha 2017/2018;